

**KANUNI ZA UPOLE KWENYE VIPINDI, “JAMBO KENYA” NA “CHAPA  
KAZI” VYA REDIO CITIZEN.**

**NA**

**OKETCH LILLIANE ATIENO**

**C50/66650/2013**

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY  
EAST AFRICANA

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA  
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO  
KIKUU CHA NAIROBI**



**A1701440A**

University of Nairobi Library Thesis

2016

**OKTOBA 2017**

## UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu asilia na wala haijapata kuwasilishwa kwa utahini kwa Chuo Kikuu cha Nairobi wala chuo kingine chochote ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika masomo ya Kiswahili.

Jina: Lilliane Atieno Oketch

C50/66650/2013

Sahihi  Tarehe 10/11/17

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Nairobi

Jina: Prof. John Habwe

Sahihi  Tarehe 10/11/2017

Jina: Ms. Mary Ndung'u

Sahihi  Tarehe 10/11/2017



## **TABARUKU**

Tabaruku hii ni kwa mume wangu mpendwa Phelix Odero pamoja na mtoto wangu Eve Shirley Odhiambo.

Na

Wazazi wangu wapendwa Dismas Oketch na Annie R. Oketch.

## SHUKRANI

Kwa dhati ya moyo wangu, namshukuru Mungu Mwenyezi kwa uhai alionipa, neema, hekima pamoja na fadhili zake ambazo hazikadiriki, fadhili ambazo ziliniongoza katika kuikamilisha kazi hii.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. John Habwe na Bi. Mary Ndung'u kwa ukarimu wao. Kwa hakika ukunjufu wa mioyo yenu pamoja na ukarimu wenu ulinisaidia kukamilisha kazi hii. Mtabaki kwenye kumbukumbu zangu daima.

Shukrani zangu vile vile ni kwa wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Maelekezo pamoja na mafunzo yenu yalinipa hamu ya kuikamilisha kazi hii. Wahadhiri hawa ni pamoja na Profesa Iribe Mwangi, Profesa Mwenda Mbatiah, Daktari Prisca Jerono, Daktari Zaja Omboga, Profesa Kineene wa Mutiso, Profesa John Habwe na Daktari Amiri Swaleh. Mwendeleo kuifanya kazi hiyo njema.

Sitawasahau wanafunzi wenzangu ambao kwa pamoja tuling'oa nanga katika bahari hii ya masomo. Ushauri wao ulinitia hamu ya kuendeleza na kuikamilisha kazi hii. Wenzangu hawa ni pamoja na Eunice Alivitsa, Roseline Nyamari, Polycap Adika, Mutali Chesebe, Emily Mosoti, Florence Mukholwe na Jane Ng'ang'a. Daima nitawakumbuka kwa hisani yenu.

Wingi wa shukrani zielekezwe kwa mume wangu mpendwa Phelix Odero pamoja na mtoto wangu Eve Shirley Odhiambo. Uvumilivu wenu ulinipa nguzo wa kuimaliza kazi hii. Maombi yenu ya kila mara yalinipa nguvu ya kuweza kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili. Mungu awape heri kulingana na mapenzi yake.

Siwezi kuwasahau wazazi wangu wapendwa katika shukrani hizi. Baba yangu Dimas Oketch na mama yangu Annie Oketch. Asanteni sana kwa kuonyesha imani katika uwezo wangu. Bila juhudi zenu za kunipeleka shule, singekuwa na fursa ya kuifanya kazi hii. Nawaombeni baraka na siha njema.

Ninawashukuru dada zangu Emilly Oketch, Maurine Oketch, Wayline Oketch, Saywayhive Oketch na ndugu yangu York Massane Oketch kwa kunitia shime ya kuendelea na masomo haya. Sitawasahau pia Jane Kaitlyne Pamoja na Kimberly Anne kwa yote waliyonitendea.

Mwisho ninawashukuru walimu wenzangu ambao walinisaidia katika kuikamilisha kazi hii. Daima nitawashukuru. Walimu hawa ni pamoja na Florence Okut, Philip Oyuga, Fredrick Odongo, Edwin Ogony, Josephine kimeli, Moureen Onyango, Salome Owiti, Anina Ndzovu, Barnabas Onyango, Edith Achieng', Gershom Odhiambo, George Matuli, Patrick Ogat na Alex Ligabo.

Shukrani ziwafikie wale wote walionisaidia kukamilisha kazi hii. Mola awape dua njema.

## IKISIRI

Upole husaidia katika kudumisha mahusiano mema katika mazungumzo. Upole vile vile husaidia katika kuhakikisha kuwa wazungumzaji wanaingiliana vyema katika mazungumzo yao. Wazungumzaji huweza kufahamu kuwa wanatumia mikakati ya upole katika mazungumzo yao lakini mara nyingine, wao huweza kuitumia mikakati ya upole bila wao kufahamu. Tasnifu hii inachunguza kanuni ya upole kwenye vipindi “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha utangazaji cha Redio Citizen. Uchunguzi huu ulinua kuchunguza ikiwa mikakati ya upole inatumika katika mazungumzo na vipindi vya salamu, jinsi kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) zinafanikisha lengo la mikakati ya upole katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” pamoja na kuchanganua elementi za lugha zinazofanikisha matumizi ya upole kwenye mawasiliano. Mchango wa Leech (1983) kwenye nadharia ya upole umetumika katika kuthibitisha kuwa, wazungumzaji kwenye kituo cha Redio Citizen hutumia mikakati ya upole kwenye mazungumzo yao. Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) pia zimetumika katika kubainisha kuwa upole kwa kiwango fulani huweza kusaidia katika kuleta maelewano baina ya wanaohusika katika mazungumzo. Utafiti huu vile vile umethibitisha kuwa mzungumzaji huweza kunyamazia anachokifahamu ili kutoibua mkwaruzano katika mazungumzo. Lazima pawe na upole ili kudumisha mawasiliano katika mitagusano ya kila siku.

## **YALIYOMO**

Ungamo.....	i
Tabaruku.....	ii
Shukrani.....	iii
Ikisiri.....	v

## **SURA YA KWANZA**

1.1 Usuli wa mada.....	1
1.1.1Kuhusu Redio Citizen.....	3
1.2 Tatizo la Utafiti.....	5
1.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.4 Malengo ya Utafiti .....	6
1.5 Sababu ya Kuchagua mada hii.....	7
1.6 Upeo na Mipaka.....	8
1.7 Yaliyoandikwa .....	9
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu Mazungumzo kwenye Redio.....	9
1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Upole.....	12
1.8 Msingi wa Kinadharia.....	14
1.8.1 Taratibu za Kuendesha Lugha Kulingana na Leech (1983).....	15
1.8.1.1 Utaratibu wa Ushirikiano.....	15
1.8.1.2 Utaratibu wa Kinaya.....	15

1.8.1.3 Utaratibu wa Kibanta.....	15
1.8.1.4 Utaratibu wa Upole.....	16
1.8.2 Kanuni za Upole.....	17
1.8.2.1 Kaida ya Mkakati.....	17
1.8.2.2 Kaida ya Ukarimu.....	17
1.8.2.3 Kaida ya Kusifu.....	18
1.8.2.4 Kaida ya Makubaliano.....	18
1.8.2.5 Kaida ya Huruma.....	18
1.9 Mbinu za Utafiti.....	18
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli.....	19
1.9.2 Ukusanyaji wa Data.....	19
1.9.3 Uchanganuzi wa Data.....	19
1.9.4 Uwasilishwaji wa Data.....	19
1.10 Hitimisho.....	20
 <b>SURA YA PILI</b>	
2.0 Dhana ya Upole.....	21
2.1 Utangulizi.....	21
2.2 Upole Kwenye Mawasiliano.....	21
2.2.1 Kanuni ya Kusifu Katika Kufanikisha Mawasiliano.....	23
2.2.2 Kanuni ya Huruma Katika Kuleta Maridhiano Baina ya Wahusika.....	24
2.2.3 Kanuni ya Kujitweza Katika Kuleta Maridhiano Kwenye Mazungumzo.....	24



2.2.4 Kanuni ya Ukarimu Katika Kufanikisha Maelewano Katika Mawasiliano.....	25
2.2.5 Kanuni ya Kukubaliana Katika Kufanikisha Upole Kwenye Mazungumzo.....	26
2.2.6 Kanuni ya Mkakati Katika Kuhakikisha Maelewano Baina ya Wazungumzaj.....	27
2.3 Nadharia ya Uso.....	28
2.3.1 Kauli Zinazotisha Nyuso Chanya za Wasikilizaji.....	30
2.3.2 Kauli Zinazotisha Nyuso Chanya za Wasemaji.....	32
2.3.3 Kauli Zinazotisha Nyuso Hasi za Wasikilizaji.....	33
2.3.4 Kauli Zinazotisha Nyuso Hasi za Wasemaji.....	34
2.4 Matumizi ya Upole Katika Kukabiliana na Vitisho vya Uso.....	35
2.4.1 Kutowasilisha Taarifa.....	36
2.4.2 Matumizi ya Maneno Kiufundi.....	38
2.4.3 Kuafikiana Katika Mazungumzo.....	40
2.4.4 Ucheshi.....	41
2.4.5 Kuepuka Kutoafikiana.....	42
2.4.6 Kutumia Maneno Yenye Maana Fiche.....	43
2.5 Hitimisho.....	44

## **SURA YA TATU**

3.0 Kaida za Upole Katika vipindi “Jambo Kenya na “Chapa Kazi”.....	46
3.1 Utangulizi.....	46
3.2 Kanuni za Ushirikiano (Grice, 1975) Katika Kuibua Upole.....	47
3.2.1 Kanuni ya Ukweli Katika Kujenga Mawasiliano.....	48

3.2.2 Kanuni ya Idadi Katika Kuimarisha Makubaliano.....	50
3.2.2.1 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Idadi Katika Kuleta Maelewano.....	51
3.2.3 Kanuni ya Namna Katika Kuepuka Utata.....	51
3.2.3.1 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Namna Katika Mazungumzo.....	52
3.2.4 Kanuni ya Uhusiano Katika Kufanikisha Kinachosemwa.....	53
3.3 Taratibu za Kuendesha Lugha Katika Mawasiliano.....	54
3.3.1 Matumizi ya Taadhira Katika Kuibua Upole Kwenye Mawasiliano.....	55
3.3.2 Utaratibu wa Kibanta Katika Kuzua Upole Kwenye Mazungumzo.....	56
3.3.3 Matumizi ya Takrima Kama Mkakati wa Upole.....	57
3.3.4 Matumizi ya Tasfida Katika Kuleta Mapatano Kwenye Mazungumzo.....	58
3.3.5 Kujitweza katika Kuleta Maridhiano Kwenye Mazungumzo.....	59
3.3.6 Ufundi wa Kusema Katika Kuleta Ushirikiano.....	59
3.4 Hitimisho.....	60

## **SURA YA NNE**

4.0 Uteuzi wa Elementi za Lugha Katika Kufanikisha Upole Kwenye Mawasiliano.....	61
4.1 Utangulizi.....	61
4.2 Uteuzi wa Vipengele vya Kiisimu Katika Kufanikisha Upole.....	61
4.2.1 Neno.....	62
4.2.2 Virai.....	63
4.2.2.1 Aina za Virai.....	64
4.2.2.1.1 Kirai – Nomino.....	64



4.2.2.1.2 Kirai – Kitenzi.....	65
4.2.3 Vishazi.....	66
4.2.4 Sentensi.....	67
4.3 Uteuzi wa Mbinu za Lugha Katika Kuibua Upole.....	68
4.3.1 Matumizi ya Kinaya Kwenye Mawasiliano.....	68
4.3.2 Matumizi ya Sitiari Katika Kuibua Upole.....	70
4.3.3 Matumizi ya Taswira.....	71
4.3.4 Matumizi ya Chuku.....	72
4.4 Hitimisho.....	72

## **SURA YA TANO**

5.0 Hitimisho.....	74
5.1 Utangulizi.....	74
5.2 Muktasari wa Utafiti.....	74
5.3 Matokeo ya Utafiti.....	76
5.4 Mapendekezo.....	77
<b>MAREJELEO.....</b>	<b>78</b>

Viambatisho

# Sura ya Kwanza

## Utangulizi

### 1.1 Usuli wa Mada

Katika kuwasiliana, watu hutumia lugha kama njia mojawapo ya mawasiliano. Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zenye kubeba maana zilizokubaliwa na jamii ya watu fulani ili zitumike katika mawasiliano. Lugha huweza kuwa nyenzo kuu ya mawasiliano baina ya binadamu. Lugha hutumika mara kwa mara na wazungumzaji pamoja na wasikilizaji kwa sababu lugha huwasilisha dhana, azimio na maarifa.

Lugha huwa na vipashio vyake, vipashio hivyo vikiwa sauti, silabi, neno pamoja na sentensi. Lugha hujengwa kwa maneno. Msingi wa maneno ni sauti moja moja. Sauti hizo ambazo hujenga maneno huitwa vitamkwa. Vitamkwa hivyo, huwa katika mpangilio maalum unaolipatia neno maana. Kati ya vipashio hivi vinne vya lugha vilivyotajwa hapo juu, viwili vitasaidia katika utafiti huu, navyo ni neno pamoja na sentensi. Kwa hivyo, ni muhimu kutambua kuwa, bila lugha watu hawawezi kuwasiliana.

Lugha huwa na dhima tofauti tofauti. Lugha hutumika kama chombo cha mawasiliano kwa kupashiana habari. Lugha hujenga umoja, mshikamano na ushirikiano miongoni mwa wanajamii. Lugha hutunza, hukuza na kuendeleza utamaduni wa jamii. Lugha hutumika kutetea maarifa mbali mbali kwani huwa nyenzo ya kufundishia. Lugha hutumika kama alama ya utambulisho wa jamii au taifa fulani.

Lugha hutumiwa kuleta mtagusano baina ya watu. Watu wa kabila tofauti tofauti huweza kuingiliana kutokana na matumizi ya lugha. Watu hawa huweza kushirikiana kwa sababu ya kuelewana katika mazungumzo, hivyo kazi katika nyanja tofauti tofauti hurahisishwa na kuwepo kwa lugha ambayo huweza kutumika katika mawasiliano. Kurahisishwa kwa kazi kwa sababu ya kuwepo kwa lugha hufanya taasisi mbali mbali kutimiza malengo yao ya kutaka kupitisha ujumbe maalum kwa wateja wao.

Lugha vile vile huwa na sifa zake. Kwanza, lugha lazima iwe inahusu binadamu. Lugha huwa na kipashio kinachojulikana kama sauti. Lugha vile vile hufuata misingi ya fonimu, yaani, huwa na

mpangilio maalum wenye kubeba maana. Mpangilio huo huanza na fonimu, kisha silabi halafu neno. Lugha vile vile hujitambulisha ili kuzalisha maneno mengi.

Lugha huzaliwa, lugha hukua, lugha hufundishika na kuathiriana. Lugha lazima ijitosheleze kimaana na hakuna lugha bora zaidi duniani kwa kuwa lugha zote ni bora mradi, zikidhi matakwa ya jamii husika. Lugha vile vile huweza kufa.

Lugha huwa kigezo cha uwasilishwaji. Kimsingi, lugha ni moja, uwasilishwaji wake ndio huigawa katika tanzu mbili kuu. Tanzu hizi mbili ni lugha ya mazungumzo pamoja na lugha ya maandishi. Lugha ya mazungumzo ambayo itasaidia katika kufanikisha utafiti huu, ni lugha ambayo huwasilishwa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo na hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mazungumzo. Lugha ya mazungumzo ni kongwe, hai na halisi na ina maana nyingi. Lugha ya mazungumzo huwa na stadi zake, stadi hizo zikiwa kuzungumza na kusikiliza.

Crystal (1990) anadai kuwa kitendo cha mawasiliano kimsingi, ni upitishaji wa ujumbe wa aina fulani kutoka kwa mzungumzaji hadi kwa msikilizaji. Ujumbe huweza kuwa wa kufurahisha au hata kuhuzunisha, huweza kuwa wa kuonya au hata wa kutoa mafunzo, lakini licha ya haya yote, lugha huhakikisha kuwa jumbe zote zinawafikia walengwa kwa njia inayofaa.

Dai la Crystal (1990), kuwa mawasiliano huhusu upitishaji wa ujumbe kutoka kwa mzungumzaji hadi msikilizaji linaweza kuthibitishwa na vipindi vinavyopeperushwa kwenye vituo vya utangazaji, kwani, watangazaji huwa na nia ya kupitisha ujumbe maalum kwa wasikilizaji wao, kwani, pasipokuwepo wasikilizaji, basi mawasiliano hayatakamilika. Mawasiliano hukamilika pakiwa na watu wawili au zaidi, ambao aidha wanashiriki katika mazungumzo fulani, au ambao huhukuliwa kama hadhira.

Mawasiliano huweza kuwa mchakato wa kuhamisha taarifa kutoka chombo kimoja hadi kingine. Michakato ya mawasiliano ni mwingiliano unaohusisha ishara kati ya angalau mawakala wawili walio na mkusanyiko wa ishara na sheria za elimu ishara. Mawasiliano kwa kawaida hufafanuliwa kama kupashana au kubadilishana mawazo, maoni au habari kwa maneno, maandishi au ishara.



Ingawa kuna mawasiliano ya njia moja, mawasiliano yanaweza kueleweka vyema kama mchakato kati ya wahusika wawili ambapo kuna mabadilishano na kukuzwa kwa fikra, hisia au mawazo, ili kufikia lengo lililokubaliwa au mwelekeo unaokubaliwa.

Maongezi huhusu mambo mengi, ikiwemo mikakati ya upole ambayo huwa dhana muhimu katika mawasiliano na hata katika pragmatiki; eneo linalodadisi maana kama inavyoeleweka katika muktadha, maana ambayo hutegemea mtumizi wa lugha fulani. Swala hili la matumizi ya maneno yenye upole katika mazungumzo huweza kufanikishwa na vipengele vya arudhi katika lugha kama vile kiimbo.

Kiimbo hufafanuliwa kama kupandishwa au kushushwa kwa mawimbi ya sauti katika usemaji wa lugha. Hivyo, kushusha mawimbi ya sauti katika mazungumzo huweza kudhihirisha upole wa kiwango fulani. Toni ya mzungumzaji pia huweza kudhihirisha upole katika mazungumzo. Maswala haya ya toni na kiimbo hata hivyo, huweza kufanikishwa tu na kuwepo kwa lugha.

Vipengele vingine vya kiisimu kama vile mofimu, virai pamoja na vishazi huweza kusaidia katika kudhihirisha upole katika mazungumzo fulani. Hii ni kwa sababu ndani ya sentensi, mzungumzaji huweza kutumia virai, vishazi au hata mofimu ambazo hudhihirisha upole, huku zikihakikisha kuwa mazungumzo yanafikia malengo yake.

Vishazi hufafanuliwa kama kundi la maneno lenye kiima pamoja na kiarifu. Katika sentensi, kunaweza ibuka kishazi tegemezi au kishazi huru. Kirai ni fungu la maneno ambayo huwekwa pamoja ili kuashiria kitu kimoja. Maneno haya ambayo huwekwa katika kifungu huwa na uhusiano, kwa mfano, nomino na kivumishi katika kauli moja au kitenzi na kielezi katika kauli fulani.

Lazima ikumbukwe kuwa kile ambacho kinafanya binadamu kuwa tofauti na wanyama ni uwezo wao wa kutumia lugha. Kwa hivyo, lugha huweza kutumika katika kutofautisha wanyama na binadamu. Swala hili linadhihirisha umuhimu wa matumizi ya lugha miongoni mwa binadamu.

### **1.1.1 Kuhusu Redio Citizen**

Redio ni chombo cha habari ambacho huwa na uwezo wa kufikia watu wengi, angalau asilimia tisini, kupitia kwa matangazo yake. Redio huwa chombo ambacho si bei ghali hivyo kuifanya kuwa chombo kinachomilikiwa na watu wengi.

Kituo cha Redio Citizen ni mojawapo kati ya vituo vya huduma vya 'Royal Media,' kampuni ambayo hupatikana jijini Nairobi na ambayo ina wasikilizaji wengi. Kituo hiki vile vile kina wafanyikazi wengi wanaofikia mia saba. Hii inamaanisha kuwa, kituo hiki cha Redio Citizen kimewafanya watu wengi kuwa na uwezo wa kujikimu kimaisha kutokana na mapato yao ya kila mwezi, hivyo kukomesha umasikini kwa kiwango fulani.

'Royal Media' ina vituo kumi na viwili vya utangazaji, vituo ambavyo vimeweza kutilia maanani matakwa ya vikundi tofauti tofauti vya watu wanaopatikana nchini Kenya. Kati ya vituo hivyo kumi na viwili, vituo viwili vinatumia lugha ya taifa (Kiswahili) katika kutoa matangazo yao huku vituo kumi vikitoa matangazo kwa kutumia lahaja za kienyeji. Vituo hivyo vya redio ni pamoja na "Bahari fm", "Changei fm", "Vuuka fm", "Egesa fm", "Mulembe fm", "Musyi fm", "Muuga fm", "Ramogi fm", "Radio maa fm", "Inooro fm", "Wimwaro fm" pamoja na "Radio Citizen", kituo ambacho kitasaidia katika kufanikisha malengo ya utafiti huu.

Kituo cha Redio Citizen kimebakia kuwa kituo kikubwa cha redio kikilinganishwa na vituo vingine vya redio. Kituo hiki kina wasikilizaji wengi kwa sababu ya muziki yao yenye kupendeza, programu zao za kuelimisha pamoja na watangazaji wenye ustadi katika utangazaji.

Kituo hiki cha Redio Citizen vile vile kinatoa matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili. Matangazo kwenye kituo cha Redio Citizen vile vile hutolewa kwa kutumia lugha sahili, lugha inayoeleweka kwa wote, waliosoma na wasiosoma, yaani, kituo hiki hakina ubaguzi wa aina yoyote.

Redio Citizen ni mojawapo kati ya vituo vya utangazaji vya radio vya mwanzo kabisa, na ambacho kiliweza kutoa njia mbadala ya kutoa matangazo katika taifa la Kenya katika miaka ya tisini, kwani katika miaka hiyo ya awali, watu wengi walikuwa wakisikiliza matangazo kutoka kwa kituo cha Redio cha "KBC idhaa ya taifa" Programu za kila siku za Redio Citizen zimeweza kufanikisha matarajio ya hadhira yake, wakiwemo vijana kwa watu wazima, wanafunzi, wakulima, wanaspoti pamoja na wafanyi biashara wanaopatikana katika nyanja tofauti tofauti nchini Kenya.

Redio Citizen huanza siku kwa kipindi cha "Jambo Kenya" cha Francis Luchivia, Wilbroda pamoja na Mwala. Kipindi hiki huwapa nuru wasikilizaji wake. Kipindi hiki cha "Jambo Kenya"



hufuatwa na kipindi cha “Chapa kazi” ambacho huwezesha watu walioko katika ajira tofauti tofauti kujadili matukio tofauti ya kila siku katika sehemu zao za kazi.

Kipindi cha vijana kinachofahamika sana kama “Mambo Mseto” pia hupeperushwa wakati wa alasiri, Mzazi Tuva akiwa ndiye mtangazaji. Kipindi cha “Vichekesho” cha Tina Ogal na Abdi hufuata kisha Kamau Munywa huchukua usukani na kuchezea watu muziki pamoja na kuleta mazungumzo katika “Good Evening Kenya.” Mjomba Obachi Machoka huja kila wikendi na kipindi kinachosisimua cha Rogaroga.

Kituo cha Redio Citizen kwa hivyo huburudisha, huelimisha, hutoa maadili kwa jamii, hutahadharisha, huonya na hata kuwapa hadhira yake muda wa kuweza kuchangia majadiliano na kutoa maoni yao kuhusu maswala tofauti yanayoathiri jamii kiuchumi na kisiasa, hasa kwa kutumia lugha ya Kiswahili, lugha ambayo hueleweka kwa wote.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Utafiti huu umechunguza ikiwa maneno yenye kuibua upole hutumika kwenye vituo vya utangazaji, hasa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya Redio Citizen. Utafiti huu vile vile umechunguza vipengele tofauti tofauti vya kiisimu ambavyo vinatumika katika matangazo wa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya Redio Citizen, ili kutoa ithibati ya kuwepo kwa matumizi ya maneno yenye upole katika vipindi hivi viwili vya Redio Citizen.

Ili kuingiliana katika mazungumzo, lazima mikakati ya upole iweze kutumika kwa sababu mikakati hii ya upole hubainisha kukamilika kwa mazungumzo au la. Mikakati hii ya upole huhakikisha kuwa yeyote haudhiki kutokana na mazungumzo yanayoendelea, jambo ambalo limethibitishwa na utafiti huu.

Utafiti huu umetathmini kanuni ya upole kwenye matangazo ya Kiswahili katika kituo cha Redio Citizen. Kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu mikakati ya upole katika vituo vya utangazaji, moja wapo ikiwa utafiti kutoka kwa runinga ya Citizen, utafiti ambao ulifanywa na Raitani A. M. Raitani alifanya utafiti kutoka katika kipindi cha Bi. Msafwari kinachoendeshwa kwa lugha ya kiswahili.

Kuna maswali ambayo nilitamani kuyafanyia utafiti ili niweze kupata majibu yao. Majibu ambayo yamepatikana katika utafiti huu wa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya

kituo cha Redio Citizen yamesaidia katika kuziba pengo la umuhimu wa matumizi ya mikakati ya upole katika maongezi, suala ambalo kwangu mimi, halikushughulikiwa na watafiti wa hapo mwanzoni. Maswali haya ni pamoja na:

Je, mikakati ya upole inatumika katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa kazi” vya Redio Citizen? Na ikiwa mikakati ya upole inatumika katika vipindi hivi, mikakati hii inaweza kujulikana bayana? Je, kuna umuhimu wa kutumia mikakati ya upole katika vipindi hivi viwili? Wanaotumia mikakati ya upole huwa na lengo gani wanapotumia mikakati ya upole katika maongezi yao?

Kwa maoni yangu, hakuna utafiti umefanywa kuhusu vipindi vya salamu katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen, hasa kwa kuangazia vipindi vya “Jambo Kenya” pamoja na kile cha “Chapa Kazi”. Mazungumzo katika vipindi hivi viwili hufanyika kwa namna ambayo hufanya wazungumzaji na wasikilizaji kuingiliana katika mazungumzo yao.

### **1.3 Maswali ya Utafiti**

Maswali ya utafiti huu ambayo yanaibuka kutokana na tatizo la utafiti ni pamoja na:

1. Je, watangazaji wa kituo cha Redio Citizen hutumia mikakati ya upole katika matangazo yao?
2. Ni kanuni zipi za upole zinatumiwa katika upeperushwaji wa habari katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio citizen?
3. Vipengele vipi vya kiisimu hufanikisha matumizi ya upole kwenye mawasiliano?

### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kufanikisha baadhi ya mambo ambayo hayajaweza kutafitiwa na watafiti wa hapo mwanzoni, hasa kanuni ya Upole kwenye matangazo ya Kiswahili katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya Redio Citizen. Malengo ya utafiti huu ni:

1. Kubainisha mikakati ya upole inayotumiwa katika mazungumzo na vipindi vya salamu.
2. Kubainisha jinsi kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) zinafanikisha lengo la mikakati ya upole katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”, vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha Redio Citizen.



3. Kuchanganua elementi za lugha zinazofanikisha matumizi ya upole kwenye mawasiliano.

### **1.5 Sababu ya Kuchagua Mada Hii**

Utafiti huu umechunguza Kanuni ya Upole kwa kujikita katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vinavyopeperushwa katika kituo cha Radio Citizen kwa sababu ya lugha ambayo hutumika katika uwasilishwaji wa vipindi hivi, lugha hiyo ikiwa ni Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya taifa na ambayo inaeleweka kwa waliosoma na wasiosoma. Kwa hivyo, lugha hii ya Kiswahili huleta watu pamoja na haibagui kwa vyovyote vile, huku kikitumika na watangazaji katika kituo cha Redio Citizen kufahamisha wasikilizaji kuhusu maswala muhimu ya kijamii, hasa kiuchumi na kisiasa.

Sababu nyingine ya kuteua mada hii ni kuwa, vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha Redio Citizen hutolewa kwa njia iliyo wazi na ambayo hutia maanani hisia za wasikilizaji, hisia hizi zikiwa hisia hasi pamoja na hisia chanya za watangazaji pamoja na wasikilizaji wao.

Katika kujali hisia za wale wanaohusika katika mazungumzo, nyuso zao huhifadhiwa, jambo ambalo lilinipa msukumo kufanya utafiti huu. Aidha kwa mujibu wa utafiti huu, hakuna utafiti wowote unaohusu mikakati ya upole kwenye vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio Citizen ambao umewahi kufanywa, hivyo ari ya kutaka kuziba pengo hili ilinifanya kufanyia suala hili utafiti.

Vipindi vilivyoteuliwa kupeperushwa kwenye kituo cha Redio Citizen vina umuhimu katika jamii. Hii inatokana na malengo ya kituo hiki ya kuzungumzia mambo muhimu na kuhakikisha kuwa ujumbe muhimu tu ndio unaopitishwa kutoka kwa mtangazaji hadi msikilizaji. Vile vile wale watangazaji huhakikisha kuwa wamehifadhi nyuso hasi na nyuso chanya za wahusika.

Hali kadhalika, utafiti huu unaweza kuchangia katika kukua kwa taaluma ya Kiswahili. Baada ya kudhihirisha kuwa kituo cha Redio Citizen huokoa nyuso hasi na nyuso chanya za wahusika hasa kwa kutumia maneno yenye upole katika matangazo yao, watu wengi watatiwa moyo na watakuwa na hamu ya kusikia vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha Redio Citizen kwa sababu nyuso zao zitahifadhiwa, huku wakijifunza lugha hii ya Kiswahili kupitia kwa matumizi ya Kiswahili sanifu kwenye kituo hicho. Watu wengi kwa hivyo, wataweza kutumia lugha hii ya



Kiswahili katika mazungumzo yao, jambo litakalofanya Kiswahili kukua na lugha ya Kiswahili kitatukuzwa.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umeangazia vipindi maalum ambavyo vinapeperushwa katika kituo cha Redio Citizen. Vipindi hivi ni pamoja na kipindi cha “Jambo Kenya” kinachopeperushwa na Wilbroda, Mwala, Munai pamoja na Francis Luchivia. Kipindi cha pili ni kile cha “Chapa Kazi” kinachopeperushwa na Jerida Andai na Syombua Mwele. Vipindi hivi vilivyoteuliwa vina mada nyingi ambayo imesaidia katika kuthibitisha kuwa vituo vya utangazaji hutumia upole katika matangazo yao. Vipindi hivi vile vile vimenipa data ya kutosha katika utafiti huu, huku vikihakikisha kuwa malengo ya utafiti huu yametimizwa kikamilifu.

Vipengele vya kiisimu ambavyo vimeshughulikiwa katika utafiti huu ni maneno, sentensi, mofimu, vishazi na virai, vipengele ambavyo vinatumika na watangazaji wa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”. Vipengele hivi ambavyo viliteuliwa huweza kudhihirisha upole katika mazungumzo.

Utafiti huu umefanikishwa na Nadharia ya Upole iliyoasisiwa na Geoffrey Leech (1983). Hata hivyo, utafiti huu umeangazia taratibu mbali mbali za kuendesha lugha, taratibu ambazo zilichanganuliwa na Leech (1983), taratibu zinazosaidia katika kuhakikisha kuwa mawasiliano yametimizwa kwa njia inayofaa.

Utafiti huu haujaegemea kwenye vipindi vya muziki pamoja na vipindi vya majadiliano baina ya watangazaji na wasikilizaji wao kwa sababu mijadala hii hukosa mielekeo. Vile vile kutabiri kile ambacho kinazungumziwa hutatiza kwa sababu wazungumzaji hubadilisha mada mara kwa mara. Vile vile, maswala ya kisayansi huhitaji kuwa mambo yaweze kutajwa jinsi yalivyo, na kuwa maneno mbadala yasiweze kutumika. Kwa hivyo, huwa jambo la kutatiza kupata maneno yenye upole katika mambo ya kisayansi, ndipo vipindi hivi havitashughulikiwa katika utafiti huu.

Vipindi vingi katika kituo cha Redio Citizen hudhihirisha upole, lakini vipindi viwili tu ndivyo vimeshughulikiwa kwani vipindi hivyo vyote vingeshughulikiwa, muda haungetosha hivyo,

utafiti huu ungeacha pengo ambalo lingehitaji kuzibwa baadaye. Vipindi viwili ambavyo vimeshughulikiwa ni “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi.”

## **1.7 Yaliyoandikwa**

Kuna mengi ambayo yameandikwa kuhusu mazungumzo kwenye vituo vya utangazaji vya Redio. Vile vile, kuna watafiti ambao tayari washashughulikia suala la mikakati ya upole, na jinsi ambavyo mikakati hii ya upole hutumika katika mazungumzo, hasa kwenye mazungumzo katika vituo vya utangazaji. Sehemu hii, hivyo basi imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mazungumzo kwenye Redio, pamoja na yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Upole.

### **1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mazungumzo kwenye Redio**

Tafiti nyingi ambazo zimefanywa zimeshughulikia mikakati ya upole katika mazungumzo kwenye vipindi mbalimbali vinavyopeperushwa kwenye redio. Redio ni chombo cha habari ambacho huwa na uwezo wa kufikia watu wengi sana kwa wakati mmoja. Angalau asilimia themanini ya wananchi kwa jumla, humiliki chombo hiki cha utangazaji kwa sababu si bei ghali, pia huwa rahisi kupatikana katika soko.

Coates (2004:105) anadai kuwa katika muktadha wa mazungumzo ambayo huendelezwa katika vituo vya utangazaji vya redio, mhojaji hujaribu kuokoa uso chanya wa mhojiwa kwa kumsalimia kwanza na kumuuliza anavyoendelea kabla ya kuingilia mada kuu kwenye mazungumzo.

Salamu zinazopitishwa kwa msikilizaji humfanya kuhisi kuwa amekaribishwa na yule mtangazaji, na kuwa yuko huru kuchangia katika mjadala unaoendelea. Swala hili vile vile humfanya msikilizaji kuwa huru, hivyo huweza kusema mambo kwa njia wazi, bila kuficha chochote anachofahamu kuhusu suala linalojadiliwa.

Thimm et.al (2004: 539) anasema kuwa lengo la salamu ambayo huelekezwa kwa msikilizaji huweza kuelezwa kama mikakati ya kujaribu kuokoa wadhifa wa mtu fulani. Mikakati ya kudumisha uhusiano hutumika na watangazaji ili kuhakikisha kuwa wanaendeleza uhusiano mwema. Vile vile, wao hudhibiti maingiliano yao kwa kutumia mkakati huu.

Msikilizaji kwa hivyo, huweza kudumisha uhusiano wake na mtangazaji yeyote kwa kutumia majina yao ya kibinafsi na kuwauliza maswali ambayo hayawapi hofu, yaani, maswali yasiyowatia shaka katika hali yoyote. Maswali ambayo hayaingilii maisha ya kibinafsi ya mtangazaji au hata msikilizaji kwa vyovyote vile.

Gee (2005:95) anadai kuwa uchanganuzi wowote wa kipragmatiki unaohusu maneno teule katika utafiti, na unaohusu mikakati ya upole katika kituo cha redio, huchukuliwa kuwa kamilifu ikiwa muktadha wa mazungumzo yanayoendelezwa katika vituo hivyo tofauti tofauti vya redio vimetiwa maanani.

Muktadha wa mazungumzo hutegemea wale wanaozungumziwa, kwa mfano, ikiwa wale wanaopitishiwa ujumbe ni vijana, basi itambidi mzungumzaji kutumia maneno teule yenye upole, lakini ambayo yanatoa maarifa kwa wale vijana. Maneno ambayo huteuliwa vile vile lazima yawe yale ambayo huweza kunasa makini ya vijana lengwa, huku ujumbe muhimu ukipitishwa kupitia kwa maneno yale yaliyoteuliwa. Kwa ufupi, lugha ya vijana hutumika ili kuweza kupitisha ujumbe muhimu kwa vijana.

Tolson (2006:29) anadai kuwa mijadala pamoja na mazungumzo katika radio yanajengwa kulingana na matarajio fulani ya wasikilizaji, matarajio ambayo hutokana na picha inayochorwa na vipindi vinavyopeperushwa katika vituo vya utangazaji.

Kuna yale mambo ambayo wasikilizaji hutarajia kusikia kutoka kwa vituo tofauti tofauti vya utangazaji vya redio. Vipindi mbalimbali huweza kuchora picha za aidha machukizo au upendo katika akili za wasikilizaji. Picha inayochorwa akilini mwa msikilizaji huwa na athari kubwa kwa kituo cha utangazaji kwani huweza kuwafanya wasikilizaji aidha kupenda au kuchukia kituo cha utangazaji.

Kwa mfano, ikiwa mtangazaji anashughulikia maswala ya kiuchumi, msikilizaji atatarajia kuwa aweze kuelezwa maswala yanayohusishwa na ukulima, bei ya vyakula, maswala ya kunyesha kwa mvua, pamoja na mambo muhimu ambayo huchangia pakubwa katika kuhakikisha kuwa binadamu anaishi maisha mazuri.



Kwa hivyo, mtangazaji hupaswa kujua yale ambayo hutarajiwa na wasikilizaji wake, hasa kutoka kwa vipindi tofauti tofauti vinavyopeperushwa na vituo vya utangazaji. Matarajio haya yakitiwa maanani, na maneno ya kuokoa nyuso kutumika, vituo vya utangazaji vitaweza kupata umaarufu usiopigiwa mfano. Mhojaji huuliza mhojiwa maswali na kuhakikisha kuwa mazungumzo yanaendelea huku mhojiwa akitarajiwa kujibu maswali anayoulizwa na mhojaji.

Tolson (2006:30) anaendelea kusema kuwa idadi ya mahojiano tofauti tofauti yanayoendelezwa katika vituo vya redio imeongezeka na kufanya mijadala katika redio kukosa urasmi. Wahojiwa hujaribu kuwa wabinafsi na kuathiri mielekeo ya mazungumzo. Wahojiwa hushirikisha wahojaji katika mazungumzo na mijadala kwa kutaja majina yao na kuwauliza maswali ambayo wakati mwingine, hufanya mazungumzo kuchukua mkondo tofauti na ule uliodhamiriwa.

Tolson (2006) anajadili mikakati ya huruma kama ile inayofanya mzungumzaji kuteua maneno fulani katika mazungumzo, maneno ambayo hudhamiria kuhakikisha kuwa majibu chanya yanapatikana kutoka kwa msikilizaji. Licha ya kuhakikisha kuwa majibu chanya yanapatikana kutoka kwa msikilizaji, uteuzi wa maneno katika mazungumzo hudumisha uhusiano mwema kati ya mtangazaji na msikilizaji wake.

Uteuzi wa maneno huweza kusaidia pakubwa katika kuokoa nyuso hasi na nyuso chanya za wazungumzaji pamoja na wasikilizaji. Kuokolewa kwa nyuso hasi na nyuso chanya za wahusika huwafanya kutoaibika. Vile vile huwafanya wale wanaohusika katika mazungumzo kuhusika katika mazungumzo yale bila hofu, bila woga, hivyo kufanya mawasiliano kukamilika. Kwa hivyo, salamu inawakilisha mikakati ya kuokoa uso huku ikisaidia watangazaji kualika wasikilizaji katika mazungumzo na vile vile, kuokoa uso chanya ya wasikilizaji wake.

Young (2008:2) anasema kuwa, watu wanaojitambulisha na utamaduni na desturi fulani, wakishiriki katika mazungumzo yanayoendelezwa katika vituo tofauti tofauti vya redio, huchukua nafasi ya kujihusisha katika maswala ya kiisimu. Ni muhimu sana kutoa maelezo ya aina mbalimbali za maneno, virai, vishazi na hata sentensi ambazo hutumika katika vituo vya radio. Vile vile, ni muhimu kuonyesha maana inayokusudiwa na maneno, virai, vishazi na hata sentensi ambazo zinatumiwa katika vituo hivyo vya utangazaji.

Kuonyeshwa kwa maana ya maneno, virai, vishazi pamoja na sentensi ambazo huteuliwa na kutumika katika kupeperusha habari, husaidia wasikilizaji kuweza kuelewa umuhimu wa matumizi ya lugha yenye upole katika maongezi. Kuwa, lugha hiyo iliyojaa upole huwasaidia wale wazungumzaji kudumisha uhusiano mwema na wasikilizaji wao, pamoja na kuokoa nyuso hasi na nyuso chanya zao, huku malengo ya mazungumzo yale yakifikiwa.

Hawa ni baadhi ya wataalamu ambao walitoa mchango wao kuhusu mazungumzo kwenye Redio. Mawazo yao ambayo yameshughulikiwa hapo juu ni muhimu kwani, yaliweza kutumika na watafiti wengine katika kufanikisha tafiti zao. Mawazo haya ya wataalamu mbalimbali yamewaongoza baadhi ya watafiti katika utafiti wao, utafiti mojawapo ukiwa wa Raitani A. M, utafiti aliofanya kutoka kwa runinga ya Citizen. Raitani alifanya utafiti kutoka katika kipindi cha Bi. Msafwari kinachoendeshwa kwa lugha ya kiswahili, Raitani akionyesha kuwa vituo vya utangazaji hutumia maneno yaliyoteuliwa, na yenye upole wa kiwango fulani.

Katika runinga ya Citizen kwa mfano, Kulingana na Raitani, Bi. Msafwari anateua maneno katika mazungumzo yake. Anne anatoa mfano wa wanawake kuitwa 'Type writer' na Bi. Msafwari katika kipindi cha kukinai ndoa. Bi. Msafwari anateua maneno haya anapotoa ushahidi kuwa kuna kile kinachowapa wanawake msukumo kupiga kelele wakiwa nyumbani. Asema kuwa, anayechapisha makala kwa kutumia taipureta ndiye huifanya kupiga kelele, kwa hivyo, kuna kile kinachomfanya mwanamke kupiga kelele katika nyumba yake.

Vile vile kulingana na Raitani, Bi. Msafwari katika kipindi cha ushindani wa watoto anapunguza vitisho kwa nyuso chanya ya wasikilizaji anaposema, "Ni babake naelewa kweli lakini kuna vingine ambavyo havitakikani kuonwa na baba." Bi. Msafwari anateua maneno anayotumia katika sentensi yake ili kuonyesha kuwa baba hafai kumwogesha binti yake kwani kuna sehemu za mwili wa mtoto msichana ambazo baba yake hafai kuziona. Utafiti wa Raitani A. unaonyesha jinsi wazungumzaji huteua maneno katika mazungumzo yao pamoja na lengo la mzungumzaji kuteua maneno katika mazungumzo yake.

### **1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Upole**

Upole ni dhana inayoongoza uhusiano uliopo baina ya wazungumzaji na wasikilizaji wao. Upole huibua hali ya maridhiano katika mawasiliano, huku ukihakikisha kuwa mawasiliano



yameendelea bila mkwaruzano wowote. Vile vile, upole huhakikisha kuwa malengo ya mawasiliano yametimizwa.

Leech (1983: 82) anadai kuwa, matumizi ya upole kwenye mawasiliano huwa njia ya kutengana na mgongano wa aina yoyote katika mawasiliano. Leech (1983) anaendeleza dai lake kwa kusema kuwa jukumu la mikakati ya upole ni kuhakikisha kuwa kuna usawa katika mawasiliano ya kijamii, pamoja na kudumishwa kwa uhusiano mwema baina ya wazungumzaji na wasikilizaji.

Madai haya ya Leech (1983) yamesaidia sana katika utafiti huu kwa sababu, baadhi ya watangazaji wa Kituo cha Redio Citizen hujaribu kuhakikisha kuwa wanatumia mikakati ya upole katika mazungumzo yao ili kuepukana na migogoro inayoweza kuibuka kati yao na wasikilizaji wao.

Leech (1983: 131) anasisitiza kuwa lazima kuwe na watu wawili au zaidi kwenye mazungumzo; aidha mzungumzaji na msikilizaji au mzungumzaji na wasikilizaji. Kuna baadhi ya mambo ya kimsingi katika mawasiliano. Kwanza, mzungumzaji huwa muhimu katika mawasiliano yoyote, msikilizaji vile vile hudhihirisha umuhimu katika mawasiliano. Upole huwa elementi ya tatu ambayo hubainisha kukamilika kwa mawasiliano baina ya watu wawili au zaidi.

Leech (1983) vile vile alidai kuwa, upole huhusu uhusiano baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Mzungumzaji huonyesha upole kwa msikilizaji wake pamoja na wale wote ambao hawahusiki katika mazungumzo hayo. Kuwa, mikakati ya upole hupunguza ukali wa maneno pamoja na athari ya kutumika kwa maneno ambayo hayana upole. Kwa hivyo, mikakati ya upole huangazia mchakato wa utafsiri kwamba, kiini cha matumizi ya maneno yenye upole kwenye mazungumzo ni kuibuka na matokeo chanya kutoka kwa msikilizaji.

Fraser (1990: 232) anasema kuwa watu wanapoingilia mazungumzo yoyote, kila mmoja wao huwa na matarajio fulani kutoka kwa mwenzake. Fraser (1990) anadai kuwa upole huleta maridhiano baina ya wanaohusika katika mazungumzo, na kuwa, wale ambao huhusika katika mazungumzo hulazimika kubadilisha mkondo wa mawasiliano, hasa ikiwa mkondo wa mawasiliano uliotumika awali ni tishio kwa uso wa mmoja wao.

Madai ya Leech (1983) yanakaribiana na yale ya Mills (2003). Mills (2003: 6) anadai kuwa upole huweza kuwa maelezo ya madhumuni ya mzungumzaji ambayo hupunguza makali ambayo huweza kufedhehesha au hata kuudhuru uso wa yeyote ambaye anahusika katika mazungumzo.

Brown na Levinson (1978, 1987) wanadai kuwa mikakati tofauti tofauti ya upole husaidia katika kudumisha uhusiano mwema baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Brown na Levinson (1978, 1987) wanasema kuwa mikakati hii ya upole husaidia katika kuokoa nyuso za wahusika, kwa sababu nyuso za wahusika lazima zihifadhiwe katika hali zote.

Brown na Levinson (1978) wanatumia madai ya Paul Grice (1975), kuwa wote ambao huhusika katika mazungumzo hutaka ujumbe kupitishwa kwa njia inayotosheleza kwa kusema kuwa, watu wote wanaohusika katika mazungumzo huchagua mikakati sawa ya upole katika kuendeleza mazungumzo yao, na kuhakikisha kuwa mazungumzo yanatimiza mahitaji yake. Hii husababishwa na mahitaji ya wanaozungumza kuwa, nyuso zao zikolewe katika mazungumzo hayo.

Kauli hii ya Brown na Levinson (1978, 1987) na ya Leech (1983) imesaidia katika harakati ya utafiti huu kuonyesha kuwa maneno yenye upole yanayotumika katika mazungumzo huwa na dhamira ya sio tu kuokoa nyuso za wanaohusika katika mazungumzo, bali pia kuhakikisha kuwa malengo ya mazungumzo yametimizwa.

## **1.8 Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Upole ambayo iliasisiwa na Geoffrey Leech (1983). Leech (1983: 82) anadai kuwa, matumizi ya upole kwenye mawasiliano huwa njia ya kutengana na mgongano wa aina yoyote katika mawasiliano.

Leech (1983) anaendeleza dai lake kwa kusema kuwa jukumu la mikakati ya upole ni kuhakikisha kuwa kuna usawa katika mawasiliano ya kijamii, pamoja na kudumishwa kwa uhusiano mwema baina ya wazungumzaji na wasikilizaji. Leech aliibuka na taratibu za kuendesha lugha, hivyo, utafiti huu umejikita katika taratibu za kuendesha lugha kama ilivyodaiwa na Leech (1983).

### **1.8.1 Taratibu za Kuendesha Lugha Kulingana na Leech (1983)**

Leech (1983) katika kutoa mchango wake kuhusu Nadharia ya Upole alisema kuwa, utaratibu wa ushirikiano pekee hautoshi kueleza lugha inavyoendeshwa. Leech vile vile alisema kuwa mtagusano wa mazungumzo una taratibu zake, taratibu ambazo zinasaidia katika kutoa maelezo ya jinsi lugha inavyoendeshwa, hasa katika harakati ya mawasiliano, taratibu hizo kulingana na Leech (1983) ni pamoja na:

#### **1.8.1.1 Utaratibu wa Ushirikiano**

Utaratibu huu huhitaji mzungumzaji kushirikiana na msikilizaji ili waweze kuelewana katika mazungumzo. Utaratibu huu vile vile huhakikisha kuwa mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji yametekelezwa kama ilivyokusudiwa. Mzungumzaji hushirikiana na msikilizaji katika mazungumzo yoyote ile, ili waweze kuonekana kama kitu kimoja.

Utaratibu huu umeweza kujibu swali la lengo la mzungumzaji katika kuteua maneno katika maongezi yake. Kuwa, wazungumzaji huwa na lengo fulani katika maongezi yao, lengo kuu likiwa ni kupitisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia inayotosheleza.

#### **1.8.1.2 Utaratibu wa Kinaya**

Utaratibu huu huashiria kuwa mzungumzaji husema mambo kinyume na anachomaanisha. Mambo husemwa kinyume ili kuhifadhi uso wa msikilizaji, huku ujumbe ukipitishwa kama ulivyokusudiwa. Utaratibu huu vile vile huhakikisha kuwa hakutokei mkwaruzano kati ya mzungumzaji na msikilizaji wake, hivyo kudumisha amani. Utaratibu wa kinaya umesaidia katika kujibu swali la ikiwa watangazaji wa vipindi vya “Jambo Kenya” pamoja na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio Citizen, hutumia mikakati ya upole katika maongezi yao ya kila siku.

#### **1.8.1.3 Utaratibu wa Kibanta**

Utaratibu huu huhusu lugha inayotumika kwa makali lakini lugha yenyewe huashiria upole. Maneno makali huweza kutumika katika mazungumzo yoyote, lakini jinsi mzungumzaji anavyoyatamka maneno hayo yenye makali huweza kudhihirisha upole kwa kiwango fulani. Haya yanaelekezwa katika kupandishwa na kushushwa kwa mawimbi ya sauti wazungumzaji wakiwa katika harakati ya mazungumzo.



Utaratibu wa kibanta umebainisha vipengele vya kiisimu ambavyo vinasaidia katika kufanikisha kanuni ya upole kwenye mawasiliano, hasa katika vituo mbali mbali vya utangazaji.

#### **1.8.1.4 Utaratibu wa Upole**

Huu ni utaratibu ambao hufanya mawasiliano kukamilika. Mawasiliano hukamilika kwa sababu kanuni ya upole huelekeza watu kutumia lugha inayoficha ukweli fulani. Watu huweza kutumia maneno fulani bila uwazi kwa sababu ya kukosa ushahidi wa kisheria. Kuficha ukweli katika mawasiliano au kutosema maneno fulani kwa njia wazi, husaidia katika kutambua lengo la wazungumzaji katika kuteua virai, vishazi na maneno katika harakati ya kuwasiliana.

Kuna aina tatu za upole. Kuna upole ambao hutarajia mtu kutumia lugha fiche kwa sababu hana ushahidi wa kutosha kuhusu mada anayozungumzia. Kuna upole unaotumika ili mtu asijitie matatani kutokana na matamshi yake katika mazungumzo fulani. Kuna upole unaodhihirisha heshima. Kwa mfano, mtu anapotumia neno najisi badala ya kubaka katika matamshi yake, anadhihirisha heshima katika kauli yake.

Nadharia ya Upole huhusu uhusiano kati ya mzungumzaji na anayezungumziwa. Upole huibua hali ya maridhiano na maelewano katika mawasiliano. Vile vile, upole hupendekeza jinsi ya kubuni na kuelewa lugha hasa katika mawasiliano.

Upole ni namna ya kuonyesha heshima kwa wengine katika mazungumzo. Heshima inayoonyeshwa kwa wasikilizaji pamoja na watangazaji kupitia kwa matumizi ya maneno yenye upole, huhakikisha kuwa ujumbe unaodhamiriwa unafikia hadhira lengwa, na vile vile malengo ya mawasiliano yamehitimu.

Kusudi la mikakati ya upole katika mawasiliano ni kuhakikisha kuwa kuna uhusiano mzuri baina ya watu katika jamii. Mikakati ya upole huhakikisha kuwa mawasiliano yanatimiza mahitaji yake. Goffman (1967) anadai kuwa, upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kupitia kutimiza au kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo.

Grice (1975) anadai kuwa, watu wote ambao huhusika katika mazungumzo kimsingi, hutaka ujumbe kupitishwa kwa njia inayotosheleza. Brown na Levinson (1978) wanatumia dai hili la Grice katika Nadharia yao ya Upole kwa kusema kuwa watu wote wanaohusika katika mazungumzo huchagua mikakati sawa ya upole katika kuendeleza mazungumzo yao na

kuhakikisha kuwa mazungumzo hayo yametimiza mahitaji yake, kwa sababu mikakati tofauti ya upole inapotumika katika mazungumzo, huweza kudhuru uso wa aidha mzungumzaji au msikilizaji. Kwa hivyo, mikakati ya upole inahusu ufafanuzi wa athari ya maongezi yanayoelekezwa kwa msikilizaji zaidi ya mzungumzaji.

## **1.8.2 Kanuni za Upole**

Watangazaji pamoja na wanaohusika katika mijadala tofauti tofauti hutarajiwa kutumia kanuni mbalimbali za mikakati ya upole ili kuweza kuhifadhi mahusiano yaliyopo kati yao na wasikilizaji wao. Kanuni hizo za Nadharia ya Upole zinazoelezwa hapa chini ndizo zimesaidia kukamilisha utafiti huu.

### **1.8.2.1 Kanuni ya Mkakati**

Kaida hii huhusu maongezi ambayo humsababisha msikilizaji kufanya jambo fulani ambalo hakunua kulitenda. Kaida hii huhusu kupunguza gharama kwa mmoja huku manufaa yakimwendea yule anayezungumziwa.

Kwa mfano, mtu anapoambiwa, “Je, hutaketi?” Mzungumzaji anaonyesha kuwa, kule kuketi kunamfaidi tu yule anayezungumziwa, kwa hivyo kutokana na matumizi ya kaida ya upole kwenye usemi huu, manufaa yanamwendea yule anayezungumziwa, huku mzungumziwa akilazimika kutenda jambo ambalo pengine hakunua kulitenda, kitendo hicho kikiwa ni kuketi.

### **1.8.2.2 Kanuni ya Ukarimu**

Kaida hii hudhamiria kuonyesha kuwa anayezungumziwa huwa na uwezo wa kutenda jambo fulani. Kaida hii ya ukarimu huagiza wazungumzaji kutosema au kutotumia maneno au hata sentensi ambazo huweza kukasirisha wasikilizaji. Kwa hivyo, kaida hii hutarajia kwamba wazungumzaji waweze kuonyesha wanaowasiliana nao kila mara kwamba wana ukarimu wa kiwango fulani.

Kwa mfano, mzungumzaji anapomwambia msikilizaji wake kuwa, “Lazima uje leo ili tule chajio pamoja,” mzungumzaji yule huonyesha ukarimu kwa yule msikilizaji, na kuwa yule msikilizaji ndiye atafaidika kutokana na kitendo kile cha ukarimu.

### **1.8.2.3 Kanuni ya Kusifu**

Kaida hii huagiza wale ambao hujihusisha katika mazungumzo kutojisifu na kuhakikisha kuwa sifa zinawaendea wengine. Katika kaida hii, manufaa yanamwendea msikilizaji. Kaida hii vile vile humpa mzungumzaji ushauri wa kutosema mambo yasiyowapendeza wasikilizaji wake. Mzungumzaji anaposema kuwa uigizaji fulani ulikuwa wa kupigiwa mfano, anatoa kauli nzuri kuhusu uigizaji ule, hivyo anasema maneno yenye kupendeza, na ambayo hayachukizi.

### **1.8.2.4 Kanuni ya Makubaliano**

Kaida hii hunuia kutahadharisha wale ambao wanashiriki katika mazungumzo kuwa, huwa ni muhimu kukubaliana watu wanapowasiliana na kuwa kutokubaliana kuwe katika kiwango fulani, kiwango cha chini kabisa.

Kwa mfano, mzungumzaji huweza kusema kuwa Kiswahili ni somo lisiloeleweka kabisa, kisha msikilizaji wake amjibu kuwa analosema ni kweli ingawa sehemu ya lugha ni nyepesi. Katika mfano huu, msikilizaji haonyeshi kutokubaliana na kauli ya mzungumzaji kwa njia inayoleta mkwaruzano, bali kiwango chake cha kukubaliana na mzungumzaji hufanya mawasiliano yao kuweza kuendelea.

### **1.8.2.5 Kanuni ya Huruma**

Hii kaida huhakikisha kuwa kuna huruma ya moja kwa moja katika mazungumzo. Kaida hii hutarajia kuwa mafanikio yanayojitokeza baada ya huruma kuonyeshwa yanatambulika. Kaida hii ya huruma huonyesha kuwa kuna umoja kati ya wazungumzaji na wasikilizaji.

Mzungumzaji anapomwambia msikilizaji wake kuwa anasikitika sana kutokana na kifo cha mama yake yule msikilizaji, mzungumzaji yule anatoa ujumbe wa kumfariji yule aliyefiwa, kwa hivyo, ujumbe huu unaonyesha umoja uliopo baina ya mzungumzaji na msikilizaji wake.

## **1.9 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu umefanywa maktabani pamoja na mtandaoni. Maktaba ilitumika kwa sababu ya kutaka kupata maoni mbalimbali ya watafiti wa hapo mwanzoni pamoja na mawazo waliyoyatoa wataalamu wa lugha kuhusu dhana hii ya mikakati ya upole katika mazungumzo. Kwenye mtandao, maelezo kuhusu Nadharia ya Upole, pamoja na mawazo ya watafiti wengine kuhusu



mikakati ya upole yalipatikana. Kuna mbinu mbalimbali ambazo zimesaidia katika kupata data katika utafiti huu. Njia hizo ni pamoja na:

### **1.9.1 Uteuzi wa Sampuli**

Data ambayo imefanikisha utafiti huu imetolewa katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen. Kituo hiki cha Redio Citizen kina watangazaji ambao huteua maneno yao kabla ya kuyatamka huku wakihakikisha kuwa wamedumisha uhusiano mwema kutokana na maneno teule wanayotumia. Vipindi viwili vilivyoteuliwa kufanikisha utafiti huu ni Kipindi cha “Jambo Kenya” na kile cha “Chapa kazi”.

### **1.9.2 Ukusanyaji wa Data**

Kwanza, nilisikiliza vipindi viwili vilivyoteuliwa na ambavyo vinapeperushwa kwenye kituo cha Redio Citizen. Vipindi hivi ni “Jambo Kenya” pamoja na “Chapa Kazi”, vipindi maalum ambavyo vimefanikisha utafiti huu. Nilinasa yale ambayo yanapatikana katika kituo cha Redio Citizen, hasa yale ambayo yanathibitisha upole unavyotumika katika kituo hiki kwa kutumia simu ya tamba. Yaliyonaswa kwenye simu tamba yaliamishwa na kuhifadhiwa kwenye diski.

Vile vile, nilisoma yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Upole pamoja na Nadharia ya Uso, na jinsi ambavyo mikakati ya upole husaidia katika kuokoa nyuso za wasikilizaji pamoja na wazungumzaji. Nimefanya utafiti kuhusu athari ya matumizi ya lugha ya upole katika kuhakikisha kuwa mazungumzo yameweza kufikia malengo yake.

### **1.9.3 Uchanganuzi wa Data**

Baada ya kupata data, nilihakiki na kutathmini data hiyo kulingana na malengo ya utafiti huu pamoja na mihimili ya Nadharia ya Upole. Nilichanganua data hiyo ili kufafanua ikiwa matumizi ya maneno yenye upole yanasaidia katika kukuza mawasiliano na kuhakikisha kuwa mawasiliano yanaendelea kwa njia inayotosheleza, hasa katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio Citizen.

### **1.9.4 Uwasilishwaji wa Data**

Uhakiki na utathmini wa data hiyo umewezesha kufikia uamuzi wa kukubali kuwa mikakati ya upole husaidia sana katika kutodhuru nyuso za wanaohusika katika mazungumzo yoyote.

Data iliyohakikiwa imewasilishwa kupitia kwa njia ya maelezo. Uwasilishwaji huo unahusu jinsi ambavyo mikakati tofauti tofauti ya upole hutumika katika kituo cha Redio Citizen, hasa kwenye vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”. Maelezo yaliyo kwenye tasnifu yamepelekwa maktabani, ili yawe kama kifaa cha marejeleo kwa wote ambao wanatarajia kujua mengi kuhusu mikakati ya upole katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya Redio Citizen.

Mbinu hizi za ukusanyaji data zimenisaidia katika kuthibitisha mada ya utafiti huu, kanuni ya upole kwenye vipindi “Jambo Kenya” na “Chapa kazi” vya kituo cha utangazaji cha Redio Citizen.

### **1.10 Hitimisho**

Sura hii ya kwanza kimsingi, imesaidia katika kujenga sura zingine za tasnifu hii na hatimaye kuziba pengo ambalo kwangu mimi, halijawahi kuzibwa na yeyote katika utafiti, pengo likiwa kanuni ya upole kwenye matangazo ya Kiswahili katika kituo cha Redio Citizen, hasa kwa kuangazia vipindi viwili vilivyoteuliwa na ambavyo vinapeperushwa katika kituo cha Redio Citizen. Vipindi hivyo viwili vikiwa, “Jambo Kenya” pamoja na “Chapa Kazi”.

## **SURA YA PILI**

### **DHANA YA UPOLE**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii ni ya kijumla na imesaidia katika kujenga msingi wa sura zingine za tasnifu hii. Sura hii imezingatia mitazamo mikuu ya upole, mtazamo wa uso wa Brown na Levinson (1978, 1987) pamoja na mtazamo wa upole wa Leech (1983). Katika kufanikisha swala hili, utafiti huu umeangazia jinsi nadharia ya upole ilivyokuzwa na kuendelezwa kwa kujikita katika mazungumzo ya Kiswahili.

Sehemu ya 2.2 inashughulikia dhana ya upole huku ikijikita katika madai ya wanaisimu mbali mbali waliotoa ufafanuzi kuhusu dhana ya upole. Sehemu ya 2.3 inaangazia mkakati wa upole unaotumika katika kuokoa nyuso za wazungumzaji na wasikilizaji kwenye mazungumzo. Kauli ambazo huwa tishio kwa nyuso za wazungumzaji na wasikilizaji pamoja na mikakati ya kukabiliana na vitisho vya nyuso vinajadiliwa katika sura hii.

Uchunguzi kuhusu kanuni ya upole kwenye mawasiliano kati ya mzungumzaji na msikilizaji ndio msingi wa utafiti huu, hivyo ni muhimu kutoa ufafanuzi kuhusu dhana ya upole. Upole ni dhana ambayo imefanyiwa utafiti na wanaisimu wengi. Wanaisimu hao waliofanyia utafiti dhana ya upole wanakubaliana kuwa, upole unaotumika katika mazungumzo huwa na dhamira ya kuhakikisha kuwa mawasiliano yanatimiza malengo yake.

#### **2.2 Upole Kwenye Mawasiliano**

Nadharia zinazozungumzia dhana ya upole zilijadiliwa na Brown na Levinson (1978, 1987), Leech (1983), Fraser na Nolen (1981) pamoja na Watts (2003). Ni muhimu kutambua kuwa, Brown na Levinson waliweza kutoa ufafanuzi kuhusu dhana ya upole kutoka kwa dai la uso la Goffman (1967) ambalo lilijadiliwa hapo awali.

Dhana ya upole ilishughulikiwa na Goffman (1967) hapo awali. Kulingana na Goffman (1967), upole ni hali ya kumtambua mtu anayehusika katika mazungumzo huku kaida fulani za mazungumzo zikipekwa. Kuepuka kaida fulani katika mazungumzo husaidia katika kukidhi



mahusiano mema kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Upole vile vile hudhihirisha kuwa mzungumzaji anashughulikia matakwa ya msikilizaji wake huku akimpa heshima.

Goffman (1967) vile vile aliibuka na nadharia ya uso ambayo humwelekeza mzungumzaji kutumia maneno yenye upole katika matamshi yake ili kuokoa uso wa msikilizaji. Goffman (1967) anadai kuwa, mtu huweza kujipa uso kutegemea mtazamo ambao huweza kuchukuliwa kuwa umeegemea katika maswala fulani. Kulingana na Goffman (1967), kutunzwa kwa uso humfanya mtu kuwa na hisi nzuri kwani watu huwa na uhusiano na uso, ambao wao hutunza.

Brown na Levinson (1978) walitumia dai la uso la Goffman (1967) katika kutoa ufafanuzi kuhusu dhana ya upole. Brown na Levinson (1978) walitoa ufafanuzi wa upole kama namna ya kuokoa uso wa msikilizaji, uso huu ukiwa picha ya kibinafsi ya mtu yeyote ambaye huhusika katika mazungumzo.

Brown na Levinson (1978, 1987) vile vile wanadai kuwa, kuna mikakati tofauti tofauti ya upole ambayo husaidia katika kudumisha uhusiano mwema baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Brown na Levinson (1978, 1987) wanasema kuwa mikakati hii ya upole husaidia katika kuokoa nyuso za wahusika, kwa sababu nyuso za wahusika lazima zitunzwe na kuhifadhiwa katika hali zote.

Leech (1983) akiendeleza kazi ya Grice (1975), aliibuka na kaida sita za upole, kaida ambazo hudhamiria kuonyesha wanaoingilia katika mazungumzo jinsi ya kutumia maneno yenye upole katika mazungumzo yao, pamoja na umuhimu wa kutumia maneno hayo yenye upole katika mitagusano yao ya kila siku. Kaida hizo sita ni pamoja na huruma, ukarimu, makubaliano, mkakati, sifa kwa msikilizaji na kaida ya kujitweza.

Leech (1983) anadai kuwa mikakati ya upole huweza kutumika katika mazungumzo ili wazungumzaji na wasikilizaji watengane na mgongano wa aina yoyote. Leech (1983) anatolea mikakati ya upole ufafanuzi zaidi kwa kusema kuwa, mikakati ya upole huwa na jukumu pamoja na lengo la kuhakikisha kuwa kuna urari katika mawasiliano pamoja na mahusiano mema yanayodumishwa katika mazungumzo yale.

Kulingana na Leech, (1983), mtagusano wa mazungumzo unajumuisha utaratibu wa upole, nao utaratibu wa upole una kaida zake, kaida ambazo husaidia wanaoingilia mazungumzo kutimiza

malengo yao na kuweza kutagusana kwa njia inayofaa. Ni muhimu kutambua kuwa mzungumzaji huweza kutumia zaidi ya kaida moja katika mazungumzo, mojawapo ya kaida ikiwa katika usemi, na nyingine ikiwa katika umaanisho. Kaida za upole ambazo ziliibuliwa na Leech ni:

### **2.2.1 Kanuni ya Kusifu katika Kufanikisha Mawasiliano**

Kaida ya kusifu huagiza wale ambao hujihushisha katika mazungumzo kuhakikisha kuwa sifa zinawaendea wasikilizaji wao. Sifa zinazoelekezwa kwa msikilizaji huhakikisha kuwa msikilizaji anajiunga na mzungumzaji katika mazungumzo, na kutoa mchango wake katika mjadala unaoendelea. Vile vile mzungumzaji anaweza kutumia tasfida, au hata kutosema lolote ikiwa jambo la kusifu msikilizaji haliwezekani.

Kaida hii huhakikisha kuwa wasikilizaji wanahisi vizuri, hivyo basi kuleta ushirikiano katika mazungumzo. Kwa mfano, Mzungumzaji akiwa atamsifu mzungumzaji wake kila mara kwa kumwita mrembo, basi atamfanya msikilizaji yule kuhisi vizuri na hata kuendelea kushiriki katika mazungumzo.

1. Mzungumzaji: Habari ya leo mrembo?

Msikilizaji: Sina jambo lolote la muhimu mwenzangu, ila nakupitishia tu salamu...

Mzungumzaji: Nashukuru mwenzangu.

Mzungumzaji vile vile, huweza kumfanya msikilizaji wake kuhisi vyema hata anapomsifu yule ambaye tayari ashaaga dunia. Wale ambao watafurahishwa na kauli kama hizo ni familia ya mwenda zake kwani watachukulia kuwa mwenda zake anakumbukwa kwa mema aliyoyatenda, hasa kwa kusifiwa.

2. Mzungumzaji: Marehemu Michuki alileta mabadiliko katika sekta ya usafiri, idadi ya waliokuwa wakiaga dunia ilipungua...

Msikilizaji: Mungu aendelee kuilaza roho yake mahali pema peponi.

Kupitia kwa mfano huu, mzungumzaji anazungumzia swala la ongezeko la maafa kwenye barabara zilizoko nchini Kenya na kumsifu marehemu John Michuki kwa mabadiliko aliyoleta katika sekta ya usafiri. Watu wengi kama si wote, wana uwezo wa kukumbuka marehemu Michuki alivyohakikisha kuwa magari yaliwekewa vidhibiti mwendo vilivyohakikisha kuwa



magari yaliendeshwa kwa kasi inayofaa, pamoja na sare za madereva, zilizowafanya polisi kuwatambua wale dereva kwa urahisi.

Katika kuwasifu wasikilizaji na hata watangazaji, nyuso zao chanya huhifadhiwa kwani nyuso chanya hutaka kusifiwa, kuthaminiwa na hata kutambuliwa. Vile vile maneno ya kusifu mara nyingi huwa yamejaa upole, hivyo, maneno hayo yenye sifa huhakikisha kuwa wanaohusika katika mazungumzo wanafurahia mazungumzo hayo kutokana na hisia nzuri.

### **2.2.2 Kanuni ya Huruma katika Kuleta Maelewano Baina ya Wahusika**

Kanuni hii huhakikisha kuwa kuna huruma ya moja kwa moja katika mazungumzo au mjadala wowote. Kauli nyingi katika kaida ya huruma hujitokeza katika usemi wa kutoa rambi rambi, kauli ambazo hushughulikia mahitaji na matamania ya wasikilizaji. Kanuni hii vile vile hutarajia kuwa mafanikio yanayojitokeza baada ya huruma kuonyeshwa yanatambulika, mafanikio hayo yakitokea upande wa msikilizaji.

3. Mzungumzaji A: Tulimpoteza baba yetu siku mbili zilizopita.

Mzungumzaji B: Pole sana rafiki yangu, njia yetu sote. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi.

Mzungumzaji A baada ya kusikia anachosema mzungumzaji B kupitia kwa mfano huu, anamwonyesha mzungumzaji A huruma kwa kutoa rambi rambi zake. Kwa kutuma risala za rambi rambi, mzungumzaji B anaonyesha kuwa yuko pamoja na msikilizaji yule katika machungu yaliyompata.

Katika kutuma risala za rambi rambi au hata kutumia kaida ya huruma katika mazungumzo, msikilizaji hupata kuliwazwa. Aliyepatwa na msiba vile vile huhisi kuwa, watu wameungana naye katika matatizo yaliyompata, pamoja na kuwa watu wale wanaoonyesha huruma wanamsaidia katika kuomboleza. Kuonyesha huruma katika mazungumzo huleta ushirikiano kati ya msikilizaji na mzungumzaji.

### **2.2.3 Kanuni ya Kujitweza Katika Kuleta Maridhiano Kwenye Mazungumzo**

Kaida hii hutoa ufafanuzi wa msemaji kujidunisha na kuzidisha kauli ya kujitweza katika mazungumzo baina yake na msikilizaji wake. Msaada huweza kuombwa katika kaida ya

kujitweza, huku msikilizaji akipata sifa katika jambo linalozungumziwa. Kwa mfano, mtu atendapo tendo fulani kisha ajaribu kujitetea kwa kusema:

4. Mzungumzaji: Hongera kwa kazi nzuri uliyofanya.

Msikilizaji: Asante tunajaribu tu, tunatarajia kufikia kiwango cha juu hapo mbeleni.

Huyu msikilizaji anajaribu kuonyesha kuwa yuko katika kiwango kimoja na yule mzungumzaji hata ingawa yule mzungumzaji anampongeza kwa jambo ambalo amelitenda. Mzungumzaji anahakikisha kuwa sifa zote zimeelekezwa kwa msikilizaji wake. Msikilizaji yule anaonekana akijaribu kujitetea kwa kudai kuwa bado hawajafikia kiwango kinachotarajiwa hata ingawa wamejaribu.

Kaida ya kujitweza kwa hivyo, huwa na lengo la kuhakikisha kuwa yeyote anayeingilia mazungumzo hakwaziki, bali anafurahia na kuridhishwa na mazungumzo yanayoendelea kati yao. Katika kufanya hivi, uhusiano baina ya mzungumzaji na msikilizaji wake hudumishwa, huku mitagusano kati yao ikionekana kuwa jambo rahisi linaloweza kutimizwa na hao wote ambao wanajihusisha na dayalojia inayoendelea.

#### **2.2.4 Kanuni ya Ukarimu Katika Kufanikisha Maelewano Katika Mawasiliano**

Kaida ya ukarimu hudhamiria kuonyesha kuwa anayezungumziwa ana uwezo wa kulitenda jambo fulani. Kaida hii huagiza wazungumzaji kutosema au hata kutotumia maneno ambayo huweza kukasirisha wasikilizaji wao. Kwa hivyo, msemaji hutarajia kupunguza uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga manufaa kwake binafsi. Kwa mfano, Msemaji anaposema:

5. Msemaji: Utaninunulia kikombe cha chai leo.

Msikilizaji: Aah! Ungekuja hata jana ningekununulia.

Kauli hii inalenga kumnufaisha yule anayezungumziwa. Hii ni kwa sababu yeye ndiye atafanyiwa kitendo kinachozungumziwa katika dayalojia hii, kitendo chenye kikiwa, kununuliwa kikombe cha chai. Kwa hivyo, kaida hii inaonyesha kuwa wasikilizaji wanafaa kushugulikiwa kwanza katika mazungumzo.

6. A: Wanawake watanivunja mbavu siku moja, eti mtu amelazwa hospitalini baada ya kukatwa sehemu zake za siri na mkewe...

B: Lakini kuna wakarimu humu duniani, gavana wake amechukua mzigo huo wa kumtibu katika hospitali ya Kapsabet.

Kupitia kwa mfano huu, mzungumzaji A anamwambia B kuwa bwana mmoja amelazwa katika hospitali huko Kapsabet baada ya kukatwa sehemu yake ya siri na mkewe, baada ya kudinda kuacha pombe. Baada ya matamshi ya A, B anamkumbusha kuwa Gavana wa kaunti yake yule mhasiriwa amejitolea kwa ukarimu na kushughulikia malipo ya hospitali ya yule mhasiriwa na kuwaomba watu kutofanya kitendo kama kile ambacho huweza kudhuru uso hasi wa mtu yeyote katika jamii.

Mtu yeyote anapotenda kitendo cha ukarimu, yeye huonyesha heshima kwa yule ambaye amemtendea mazuri, huku akihifadhi uso wake pamoja na ule uso wa anayetendewa kitendo cha ukarimu. Huwa jambo nzuri kutendea watu mema. Matendo mazuri huhusishwa na mikakati ya upole, mikakati ambayo huelekeza watu katika kuheshimiana hasa wanapohusika katika mawasiliano.

### **2.2.5 Kanuni ya Kukubaliana Katika Kufanikisha Upole kwenye Mawasiliano**

Kaida ya makubaliano hutahadharisha wanaoshiriki katika mazungumzo kuwa, kuna umuhimu wa kukubaliana watu wanapowasiliana. Kaida hii vile vile, inadai kuwa kunapotokea kutokubaliana katika mazungumzo, kutokubaliana huko kuwe wa kiwango cha chini kabisa.

7. A: Naomba uniambie chochote unachofahamu kuhusu ufisadi.

B: Hamna shida nitakuambia lakini ngojea kidogo.

A: Hamna tatizo, nitasubiri.

A anamwomba B kumwambia kisa chochote ambacho kinaweza kuhusishwa na ufisadi pamoja na athari ya ufisadi katika jamii. B anamwomba A kumpa muda wa kumaliza alichokuwa akifanya ndipo aweze kutoa mfano wa kisa kinachohusishwa na mada ile ya ufisadi na athari zake. B anakubaliana na ombi la A kwa kusema kuwa, yuko tayari kungojea. Jibu la mzungumzaji A kuwa yuko tayari kusubiri linaonyesha kuwa amekubaliana na ombi lake mzungumzaji A kuwa aweze kungojea kidogo, na kuwa hamna tatizo lolote.

Kaida hii ya kukubaliana hutumia upole katika maneno ambayo huteuliwa kutumika katika mazungumzo. Maneno yenye upole hunuia kuhakikisha kuwa nyuso chanya za wanaohusika



katika mazungumzo fulanizinaokolewa na kuhifadhiwa, kwani nyuso chanya hutaka kuhusishwa katika mambo ya kijamii.

Kaida hii ya makubaliano vile vile inaweza kufananishwa na mkakati chanya wa upole wa Brown na Levinson (1978), mkakati ambao hunuia kutafuta makubaliano na kuepuka kutokubaliana. Kuepuka kutokubaliana husaidia katika kuokoa nyuso chanya za wanaohusika katika mazungumzo yoyote yale, kwani wao huhakikishiwa kuwa maoni yao yanathaminiwa.

### **2.2.6 Kanuni ya Mkakati Katika Kuhakikisha Maelewano Baina ya Wazungumzaji**

Kaida ya mkakati hutoa maelezo kwa msemaji kuzidisha uwasilishaji wa kauli ambazo huelekeza manufaa kwa msikilizaji, huku gharama ikimwendea yule mzungumzaji. Maongezi katika kaida ya mkakati humfanya msikilizaji kufanya jambo fulani ambalo hakunua kulitenda.

8. A: Naomba unisaidie kusoma ujumbe huu, lugha hii ya vijana wetu inanitiza mno.

B: Nitakusaidia lakini kumbuka kuwa, hata mimi sielewi baadhi ya mambo katika lugha hii ya sheng'.

Mzungumzaji A anamwomba msikilizaji wake ambaye ni B kumsaidia kusoma ujumbe ambao umeandikwa kwa kutumia lugha ya sheng'. B anaitika kumsaidia lakini anamhakikishia kuwa hata yeye si gwiji wa lugha hiyo ya vijana. Kwa kufanya hivi, B anakubaliana na ombi lake A na kuhakikisha kuwa manufaa yamemwendea mzungumzaji A.

Kaida hizi sita za upole ndizo ziliibuliwa na Leech (1983). Kaida hizi sita za upole ni muhimu katika mazungumzo. Mazungumzo huwa maongezi yanayoendelea kati ya watu wawili au zaidi, maongezi hayo yakiwa na lengo fulani. Mara nyingi, watu huingilia mazungumzo wakiwa na nia ya kupitisha ujumbe. Ujumbe unaweza kupitishwa kwa njia inayotosholeza ikiwa watu wataelewana katika mazungumzo. Maelewano huweza kufanikishwa na kuwepo kwa matumizi ya upole kwenye mawasiliano.

Baada ya Leech (1983) kutoa ufafanuzi kuhusu dhana ya upole na kuibuka na kaida sita za upole, Fraser (1990) alitoa mapendekezo yake kuhusu dhana ya upole kwa kuibuka na mikakati minne. Akizungumzia dhana ya upole, Fraser (1990) aliibuka na mkakati wa kuwa kwenye mazungumzo, mitazamo ya kanuni za kijamii, mikakati ya makubaliano kwenye mazungumzo pamoja na mikakati ya upole kwa mtazamo wa kuokoa uso. Mkakati huu wa upole kwa mtazamo

wa kuokoa uso ndio imejadiliwa kwa kina katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu lengo la utafiti huu ni kubainisha upole unavyosaidia katika kukidhi mawasiliano.

### 2.3 Nadharia ya Uso

Dhana ya uso imejadiliwa na wanaisimu wengi ambao wanakubaliana kwa kiwango fulani kuwa, kila binadamu huwa na uso. Uso wa binadamu huweza kuhifadhiwa au hata kupotezwa. Uso wa binadamu vile vile huweza kupokelewa tena baada ya kupotezwa.

Kwa mujibu wa Goffman (1967:5), uso huwa picha ya kibinafsi na ya kipekee ambayo kila binadamu hujaribu kulinda. Uso huweza kuwa thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao wengine huchukulia kuwa umeegemea katika mtagusano fulani.

Brown na Levinson (1978), wanatoa maelezo ya wazungumzaji na wasikilizaji kuwa na ama uso chanya au uso hasi. Uso chanya ni uso ambao binadamu hutaka kusifiwa, kuthaminiwa na kuhusishwa katika mambo ya kijamii. Uso chanya vile vile hutaka kutambuliwa na kwamba kutotambuliwa kwa uso huu huweza kuudhuru uso wenyewe.

Kulingana na tamko la mzungumzaji katika mfano wa tisa, mzungumzaji anamwambia msikilizaji wake kuwa bila usaidizi wake hawangetimiza lengo lao. Mzungumzaji anapoyasema hayo, anaokoa uso chanya wa msikilizaji huyo. Hii ni kwa sababu, kwa kusema hivi, mzungumzaji atakuwa amemtambua msikilizaji yule, na kuwa, uso chanya hutaka kutambuliwa na kuhusishwa katika mambo. Mzungumzaji vile vile anamwonyesha msikilizaji huyo kuwa mchango wake ulikuwa wa manufaa, na kuwa mchango huo umewafanya kutimiza matakwa yao kama walivyopanga hapo awali.

9. Mzungumzaji: Nashukuru sana kwa yote uliyotenda, nakiri kuwa bila usaidizi wako, hatungetimiza lengo letu.

Msikilizaji: Shukrani zimwendee Maulana.

Uso hasi huwa uso usiotaka kusumbuliwa au hata kuingiliwa kwa vyovyote vile. Uso hasi huwa uso unaohitaji uhuru wake. Kwa mfano, mzungumzaji anapomlazimisha msikilizaji wake kufanya jambo ambalo hakunua kulitenda, basi atakuwa anamwingilia msikilizaji yule, hivyo, kutisha uso hasi wake. Katika kumlazimisha msikilizaji kutenda kitendo fulani, mzungumzaji atamfanya msikilizaji kutokuwa na uhuru wa kuchagua ikiwa atafanya tendo lile au la.



Kupitia kwa mfano wa kumi, mzungumzaji anamlazimisha msikilizaji wake kumnunulia kikombe cha chai. Msikilizaji anaonekana kama yule ambaye hana budi ila kumnunulia msikilizaji wake kikombe cha chai. Kitendo hiki kwa hivyo kinatisha uso hasi wa msikilizaji.

10. Mzungumzaji: Aah! Lazima uninunulie kikombe cha chai leo.

Msikilizaji: Hamna neno, nitakununulia tu.

Kutokana na aina hizi mbili za uso, Brown na Levinson (1978), walitoa mapendekezo kuwa wazungumzaji wanafaa kutia maanani swala la uso katika mazungumzo yao kwa sababu uso huweza kupotezwa au hata kuhifadhiwa. Kupotezwa au kuhifadhiwa kwa uso kwenye mazungumzo hutegemea matumizi ya maneno kwenye mawasiliano.

Matumizi ya maneno yenye upole katika mawasiliano huhakikisha kwamba nyuso za wahasika zimehifadhiwa katika mazungumzo. Hii ni kwa sababu, maneno yenye upole hayamtii aibu msikilizaji au hata mzungumzaji yeyote katika mazungumzo.

Fraser (1990: 229), anaonyesha makubaliano na kauli ya Brown na Levinson (1978, 1987) kuwa, huwa muhimu sana kwa mtu kuhifadhi sio tu uso wake, bali hata nyuso za wengine wote wanaohusika katika mazungumzo. Katika mtazamo huu wa kuokoa uso, wazungumzaji hujaribu kuepuka matendo yanayotisha uso kwa kutumia maneno yenye upole katika mazungumzo yao.

Kauli zenye kutisha uso katika mazungumzo ni zile kauli ambazo hudhuru uso wa aidha msikilizaji au mzungumzaji, au hata nyuso za wote ambao huhusika katika mazungumzo. Kauli hizo ambazo hutisha uso huwa na athari kubwa kwa wale wanaoingilia mazungumzo yoyote kwani huweza kuleta vikwazo katika mawasiliano, huweza kufanya ujumbe muhimu kutofikia hadhira lengwa, na vile vile huweza kufanya wanaohusika katika mazungumzo kutoaminiana, hivyo kutowasilisha taarifa inayohitajika kwa njia inayofaa.

Kauli ambazo hutisha uso vile vile huweza kufanya mazungumzo kutofikia malengo yake kwa sababu mazungumzo hukatika kabla ya kumalizika. Kauli hizo ambazo hutisha uso huwafanya wanaowasiliana kuaibika, au hata kuwalazimisha kufanya mambo ambayo hawakunua kufanya, kama vile kuomba msamaha, hivyo kutisha nyuso zao.

Nyuso za wanaohusika katika mazungumzo zinapotishwa, huweza kuleta athari kubwa katika mawasiliano. Hii ni kwa sababu aliyetishiwa uso huweza kuaibika au hata kuudhika, na kuamua



kutoendelea kushiriki katika mazungumzo. Sehemu zinazofuata zinajadili baadhi ya kauli ambazo zinaweza kutumiwa na wanaohusika katika mazungumzo katika kutisha uso.

Brown na Levinson (1978), wanadai kuwa, kuna vitendo ambavyo huweza kudhuru uso wa msikilizaji au hata mzungumzaji. Kuna kauli zinazotisha nyuso chanya za wasikilizaji, kauli zinazotisha nyuso chanya za wasemaji, kauli zinazotisha nyuso hasi za wasikilizaji na kauli zinazotisha nyuso hasi za wasemaji. Kauli hizi ndizo zinafanya wazungumzaji kutumia maneno yenye upole katika mawasiliano. Kwa kutumia maneno yenye upole, wote wanaohusika katika mazungumzo huwa na nia ya kuhakikisha kuwa mawasiliano yanafikia malengo yake.

Maneno yenye upole yanapotumika katika mawasiliano, hufanya watu kuingiliana kwa urahisi na wale ambao hupenda kutumia maneno yenye upole mara kwa mara. Hii ni kwa sababu watu wote hujaribu kuokoa na kuhifadhi nyuso zao kwa kuepukana na aibu pamoja na matusi ya aina yoyote. Matumizi ya upole huweza kufanya watu kutaka kuwasiliana kila mara, hivyo kufanya hata shughuli kama vile za kibiashara kutekelezwa kwa njia inayotosheleza.

Anayetumia maneno yenye upole hunasa makini ya watu wengi, huku akiepukana na uwezekano wa kuwa na maadui wengi. Hivyo, matumizi ya maneno yenye upole huwa muhimu sana katika maisha ya kila binadamu kwa sababu binadamu lazima awasiliane na mwenzake kila mara. Mawasiliano hufanya binadamu kuweza kutagusana kwa kupashana habari.

Lazima kila mtu anayeingilia mazungumzo yoyote aweze kuwa na stadi za mazungumzo hasa katika kuingiliana na watu wenye tajriba tofauti tofauti, pamoja na umri tofauti. Hata hivyo kauli ambazo hutisha uso huweza kutambulika na kushughulikiwa ipasavyo, ikiangaziwa kwamba, kauli hizo zinazotisha uso hufanya mawasiliano kufikia kikomo kabla ya ujumbe muhimu kupitishwa.

### **2.3.1 Kauli Zinazotisha Nyuso Chanya za Wasikilizaji**

Matendo au hata kauli ambazo huelekezwa kwa msikilizaji, na ambazo humtia aibu huweza kuwa na athari kwa uso chanya wa msikilizaji yeyote. Kauli ambazo humtia aibu aidha msikilizaji au mzungumzaji huwa kauli zenye kudunisha, zenye matusi au hata kauli ambazo hutoa tishio kwa uso wa msikilizaji au mzungumzaji.

Kuaibishwa kwa mtu humfanya kuhisi kuwa hana thamana yoyote katika jamii. Aibu humfanya mtu kuwa na hisi kuwa hafai kujiunga na wengine katika kushughulikia maswala tofauti tofauti ya kijamii, na kuwa akijiunga nao, pengine watamwaibisha. Vile vile, aibu hufanya aliyeaibishwa kuwa na ugumu wa kuweza kutambua tofauti kati ya ubaya wa kuwa binafsi katika mambo yanayotekelezwa na watu wa jamii fulani, na ubaya wa kuwa na tabia mbaya katika harakati ya kuhusiana na watu katika jamii.

Aibu huweza kufanya watu kutafuta jinsi ya kuhifadhi nyuso zao au hata kulipiza kisasi kwa waliowaibisha, kwa kutafuta makosa ambayo wameyafanya, kuyasema makosa hayo hadharani, huku wakiwa na nia ya kuhifadhi nyuso zao ambazo zilitishwa hapo awali, na kuzitisha nyuso za wale ambao waliwatia aibu.

11. Mzungumzaji: Ni wazi kuwa walinda usalama huchukua hongo, mimi siwapendi askari.

Msikilizaji: Usiongee hivyo kuwahusu askari kwa sababu si askari wote huchukua hongo.

Kupitia kwa mfano huu, mzungumzaji analalamikia swala la askari kuchukua hongo. Mzungumzaji anajumuisha askari wote katika kauli yake hivyo kuwatishia uso. Msikilizaji wake hata hivyo, anaingilia kati na kuwatetea askari kwa kusema kuwa, si wote huchukua hongo. Mzungumzaji huyu anatisha nyuso chanya za askari ambao pengine, wanamsikiliza akiongea.

Katika kauli mzungumzaji huyu, maneno yake yanaweza kuwatia aibu askari, ambao ni walinda usalama nchini Kenya, hivyo, kuwa tishio kwa nyuso zao chanya. Kauli yake mzungumzaji vile vile ni tishio kwa nyuso chanya za askari kwa sababu ni kauli ambayo inawaingilia kwa kudai kuwa wote huonekana kama wale ambao huchukua hongo wakiwa katika harakati ya kutekeleza majukumu yao.

Matamshi yake msikilizaji kwa hivyo, yanadhihirisha upole na heshima kwa askari wote, wanaochukua hongo pamoja na wasiochukua hongo kijumla. Maneno yake msikilizaji yaliyojaa upole yanasaidia katika kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji, swala linalodhihirika kupitia kwa mfano ufuatao.

12. Msikilizaji: Usiongee hivyo kuwahusu askari kwa sababu si askari wote huchukua...



### 2.3.2 Kauli Zinazotisha Nyuso Chanya za Wasemaji

Kuna kauli ambazo huweza kudhuru uso chanya wa msemaji lakini baada ya kutamkwa kwa maneno yale, hubidi kuwa mzungumzaji aliyetamka maneno yale yenye kudunisha kuomba msamaha kwa yule msikilizaji wake au hata mtu mwingine kuomba msamaha kwa niaba yake. Katika kuomba msamaha, msemaji hujidunisha mbele ya msikilizaji, ili kuweza kuruhusu mawasiliano kufikia malengo yake.

Kuomba msamaha huwa muhimu, japo huweza kumdunisha anayeomba msamaha kwa njia fulani. Kutubu makosa ambayo mtu ametenda hadharani huweza kuchukuliwa kama kitendo cha kuudhuru uso wa yule aliyetenda kosa. Kuombwa kwa msamaha huweza kuharibu uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji na msikilizaji au hata kumfanya mtu kupoteza kazi yake, katika hali tofauti tofauti, hasa kwa kumwangaia yule aliyekwazwa pamoja na tajriba yake katika jamii. Mfano ufuatao unatoa ithibati wa mhusika anayelazimika kuomba msamaha.

13. Mzungumzaji A: Shairi lako linaudhi, tukaririe shairi lingine.

Msikilizaji: Sina shairi lingine, wacha niende zangu.

Mzungumzaji B: Pole sana, unafanyiwa tu mzaha. Endelea kulikariri shairi hilo.

Mfano huu unaonyesha jinsi ambavyo msikilizaji anakwazika baada ya kuambiwa na mzungumzaji A kuwa shairi lake halipendezi, jambo ambalo linamkasirisha msikilizaji. Msikilizaji baada ya kukwazika, anaamua kuwa anaenda zake. Baada ya kutambua kuwa matamshi yake mzungumzaji A yamemkasirisha msikilizaji yule, mzungumzaji B anaaamua kujidunisha mbele ya msikilizaji yule kwa kumwomba msamaha kwa yale yaliyosemwa namzungumzaji A kisha anamwomba aweza kuendelea na shughuli ya kulikariri shairi lile.

Matamshi yake mzungumzaji A katika mfano huu ni yale ambayo yanatisha uso chanya wa mzungumzaji B ambaye ni mzungumzaji mwenzake. Hii ni kwa sababu kauli yake mzungumzaji A yanamtia ulazimu mzungumzaji B kujidunisha mbele ya msikilizaji yule na kumwomba msamaha.

Kauli ambazo huwa tishio kwa nyuso chanya za aidha wazungumzaji au wasikilizaji huweza kufanya mawasiliano kufikia kikomo bila kutimiza malengo yake, ilhali wanaowasiliana huwa na lengo moja, la kuweza kupitisha ujumbe maalum kwa njia inayotosheleza.



### 2.3.3 Kauli Zinazotisha Nyuso Hasi za Wasikilizaji

Kauli ambazo hutisha nyuso hasi za wasikilizaji hudhihirika wakati ambapo wazungumzaji huamua kufanya mambo ambayo huchukuliwa kama yale ambayo yanaingilia nyuso hasi za wasikilizaji wao. Uso hasi wa msikilizaji huweza kuingiliwa kwa kushauriwa, kuagizwa kufanya jambo fulani, kuonywa au hata kutolewa amri ya kufanya jambo fulani ambalo hayuko tayari kulifanya.

Ni muhimu kutambua kuwa katika ulimwengu huu, kuna watu ambao hawapendi kutolewa ushauri wa kufanya mambo fulani. Kuna watu ambao hutaka kujiamulia kufanya mambo, pasi na kuagizwa kufanya mambo yale. Kuna watu wasiopenda kuonywa au hata kutolewa amri ya kufanya jambo.

Mambo haya huwa tishio kwa uso hasi wa anayezungumziwa, kwani uso huu hutaka kuachwa huru katika kutekeleza jambo lolote, vile vile, uso huu huwa hautaki kuingiliwa kwa vyovyote vile. Maswala haya ya kushauri, kutoa amri au hata kuagiza ni maswala ambayo yanamwingilia msikilizaji, hivyo kutisha uso hasi wake kama unavyohibitika katika mfano ufuatao.

14. Mzungumzaji: Airo wewe ni gwiji wa lugha.

Msikilizaji: Hilo ni jambo linalofahamika kwa wote.

Mzungumzaji: Haya, tamka neno tashihisi mara kadhaa.

Msikilizaji: Tasihisi tasihisi tasihisi...

Mzungumzaji: Hamna tatizo, naelewa unakotoka hakukuruhusu kulitamka neno hili vizuri.

Mzungumzaji kupitia kwa mfano wa kumi na nne analazimisha msikilizaji wake kutamka neno “tashihisi” mara kadhaa. Jambo hili linatisha uso hasi wa msikilizaji huyo kwani pengine ana uwezo wa kulitamka neno hili lakini kwa njia isiyofaa, jambo ambalo pengine linatokana na athari ya lugha ya kwanza ya msikilizaji huyo, lugha ambayo haina sauti /sh/ kwenye fonimu zake. Jambo hili linadhihirika kutokana na jinsi anavyotamka neno hilo.

Uso hasi wa msikilizaji huyo unatishwa kwa sababu umeingiliwa na mzungumzaji, licha ya kuwa uso huu huhitaji kuachwa huru na kutoingiliwa kwa vyovyote vile. Hata hivyo, msikilizaji

anaposhindwa kutamka neno lile, mzungumzaji anamwambia kuwa anaelewa kile kinachomfanya kutokuwa na uwezo wa kutamka neno lile, na kuwa hamna tatizo lolote.

Maneno haya teule ya mzungumzaji yanadhihirisha upole unaokusudia kutoa suluhu kwa kitendo hicho ambacho kinatisha uso hasi wa msikilizaji wake. Hawa wazungumzaji wanaonyesha kuwa, kufahamu mila, desturi pamoja na fonimu zinazopatikana katika kila lugha, hufanya watu kuelewana. Maelewano husaidia wanaohusika katika mazungumzo kutoingiliana hivyo kudumisha amani miongoni mwao.

#### **2.3.4 Kauli Zinazotisha Nyuso Hasi Za Wasemaji**

Jinsi ambavyo uso wa msikilizaji huweza kutishwa ndivyo ambavyo uso wa msemaji huweza kutishwa. Msemaji anapolazimika kukubaliana na pendekezo fulani ambalo linatoka kwa msikilizaji, uso wake hasi huwa unatishwa. Uso hasi wa msemaji hutishwa ikiwa atalazimika kutafuta maafikiano na msikilizaji wake kuhusu kauli fulani. Hii ni kwa sababu, pengine kwa mtazamo wake, kauli ile haina mantiki yoyote hivyo si muhimu, lakini inambidi kukubaliana na msikilizaji ili kuweza kuokoa uso hasi wake.

Mzungumzaji huweza kujaribu kadri awezavyo na kuhakikisha kuwa msikilizaji wake hapati fursa ya kumwingilia kwa vyovyote vile. Uso hasi wa msemaji vile vile huweza kutishwa ikiwa atalazimika kutotia maanani jambo baya ambalo msikilizaji amemtendea au hata anapolazimishwa kumwahidi msikilizaji wake kitu fulani bila kupenda kwake. Mfano wa kumi na tano unaonyesha jinsi uso hasi huweza kutishwa.

15. A: Lazima umtembelee mjukuu wako kesho, ili umliwaze kutokana na majanga yaliyompata

B: Nitamtembelea tu hata ingawa hatuelewani.

Kutokana na mfano huu, kauli yake mzungumzaji B inaonyesha kuwa hana budi ila kufanya alivyoagizwa na mzungumzaji A, ingawa shingo upande. Jambo hili la kutokuwa na chaguo ila kufanya alivyoagizwa linadhihirika kutokana na kauli aliyotoa mzungumzaji B. Mzungumzaji B anapotoa ahadi hii bila kupenda kwake ni tishio kwa uso hasi wake.

Msemaji anapolazimishwa kumwahidi msikilizaji wake kitu chochote bila kupenda kwake, uso wake hasi unaotaka kuachwa huru wakati wote hutishwa. Hii ni kwa sababu, pengine yule

msemaji hana budi ila kutoa ahadi kwa msikilizaji wake na pengine hana uwezo wa kutimiza ahadi yake. Mambo haya yote hufanya uso hasi wa msemaji kutishwa.

16. Mzungumzaji B: Usijali mama, A atakuchezea wimbo huo baada ya muda mfupi.

Msikilizaji: Nashukuru sana, ubarikiwe.

Kauli inayotisha uso hasi wa msemaji inaweza kutolewa ithibati kutoka kwa mfano huu, mzungumzaji A anapolazimika kumchezea yule msikilizaji wimbo alioomba, wimbo ambao kulingana na mzungumzaji A si mtamu na vile vile umepitwa na wakati.

Kitendo hiki cha kufanya kinyume na matakwa ya mzungumzaji A kuhusu kucheza kwa wimbo huo unafanya uso wake hasi kutishwa. Mzungumzaji A anaucheza wimbo huo kwa sababu mzungumzaji B amemwahidi msikilizaji huyo kuwa wimbo huo utachezwa, hata ingawa mzungumzaji A haupendi huo wimbo.

Swala hili kwa kiwango fulani, linadhihirisha upole wa yule mtangazaji hasa anapofanya jinsi msikilizaji huyo wa kituo cha Redio Citizen anavyotaka, hata ingawa hapendezwi na jambo hilo. Swala hili linamfanya yule msikilizaji kupiga simu tena na kumshukuru mzungumzaji A kwa kumchezea wimbo ule, hivyo mawasiliano yanafikia malengo yake kupitia kwa tendo hilo la Jerida, huku uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji yule na msikilizaji wake ukihifadhiwa.

#### **2.4 Matumizi ya Upole Katika Kukabiliana na Vitisho vya Uso**

Licha ya kuwa kuna kauli ambazo huweza kutisha nyuso hasi na nyuso chanya za wanaohusika katika mazungumzo, wote wanaohusika katika mazungumzo huwa na uwezo wa kukabiliana na kauli kama hizi. Brown na Levinson (1978) walitoa kauli kuhusu jinsi ambavyo watu huweza kupigana na matendo pamoja na kauli ambazo huwa tishio kwa nyuso za wale ambao wanahusika katika mawasiliano.

Katika kutoa mchango wao kuhusu Nadharia ya Upole, Brown na Levinson (1978) wanatoa ufafanuzi wa jinsi ambavyo watu wanaoingilia mazungumzo huweza kukabiliana na mambo ambayo huweza kufanya mawasiliano kutokamilika na vile vile, kutofikia malengo yake. Mawasiliano yanapokosa kufikia malengo yake, mazungumzo yale huchukuliwa kama yale ambayo hayakuwa muhimu, pamoja na kuwa, wazungumzaji hawana ufahamu wa jinsi ya kutumia lugha katika kukidhi mahitaji ya mawasiliano.



Kauli ambazo hufanya mazungumzo kukosa kufikia malengo yake ni zile kauli ambazo hutisha nyuso hasi na nyuso chanya za wale ambao huhusika katika mazungumzo. Kauli hizi zinazotisha uso huwafanya wanaoingilia mazungumzo kutokuwa na imani katika mazungumzo yale, kisha kuamua kutojumuika tena katika mazungumzo yale.

Ufafanuzi huu wa Brown na Levinson (1978) umesaidia sana katika kubainisha mikakati ya upole inayotumika katika mazungumzo yanayoendelea kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Maneno yenye upole hudhihirisha heshima kwa wote ambao huhusika katika mazungumzo, hivyo kufanya mawasiliano kuendelea kwa njia inayofaa, huku ujumbe muhimu ukipitishwa kwa njia inayokubalika.

Matumizi ya maneno yenye upole vile vile huwa na lengo la kuhakikisha kuwa uhusiano kubalifu unadumishwa kati ya mzungumzaji na msikilizaji wake. Kila mtu anayehusika katika mazungumzo hujaribu kuhakikisha kuwa anamfanya anayehusika katika mazungumzo naye kumwamini katika hali zote. Imani inayoelekezwa kwa wote wanaohusika katika mazungumzo hufanya mawasiliano kuhitimu.

Kuna mikakati kadhaa ya upole ambayo huweza kutumika na aidha mzungumzaji au msikilizaji katika kukabiliana na matendo ambayo huweza kuchukuliwa kama yale ambayo huwa tishio kwa uso wa aidha msikilizaji au mzungumzaji. Mikakati ya upole ambayo huweza kutumika katika kukabiliana na kauli zinazotisha uso katika mazungumzo ni:

#### **2.4.1 Kutowasilisha Taarifa**

Mkakati wa kwanza unaoweza kutumika katika kukabiliana na matamshi ambayo huwa tishio kwa nyuso za wanaohusika katika mazungumzo ni kutowasilisha taarifa. Wakati mwingine mzungumzaji huweza kufahamu kuwa ujumbe anaotaka kupitisha ni ule ambao unaweza kuzua rabsha, hivyo mzungumzaji yule huweza kufikia maamuzi ya kutowasilisha taarifa ile. Mzungumzaji huweza kunyamazia anachokifahamu ili asiweze kumkasirisha msikilizaji wake au hata kuudhuru uso wake.

Brown na Levinson (1978) ndio walipendekeza mkakati huu wa kukabiliana na matendo ambayo hutisha nyuso za wasikilizaji na wazungumzaji kwa kutowasilisha taarifa, taarifa ambayo inafikiriwa kuwa kama tishio kwa uso wa aidha msikilizaji au mzungumzaji. Mkakati huu

huhakikisha kuwa mawasiliano yameendelea vizuri, na kuwa ujumbe ulio muhimu umepitishwa kutoka kwa mzungumzaji hadi kwa msikilizaji.

Kwa mfano, kupitia kwa mazungumzo, msikilizaji anayejulikana kama Tom anaweza kutuma ujumbe wa kumsalimia mzungumzaji A. Mzungumzaji B anaposikia ujumbe huo kutoka kwa mzungumzaji A, anaweza kudai kuwa kuna mambo ambayo msikilizaji huyo aliyetuma ujumbe hufanya. Lakini mzungumzaji B anaweza kukataa kuyataja hayo mambo anayoyafanya msikilizaji hata anapouulizwa na mzungumzaji A.

17. Mzungumzaji A: Nakuambia leo nina furaha, rafiki yangu Tom alinitumia ujumbe wa heri na fanaka asubuhi na mapema. Nakuambia nilianza siku vizuri.

Mzungumzaji B: Kuna mambo anayoyafanya huyu Tom lakini wacha tu nisiyaseme maanake yanaweza kuzua rabsha...

Mzungumzaji A: Kwani Tom amefanya nini?

Mzungumzaji B: Usijali, Tom ni mtu mzuri sana lakini unafahamu kuwa kilicho kizuri hakiwezi kukosa doa.

Mzungumzaji B hakamilishi kauli yake bali anaamua kunyamazia kile anachokifahamu kuhusu yule aliyemtumia mzungumzaji A ujumbe. Aliyetuma ujumbe anajulikana kama Tom. Mzungumzaji B Anaamua kutomwambia Mzungumzaji A anachokifahamu kumhusu Tom, hivyo kumwachia jukumu la kufasiri anayoyafanya yule Tom. Kile anachofanya mzungumzaji B ni kumwambia mzungumzaji A kuwa kitu kinaweza kuwa kizuri lakini hakiwezi kukosa doa. Mzungumzaji A anaachiwa jukumu la kufasiri doa alilonalo yule Tom.

Kupitia kwa mfano wa kumi na nane, unadhihirika kuwa kuna msikilizaji anayenung'unika kuwa bwana yake hamshughulikii kabisa. Yule msikilizaji hashughulikiwi kwa sababu kila mara, bwana huenda nyumbani akiwa amechelewa. Yule bwana ana kila sababu ya kuenda nyumbani akiwa amechelewa, jambo analolifahamu mzungumzaji kwa sababu ameweza kuwasiliana na yule bibi asiyeshughulikiwa na bwana yake, na yule bibi amemwelezea kila kitu anachofanya bwana yake.

18. Mzungumzaji: Niambie mtu wangu

Msikilizaji: Mimi nina huzuni kubwa kwa sababu sishughulikiwi na bwana kwa sababu yeye hudai kuwa ana shughuli nyingi mjini hivyo huja akiwa

amechelewa kila mara...

Mzungumzaji: Kwa nini yeye huchelewa na hakushughulikii kivipi?

Msikilizaji: Ilianza mwaka uliopita wakati...

Mzungumzaji B anapotaka kujua asivyoshughulikiwa yule msikilizaji, pamoja na kutaka kumfahamu yule msikilizaji asiyeshughulikiwa na bwana yake, mzungumzaji A anamwambia kuwa mambo hayo si muhimu. Mzungumzaji A anamwambia kuwa kilicho muhimu ni kuwa yule msikilizaji hashughulikiwi na mumewe.

Licha ya kuwa Mzungumzaji A anafahamu asivyoshughulikiwa yule msikilizaji, anaamua kutosema anayoyafahamu. Mzungumzaji A anafanya haya yote ili kuhifadhi uso wa huyu mwanamke asiyeshughulikiwa na mume wake, pamoja na kuhifadhi uso hasi wa yule mume asiyemshughulikia bibi yake.

19. Mzungumzaji B: Ni vipi hashughulikiwi msikilizaji?

Mzungumzaji A: Ni vyema kutoyataja hayo ili kutomwaibisha bibi huyo.

Kupitia kwa mifano hii, wazungumzaji wanakataa kuwasilisha taarifa fulani kuhusu wasikilizaji wao. Wazungumzaji wanakataa kuwasilisha taarifa ili waepukane na kauli ambazo zinaweza kutisha au hata kudhuru nyuso za wasikilizaji wao. Kwa kutowasilisha taarifa fulani ambayo wanafahamu kuhusu wasikilizaji wao, wale wazungumzaji hawahifadhi tu nyuso za wasikilizaji wao, bali wanahifadhi pia mahusiano yaliyopo baina yao.

Hata hivyo, mkakati huu wa kutowasilisha taarifa una athari zake kwani msemaji mara nyingi hafikii malengo yake. Lazima ikumbukwe kuwa, watu wanapoingilia mazungumzo, huwa wana mambo muhimu ambayo wao hutaka kujadili. Kwa hivyo, ingawa mkakati huu una kiwango kikubwa cha upole, msemaji huwa hafikii malengo yake kwa sababu ya kunyamazia mambo ambayo ni muhimu katika majadiliano yoyote, mzungumzaji akiyafanya haya yote ili kuonyesha upole katika mawasiliano.

#### **2.4.2 Matumizi ya Maneno Kiufundi**

Huu ni mkakati wa pili ambao hutumika katika kukabiliana na kauli ambazo hutisha nyuso za wanaohusika katika mazungumzo. Matumizi ya maneno kiufundi hufafanuliwa kama mikakati



chanya ya upole. Mkakati huu hudhamiria kuokoa nyuso chanya za watu wanaohusika katika mazungumzo kwa kutumia ufundi fulani wa maneno.

Mkakati huu huweza kujihusisha na kuonyeshwa heshima kwa msikilizaji. Anayemwonyesha msikilizaji heshima ni mzungumzaji hasa wakiwa katika harakati ya kujadiliana kuhusu jambo fulani. Msikilizaji anapoonyeshwa heshima katika mazungumzo, yeye hujiunga na yule mzungumzaji katika kufanya juhudi ya kuhakikisha kuwa mazungumzo yanafikia malengo yake.

Kuonyesha heshima katika mazungumzo huweza kuwa njia mojawapo ya kudhihirisha hisia za mzungumzaji kwa msikilizaji wake. Anayeonyesha wenzake heshima huwadhihirishia kuwa anawathamini sana, pamoja na kuwa, anatambua kuwa wasikilizaji wale wametenga muda ili kujiunga naye katika mazungumzo yanayoendelea. Kwa hivyo matumizi ya maneno kiufundi husaidia katika kuhakikisha kuwa, wote wanaohusika katika mazungumzo huonyeshwa heshima, kupitia kwa matumizi ya maneno yaliyojaa upole.

20. Becky: Asante sana Daktari Labaan Shabaan ukiwa mkereketwa wa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Labaan: Nashukuru sana Becky.

Kauli yake Becky katika mfano huu ni ithibati tosha kuwa, uso chanya wa Laaban unaokolewa katika mazungumzo haya kwani Laaban anatambuliwa katika maongezi haya, pamoja na kusifiwa kwa kuitwa mkereketwa wa lugha. Katika kutambua wadhifa wake msikilizaji huyu, Becky anamwonyesha heshima hivyo, kuhakikisha kuwa thamana yake inatambulika kwa wote.

21. Mzungumzaji: Nakuambia mama, mfalme yule alikuwa amefikia umri wa kufa kama wa nyanya...

Msikilizaji: Ukweli kabisa, nyanya yako ameshakula chumvi nyingi...

Kupitia kwa mfano huu, mzungumzaji anaamua kumtambia mama yake hadithi ya mfalme mmoja na kusema kuwa, mfalme anayemtaja katika hadithi hiyo yake alikuwa amezeeka. Mzungumzaji analinganisha umri wa mfalme anayemzungumzia na ule wa nyanya yake. Hata hivyo, mzungumzaji huyo anaonyesha umri wa mfalme kwa kutumia maneno kiufundi, hivyo kuuokoa uso wake nyanya yake.

Katika kauli yake mzungumzaji huyu, matumizi ya mikakati chanya ya upole imetumika katika kuonyesha umri wa nyanya yake mzungumzaji. Mzungumzaji anaonyesha kuwa nyanya yake

ana miaka nyingi lakini ufundi wake wa maneno, ambao hauwezi kufasiriwa na kila mtu, unamfanya kuokoa uso chanya wa nyanya yake.

Brown na Levinson (1987: 101) wanafafanua mkakati wa upole unaokoa uso chanya wa aidha msikilizaji au mzungumzaji kuwa kile kinachoelekezwa kwa uso chanya wa msikilizaji yeyote pamoja na matarajio ya msikilizaji kuwa, mahitaji yake yaweze kuchukuliwa kama yale ambayo yanatamanika katika hali zote. Mkakati huu huashiria kuwa mzungumzaji na msikilizaji ni washiriki katika jambo fulani na wana msimamo sawa katika mambo wanayoyatekeleza.

### **2.4.3 Kuafikiana katika Mazungumzo**

Huu ni mkakati wa tatu wa kukabiliana na kauli ambazo huwa tishio kwa nyuso za wazungumzaji pamoja na wasikilizaji. Msemaji huwa na uwezo wa kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kutafuta maafikiano naye. Hii huwezeshwa na msemaji kuchagua mada au jambo ambalo hukubalika katika mazungumzo na kuhakikisha kuwa mjadala wao unaongozwa na mada inayokubalika katika mazungumzo.

Mambo yanayokubalika katika mazungumzo ni yale mambo ambayo hayaleti mkwaruzano wowote, na ambayo hayawatii aibu wote wanaohusika katika mazungumzo. Kule kumfahamu msikilizaji humfanya mzungumzaji yeyote kuyafahamu mambo ambayo msikilizaji hukubaliana nayo na vile vile, yale ambayo hakubaliani nayo.

22. Mzungumzaji: Kamilisha hadithi yako Jane.

Msikilizaji: Lazima niwaambie hadithi yangu kwanza.

Jane: Naelewa shida yako, maliza yako kwanza kisha unipe nafasi.

Mzungumzaji kupitia kwa mfano huu anamwomba Jane kukamilisha hadithi aliyokuwa akiwatambia. Msikilizaji anaingilia kati na kutaka kuitamba hadithi yake kwanza, kisha Jane anamwambia Msikilizaji kuwa hakuwa na shida yoyote, na kuwa angeikamilisha hadithi yake baadaye. Jane ameweza kuokoa uso chanya wa Msikilizaji kwa kukubali kuwa Msikilizaji yule aweze kumaliza hadithi yake kwanza kisha yeye atamaliza kutamba hadithi yake baadaye.

Kwa kufanya hivi, Jane amemhusisha Msikilizaji katika shughuli hiyo ya kutamba hadithi. Vile vile, ameepusha majibizano kati yake na msikilizaji, majibizano ambayo yanaweza kumtia aibu Msikilizaji kwani yeye ndiye ameingilia mazungumzo kati ya mzungumzaji na Jane.



Majibizano vile vile yanaweza kufanya mawasiliano kukatika. Kwa hivyo, alichofanya Jane ni kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kumhusisha katika mazungumzo yao na kutomwingilia kwa vyovyote vile.

#### 2.4.4 Ucheshi

Msemaji huweza kukabiliana na kauli zinazotisha uso chanya wa msikilizaji kwa kutumia maneno yenye ucheshi. Ucheshi ndio mkakati wa nne wa kudhibiti vitisho kwa nyuso za wazungumzaji. Ucheshi ni hali ya kuwa mchangamfu na mwernye furaha kwa watu. Ucheshi huweza kufafanuliwa kama furaha au bashasha, kwa hivyo, ucheshi huwafanya wanaohusika katika mazungumzo kuchangamkia yale mambo ambayo yanajadiliwa, huku ukihakikisha kuwa viwango vya kutoelewana vinapunguzwa, ili wote wanaowasiliana waonekane kama kitu kimoja.

23. Mzungumzaji: Macho yako yanaweza kumtoa nyoka pangoni.

Msikilizaji: Nafurahia kuwa unayafahamu hayo...

Mzungumzaji kupitia kwa mfano huu anaokoa uso chanya wa msikilizaji wake kwa kumwambia kuwa macho yake yanaweza kumtoa nyoka pangoni, jambo linalozua ucheshi baina ya mzungumzaji na msikilizaji wake. Ucheshi huu umetekelezwa kwa sababu ya kuzungumzia mambo ya kawaida na ambayo yanajulikana na mzungumzaji yule pamoja na msikilizaji wake.

Wale ambao wanamfahamu msikilizaji anayezungumziwa katika mfano huu wanajua kuwa ana macho makubwa makubwa, hivyo, maneno yake mzungumzaji si mageni kwa wote wanaomfahamu msikilizaji. Maneno haya yaliyojaa ucheshi kwa hivyo, yanawafanya wazungumzaji kuliona jambo linalozungumziwa kuwa nyepesi, la kawaida na ambalo haliwezi kuleta mkwaruzano katika hali yoyote.

24. Mzungumzaji: Itabidi wanaokula miraa kuacha kukula miraa nyingi. Unajua leo mwandishi mmoja wa gazeti la 'The Standard' amesema kuwa kukula miraa nyingi inaweza kufanya mtu kutokuwa makini katika chumba cha kulala.

Msikilizaji: Wacha zako, huwa sili miraa, hayo waambie wanaokula miraa.

Kupitia kwa mfano huu, ni dhahiri kuwa mzungumzaji anafanyia utani alichosoma katika gazeti la 'The Standard' kwa kusema kuwa, huenda kazi ikawa ngumu katika chumba cha kulala ikiwa



mtu atatafuna miraa nyingi. Jambo hili ingawa ni la ukweli na ambalo ni swala nyeti katika jamii, linazua ucheshi miongoni mwa mzungumzaji pamoja na msikilizaji wake.

Mzungumzaji ametumia maneno yake kisanaa, akimaanisha kuwa, bwana ambaye ana bibi ataweza kushindwa kumhudumia bibi yake kimapenzi ikiwa atatafuna miraa nyingi. Maneno haya yaliyojaa upole na ambayo yametumika kiufundi yanahakikisha kuwa ujumbe muhimu unapitishwa kwa wale ambao wana mazoea ya kutafuna miraa nyingi, ujumbe huu ukiwafikia hadhira lengwa pekee.

#### **2.4.5 Kuepuka Kutoafikiana**

Katika juhudi za kukabiliana na kauli zinazotisha nyuso za wasikilizaji, wazungumzaji hujaribu kadri wawezavyo kutopingana na wasikilizaji wao. Huko kutopingana na wasikilizaji huwa na dhamira ya kuhakikisha kuwa kuna makubaliano kati ya wazungumzaji na wasikilizaji wao. Vile vile kuepuka kutokubaliana huhakikisha kuwa wazungumzaji na wasikilizaji wanafikia maamuzi kuhusu jambo linalozungumziwa.

Wanafunzi pamoja na Njogu kupitia kwa mfano unaofuata, wanadhihirisha maafikiano wanaposema kuwa, walimu hawana uhusiano wowote na tendo la kuchomwa kwa shule nchini Kenya. Njogu anasema kuwa, pengine kuchomeka kwa shule kunasababishwa na hitilafu ya nguvu za umeme, au hata shurutisho kutoka nje ya shule. Njogu kwa hivyo, anaepuka kutokubaliana na watu katika jamii anapotumia msamiati ambao hautaji jina la mtu yeyote, kuwa anahusiana na kisanga cha kuchomwa kwa shule.

25. Walimu: Sisi hatuna uhusiano wowote na janga hilila kuchomwachomwa kwa shule. Tunaomba mfanye utafiti ili muweze kubainisha chanzo cha janga hili.

Wanafunzi: Walimu wetu hawana uhusiano wowote na janga hili, hata sisi hatujui kinachosababisha moto shuleni.

Njogu: Pengine moto unasababishwa na hitilafu kwenye nguvu za umeme au shurutisho kutoka nje. Walimu ni watu wenye tajriba na hawawezi kuhusika katika mambo kama haya.

Hata ingawa watu katika jamii wanachukulia kuwa walimu wako katika mstari wa mbele kuhusu swala hili la kuchomeka kwa shule nyingi nchini Kenya, Njogu anajaribu kadri awezavyo kutotaja walimu katika kauli yake. Njogu anasema kuwa walimu ni watu wenye tajriba, hivyo hawawezi kujihusisha na janga la kuchomwa kwa shule.

Njogu anafanya haya yote ili kuhifadhi nyuso chanya za wale walimu kwani, walimu ni watu wanaoheshimika katika jamii. Vile vile, walimu hawatarajiwi kuhusika katika janga kama hili kwa sababu wao huwa na jukumu la kuhakikisha kuwa wanafunzi wana adabu. Walimu vile vile ni watu ambao hutaka kusifiwa kila mara kwa kazi ambayo wanatenda shuleni, hivyo, kuwataja katika kisanga kama hiki ni tishio kwa nyuso zao chanya.

#### **2.4.6 Kutumia Maneno yenye Maana Fiche**

Mkakati mwingine wa kukabiliana na vitisho kwa nyuso za wanaohusika katika mazungumzo ni mkakati wa kutumia maneno yenye maana fiche. Mzungumzaji anapotumia maneno kwa njia fiche, yeye hujiondolea lawama kwa kutoibua mkwaruzano kwenye mazungumzo. Hii ni kwa sababu maneno yenye mafumbo huweza kutumika kwa namna inayoibua upole kwa kiwango fulani.

Maneno yanayotumika kwa njia fiche katika mawasiliano hudhamiria kutenga wale ambao hawana uhusiano wowote na mada inayojadiliwa. Lazima ikumbukwe kuwa hata watoto husikiliza vipindi tofauti tofauti vinavyopeperushwa kwenye redio, lakini kuna mambo ambayo hujadiliwa na ambayo hayawahusu kwa vyovyote vile. Hivyo huwa muhimu kutumia maneno yenye maana fiche ili kuwatenga wasiohusika katika mazungumzo. Kuwatenga wasiohusika katika mazungumzo husaidia katika kudumisha siri.

26. A: Nakuambia mama yake huyo kidosho ni simba, atakuuma na kukuponda ugeuke unga.

B: Asante kwa kunisaidia, hebu nijaribu kukanyaga njia nyingine.

Wazungumzaji hawa wawili wanatumia maneno yaliyojaa mafumbo, wakiwa wanazungumzia alivyo mkali mama yake msichana fulani, na kuwa, heri wamtafute msichana mwingine wa kuchumbiana naye. Maneno haya yanawatenga wote ambao hawana uhusiano na mada inayoshughulikiwa na wazungumzaji hawa wawili.

Matumizi ya maneno yenye maana fiche vile vile husaidia katika kuchochea fikra za wasikilizaji. Uchochezi wa fikra huwafanya wasikilizaji kuwa na uwezo wa kuwaza zaidi kuhusu jambo linalozungumziwa. Uchochezi huu wa fikra vile vile huwafanya watu wanaohusika katika mazungumzo kuweza kutoa maoni yao kuhusu kile ambacho kinazungumziwa, hivyo kuwafanya wote kumiliki matokeo yanayotokana na mazungumzo yale.



Kupitia kwa mfano wa ishirini na saba unaotoka katika mandhari ya shule, inathibitika jinsi ambavyo wazungumzaji hutumia maneno kwa njia fiche. Mzungumzaji kupitia kwa mfano huu anasema kuwa, mwalimu wao anayejulikana kama Jude amebakia kuwa moto wa kuotea mbali. Mzungumzaji anatoa sababu ya kusema hivi japo si kwa kina hata anapooombwa na msikilizaji wake kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu kauli yake. Msikilizaji yule anabaki na maswali kuhusu anachomaanisha yule mzungumzaji. Msikilizaji yule kwa hivyo, analazimika kufasiri zaidi alivyo moto wa kuotea mbali yule mwalimu mkuu ajulikanaye kama Jude.

27. Mzungumzaji: Mwalimu mkuu Jude ni moto wa kuotea mbali, hataki mchezo katika kazi yake.

Msikilizaji: Kumbuka huyu mwalimu Jude ni mchapa kazi, tofauti na watangulizi wake ambao hawakuwa wanahudhuria vipindi. Lakini unamaanisha nini unaposema kuwa mwalimu Jude ni moto wa kuotea mbali?

Mzungumzaji: Mwalimu Jude yuko shuleni kila mara. Mengine hata wewe unajionea. Si waona anavyofanya kazi?

Mzungumzaji katika kauli yake anamaanisha kuwa mwalimu Jude sio mtu wa kuchezeza, na kuwa ameamua kuleta mabadiliko katika uongozi wa shule yake kwa kuhakikisha kuwa walimu pamoja na wanafunzi wanahudhuria vipindi vyao kama inavyotakikana. Maneno fiche yanayotumika na mzungumzaji hivyo, yanaibua na kudhihirisha matumizi ya upole kwenye mazungumzo.

Brown na Levinson (1987:211) wanadai kuwa katika mkakati huu wa kusema mambo kwa njia fiche, huwa si rahisi kuhusisha lengo moja wazi katika usemi husika. Cutting (2008:48) naye anadai kuwa uso wa msikilizaji yeyote huweza kuokolewa kutokana na kuwepo kwa afueni katika maana halisi ya yale ambayo yanasemwa, huku msemaji akiokoa uso wake kwa kukataa kusema kauli fulani.

## **2.5 Hitimisho**

Mikakati ya kukabiliana na kauli ambazo hutisha nyuso kwa kutumia maneno yenye upole yameweza kushughulikiwa kwa kina katika sura hii ya pili. Kauli hizo zinazotisha nyuso za wazungumzaji pamoja na wasikilizaji pia zimejadiliwa katika sehemu hii. Mitazamo ya kuokoa nyuso imefanyiwa utafiti, utafiti huu ukitumia Nadharia ya Upole kama ilivyoshughulikiwa na



Brown na Levinson (1978, 1987), Leech (1983), Fraser na Nolen (1981) pamoja na Watts (2003).

Ni muhimu kutambua kuwa, mawazo ya wanaisimu hawa yanasaidia katika kufafanua kanuni ya upole kwenye mazungumzo. Mtazamo wa Leech (1983) ndio umetumika sana katika utafiti huu kwa sababu mitazamo yake kuhusu upole inajumuisha maswala nyeti yanayohusu upole, huku ukitoa kanuni za upole ambazo zinaweza kusaidia katika kukidhi mahusiano kati ya watu wote ambao wanahusika katika mazungumzo.

Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) pamoja na taratibu za upole zinazoweza kutumika kuendesha lugha ya mawasiliano zinachunguzwa katika sura ya tatu ya tasnifu hii. Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) pamoja na taratibu za upole za kuendesha lugha zimesaidia katika kuthibitisha mada ya utafiti huu ambayo ni kanuni ya upole kwenye vipindi “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio Citizen.

## SURA YA TATU

### KAIDA ZA UPOLE KATIKA VIPINDI “JAMBO KENYA” NA “CHAPA KAZI”

#### 3.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia jinsi ambavyo kaida za upole zinaweza kubainika katika mazungumzo. Kanuni za ushirikiano alizoibuka nazo Grice zimesaidia katika kuthibitisha kuwa, wazungumzaji huweza kutumia kaida mbalimbali za upole katika mazungumzo yao. Grice (1975) aliibuka na kanuni za ushirikiano ambazo huwa na lengo la kuhakikisha kuwa mawasiliano yanaendelea kwa njia inayokubalika na mzungumzaji pamoja na msikilizaji wake.

Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975), zimesaidia katika kutofautisha miktadha ya matumizi ya maneno, virai, vishazi pamoja na sentensi katika mazungumzo, pamoja na mahusiano yaliyopo baina ya matumizi ya maneno yenye upole katika maongezi ya kila siku, na lengo la matumizi ya kaida zenye upole katika mazungumzo.

Sura hii inadhamiria kudhihirisha kuwa lugha yenye upole ambayo hutumika katika mawasiliano ya mara kwa mara, hasa katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vinavyopeperushwa katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen, ina umuhimu. Vile vile, sura hii ina nia ya kudhihirisha kuwa, kaida za upole huweza kuhifadhi uhusiano uliopo kati ya mzungumzaji na msikilizaji wake.

Taratibu za kuendesha lugha pia zimesaidia katika kutoa ithibati kuwa upole unatumika katika vipindi viwili vilivyoteuliwa ili kushughulikiwa katika kufanikisha matarajio ya utafiti huu. Taratibu za kuendesha lugha zinatoa ufafanuzi kuwa, mitagusano ya mazungumzo huwa na taratibu zake. Taratibu za kuendesha lugha huashiria kuwa jinsi lugha inavyoendeshwa katika mazungumzo hutegemea mtagusano wa mazungumzo hayo.

Grice (1975) alitoa maelezo kuhusu jukumu la lugha, hasa lugha kimazungumzo. Grice (1975) alidai kuwa, huwa panaibuka ushirikiano fulani watu wawili wanapozungumza. Grice aliendelea kutoa ufafanuzi wa dhana hii kwa kusema kuwa, wazungumzaji huwa watu wenye akili razini, na ambao huwa na haja kuu inayowafanya kuingilia mazungumzo, haja hiyo ikiwa ni kupitisha ujumbe. Katika mazungumzo, wasemaji mara nyingi humaanisha zaidi ya wanayoyasema. Kwa mfano, mzungumzaji anaposema:

## 28. Mzungumzaji: Anne ni fisi mkubwa.

Mzungumzaji huyu anaposema kuwa mtu ajulikanaye kama Anne ni fisi, hamaanishi kuwa Anne ni mnyama, bali anamaanisha kuwa Anne ni mlafi. Lakini lazima ikumbukwe kuwa pengine yule mzungumzaji anamaanisha zaidi ya ulafi, kuwa, pengine Anne ana tabia zingine ambazo zinaweza kulinganishwa na sifa za mnyama huyu ajulikanaye kama fisi.

Kutokana na mtazamo wa upole kama njia ya kudumisha mazungumzo yoyote, Grice (1975) alipendekeza kanuni za ushirikiano, kanuni ambazo ni: Kanuni ya ukweli, kanuni ya namna, kanuni ya idadi pamoja na kanuni ya uhusiano. Kanuni za ushirikiano kijumla hudai kuwa, msemaji yeyote anafaa kutoa mchango wake katika mazungumzo, lakini mchango huo wake, unafaa uwe ule ambao unahusiana na muktadha wa mazungumzo unaoendelezwa na wazungumzaji.

Mwelekeo unaochukuliwa na mchango huo wa mzungumzaji unafaa uwe ule ambao unakubalika katika mazungumzo yanayoendelea. Kanuni hizo za ushirikiano (Grice, 1975) pamoja na jinsi zinavyoweza kuibua upole zinajadiliwa katika sehemu inayofuata.

### **3.2 Kanuni za Ushirikiano (Grice, 1975) Katika Kuibua Upole**

Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) ni kanuni ambazo zinaelekeza wazungumzaji katika kutumia mikakati ya upole kwa kiwango fulani hata bila wao kufahamu. Jambo linalobainika kwa wote ni kuwa, wazungumzaji wasiposhirikiana na wasikilizaji wao katika mazungumzo, basi kufikia malengo ya mawasiliano itakuwa tukio gumu la kuafikiwa. Kanuni za Ushirikiano (Grice, 1975) zinaweza kutazamwa kwa pande mbili, pande ambazo zinasaidia katika kuhakikisha kuwa mazungumzo yanaendelea bila shida.

1. Kuwa wasemaji hutia maanani kanuni za ushirikiano katika mazungumzo yao.
2. Wasikilizaji huchukulia kuwa wasemaji wamezingatia kanuni za ushirikiano katika mazungumzo yao.

Wasemaji wanapozingatia kanuni ya ushirikiano katika mazungumzo yao, mitagusano baina yao na wasikilizaji wao huwa jambo dhahiri kabisa, jambo linalobainika kwa wote. Hii ni kwa sababu kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) husaidia katika kukuza uhusiano kati ya watu wanaowasiliana.



Kanuni hizi za ushirikiano huweza kuibua umaanisho, umaanisho ambao huashiria kuwa, maana ya nje ya sentensi huweza kukosa kufuata kanuni za ushirikiano (Grice, 1975), jambo ambalo humfanya msikilizaji kuwa na jukumu la kufanya utafiti kuhusu maana ya tamko ambalo limetamkwa na mzungumzaji.

Umaanisho huashiria kuwa, mara nyingine msikilizaji hulazimika kufanya utafiti kuhusu maana ya usemi unaotoka kwa mzungumzaji. Umaanisho huweza kutokea wakati ambapo mzungumzaji ameamua kutumia maneno ambayo yanamlazimisha msikilizaji kufikiri zaidi ili kuweza kupata maana ya maneno yanayotoka kinywani mwa mzungumzaji. Vile vile, umaanisho huweza kutokea wakati ambapo mzungumzaji amekosa kufuata kanuni za ushirikiano (Grice, 1975).

Ushirikiano huleta maelewano na utangamano katika mazungumzo. Maelewano ni hali ya kusikilizana. Wazungumzaji na wasikilizaji wanaposikilizana, mawasiliano hufikia malengo yake. Kwa hivyo linaweza kuwa makisio kuwa, katika kuibuka na kanuni za Ushirikiano, Grice (1975) alikuwa na nia ya kuwaonyesha wanaoshiriki katika mazungumzo jinsi ambavyo wanaweza kutagusana kwa njia inayotosheleza bila kuzua malumbano.

Lazima ikumbukwe kuwa, si watu wote wana uwezo wa kufuata kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) kila mara katika matamshi yao. Mzungumzaji huweza kuvunja kanuni hizo za ushirikiano akiwa na nia ya kuweza kueleweka na wale anaozungumza nao. Tofauti na kutaka kueleweka katika mazungumzo, mzungumzaji huweza kuvunja kanuni za ushirikiano ili kuibua upole katika mazungumzo hayo.

Yule (1996) anakubaliana na kauli hii ya kuvunjwa kwa kanuni fulani za ushirikiano kwa kusema kuwa, kuna zaidi katika umaanisho, zaidi ya yanayosemwa katika mazungumzo. Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) zinatumiwa katika sehemu zinazofuata ili kutathmini ikiwa mazungumzo kati ya wahusika wa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya Redio Citizen yanadhihirisha kufuatwa kwa kanuni za ushirikiano.

### **3.2.1 Kanuni ya Ukweli Katika Kujenga Mawasiliano**

Kulingana na kanuni ya ukweli, Grice (1975) alisema kuwa, mzungumzaji lazima aseme mambo ya ukweli katika mazungumzo yoyote, na kwamba mzungumzaji lazima awe na ushahidi wa kutosha kuhusu yale yote asemayo. Ukweli ni hali ya mzungumzaji kuwa na uhakika katika yale

anayoyasema. Mzungumzaji anapokuwa na uhakika katika mambo anayoyasema, basi hatakuwa na shaka kuwa anayoyasema pengine yanaweza kumtia matatani.

Mambo ambayo msemaji huweza kuyatolea ithibati lazima yachukue usukani katika mazungumzo. Katika kutoa ithibati, mzungumzaji huweza kutoa ufafanuzi wa dai lake. Vile vile mzungumzaji huwa na ushahidi kuhusu yale anayoyasema. Francis Luchivia anatoa ithibati ya kuwepo kwa matumizi ya kanuni ya ukweli katika kipindi cha “Jambo Kenya” cha Redio Citizen anaposema kuwa:

29. Luchivia: Ni dhahiri kuwa idadi ya waja wazito wanaoaga dunia ncini Kenya imeenda chini...

Wilbroda: Shukrani nyingi zielekezwe kwa Bi. Kenyatta kwa anayowatendea wanawake...

Matamshi haya ya Luchivia yanayotoka kwa kipindi cha “Jambo Kenya” yanadhihirisha ukweli. Hii ni kwa sababu ya sera zilizotolewa na serikali kuhusu huduma inayotolewa kwa waja wazito katika hospitali mbali mbali. Kwanza kuna ambulensi za kutosha katika hospitali nyingi nchini Kenya, ambulensi zinazotumika katika kuwahudumia wagonjwa. Vile vile, wanawake wanajifungua bila malipo yoyote, swala ambalo linawafanya hata wale wasiojiweza kuenda hospitalini ili kujifungua huko.

Swala hili la kutolipia huduma hospitalini imewafanya wanawake wengi kutotafuta huduma kwa akina mama wanaoaminika kuwa na uwezo wa kuwasaidia wanaopitia machungu ya kujifungua. Wanawake wengi wameamua kutafuta huduma hiyo muhimu hospitalini, hivyo, maisha ya wanawake wengi yameweza kuokolewa. Luchivia kwa hivyo, ana uwezo wa kutoa ithibati kuhusu kauli yake.

Hata hivyo, anapoyazungumzia swala hili la idadi ya waja wazito wanaoaga dunia kupungua, pengine Luchivia hafahamu kuwa anatumia kanuni ya ukweli ya Grice (1975) katika matamshi yake. Hili ni jambo ambalo linafaa kueleweka kwa watumizi lugha kuwa, wakati mwingine mzungumzaji huweza kutumia mojawapo ya kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) katika maongezi yake bila kufahamu.

Kupitia kwa mfano wa thelathini, mfano unaotoka katika kipindi cha “Jambo Kenya”, Wilbroda anasema kuwa, Ringera anadai kuwa walioondolewa kama majaji walijaa virusi vya ufisadi.



Wilbroda anaendelea kusema kuwa, kulingana na aliyoyasoma gazetini, pamepatikana ushahidi wa kutosha wa kuweza kudhibitisha kuwa majaji hao walikuwa wafisadi.

30. Wilbroda: ...Ringera ameamua kuwatimua majaji waliojawa na virusi vya ufnisadi...

Luchivia: Sote twafaa kupiga vita ufnisadi...

Wilbroda kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, anatumia neno ufnisadi ili kuonyesha upole wa kiwango fulani katika matamshi yake, na vile vile kuhifadhi nyuso hasi za majaji wale walioachishwa kazi. Wilbroda ana uhakika na yale anayoyasema na anaweza kuyatolea ushahidi kupitia kwa kilichochapishwa kwenye gazeti. Ushahidi unaoweza kutolewa kutoka kwa gazeti unamfanya Wilbroda kuwa mmoja wapo kati ya wale wanaotumia kanuni ya ukweli katika matamshi yao. Matumizi ya neno ufnisadi yanaibua upole kwa sababu neno hili halionyeshi wazi au halionyeshi moja kwa moja kuwa mtu ni mwizi, bali linaficha ukweli uliopo.

### 3.2.2 Kanuni ya Idadi Katika Kuimarisha Makubaliano

Kupitia dai la kanuni ya idadi, Grice (1975) alitoa pendekezo kuwa, mzungumzaji anapaswa kuzungumza kwa idadi inayofaa. Kuwa mzungumzaji asizidi wala asipunguze idadi ya maneno inayokubalika katika mazungumzo yoyote, ili kuweza kuleta maelewano kati yake na msikilizaji wake. Kanuni ya idadi husaidia katika kuhakikisha kuwa mzungumzaji hawachoshi wasikilizaji kwa kusema mambo yasiyo na mantiki.

31. Syombua: Jerida, tunafaa tuwaombe watoto wetu maanake wana uzoefu wa kujaribu mambo yanayowaumiza. Leo hii katika shule ya Bongean mwanafunzi ameaga dunia baada ya kuunda pombe kutokana na kemikali ya ‘ethanol’ aliyochanganya na soda...

Jerida: Unayoyasema yanasikitisha sana Syombua. Walimu walikuwa wapi alipokuwa akiyafanya haya?

Syombua: Wakuu wa serikali watafanya uchunguzi, mengine tutajua baadaye.

Jerida kupitia kwa kipindi cha “Chapa Kazi” anapotaka kujua zaidi kuhusu alivyoaga dunia yule mwanafunzi na walipokuwa walimu mwenda zake alipokuwa akichanganya kemikali hiyo na soda, Syombua anamwambia kuwa, aliyomwambia yametosha na kwamba yaliyobakia ni kazi ya wakuu wa serikali kufanyia uchunguzi, ili waweze kutathmini kilichosababisha kifo cha



mwanafunzi huyo. Syombua anahifadhi uso hasi wa Jerida kwa kutomwingilia, huku akihakikisha kuwa ametaja mambo ambayo yanafaa kutajwa pekee.

### **3.2.2.1 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Idadi Katika Kuleta Maelewano**

Lazima ikumbukwe kuwa kuna wakati ambapo mzungumzaji huweza kuvunja kanuni hii ya idadi. Kanuni ya idadi huvunjwa mzungumzaji anapoamua kusema mambo mengi, ambayo yanazidi kiasi kinachohitajika. Mzungumzaji huweza kulazimishwa kuvunja kanuni hii ya idadi ili aweze kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu mada aliyokuwa akizungumzia, hasa ikiwa wasikilizaji wake hawaelewi anachozungumzia. Hii ni kwa sababu, kila mara, lengo la mzungumzaji katika mazungumzo huwa ni kuhakikisha kuwa ujumbe wake umefikia hadhira lengwa kwa njia toshelezi.

Syombua akizungumza kuhusu kuja kwake Papa Francis nchini Kenya, anatoa sababu ya kujulikana kama baba mtakatifu yule papa Francis. Anavunja kanuni ya idadi kwa kusema zaidi ya yanayohitajika katika mazungumzo yake. Syombua anasema kuwa, jina Baba Mtakatifu linaambatana na matendo yake Papa Francis kwani moyo wake Papa Francis hudundadunda kila asikiapo maswala ya wanyonge.

Syombua kupitia kwa kipindi cha “Chapa Kazi” anaendelea kutoa mfano wa mzazi yeyote anavyohisi machungu mwana wake anapopatwa na mabaya, na kulinganisha haya na anavyohisi Papa Francis kila anapozungumza kuhusu wanyonge. Syombua kwa hivyo, anatoa makisio kuhusu sababu ya Papa Francis kujulikana kama Baba Mtakatifu.

32. Syombua: ...Kila mtu anafahamu jinsi ambavyo wazazi hupatwa na machungu mabaya yanapowapata watoto wao. Hivyo ndivyo anavyohisi Papa Francis wanyonge...

Jerida: Tunamshukuru Mola kwa kumpa moyo huo...

### **3.2.3 Kanuni ya Namna Katika Kuepuka Utata**

Grice (1975) anadai kuwa, msemaji anafaa kusema mambo kwa njia wazi, njia isiyowachanganya wasikilizaji wake, njia inayoeleweka kwa wote. Maneno yanafaa kusemwa jinsi yalivyo bila kutumia maneno yyenye kukanganya. Hii inamaanisha kuwa, mambo ambayo yanazungumziwa au maneno ambayo yameteuliwa kutumika, hayatarajiwi kuleta utata wowote

katika mazungumzo. Hii ni kwa sababu utata unaojitokeza katika mazungumzo yoyote huweza kumfanya msikilizaji kufasiri ujumbe kwa njia isiyofaa, hivyo, kanuni ya namna huhakikisha kuwa ujumbe unaeleweka jinsi alivyokusudia mzungumzaji.

33. Linkon: Uhasama kati ya wanafunzi wa makabila mbili tofauti umefanya chuo hicho kufungwa kwa muda usiodhihirika...

Linkon anapotoa matangazo ya habari anasema kuwa, chuo kikuu cha Maasai Mara kimefungwa baada ya kuzuka uhasama kati ya wanafunzi wa makabila mbili tofauti. Ni wazi kuwa, Linkon anachorea watangazaji pamoja na wasikilizaji wa Redio Citizen picha akilini mwao, picha inayoonyesha kuwa, swala la ukabila limeweza kufika katika vyuo vikuu nchini Kenya. Linkon hataji majina ya makabila hayo mawili, hivyo basi kuokoa nyuso hasi za watu wa makabila hayo.

Watu wengi wanafahamu maana ya ufisadi, kwa hivyo, Linkon anapozungumzia swala hili, watu wote wana uwezo wa kumwelewa, hivyo, kutopata ugumu wowote wa kufasiri anachomaanisha yule Linkon. Vile vile, watu wanafahamu maana ya ufisadi. Hii ni dhihirisho tosha kuwa Linkon amezingatia kanuni ya namna katika mazungumzo yake.

### **3.2.3.1 Kuvunjwa kwa Kanuni ya Namna Katika Mazungumzo**

Kanuni ya namna huweza kuvunjwa katika mazungumzo ikiwa mzungumzaji analenga tu hadhira fulani. Hii ni kwa sababu watu wengi husikiliza vipindi tofauti tofauti vya Redio wakiwemo watoto pamoja na watu wazima. Hivyo, ujumbe unaopitishwa ukiwa ujumbe wa watu wazima kwa mfano, mzungumzaji huweza kutumia maneno yenye mafumbo ambayo hayataeleweka kwa watoto wadogo bali yataeleweka kwa watu wazima pekee.

34. Jerida: Inastaajabisha kuwa wasichana siku hizi hawavai shimizi. Baada ya kuvaa kifuniko cha asali, basi tosha!

Syombua: Wanasema hiyo ndiyo fashoni ya sasa.

Mfano huu unaotoka kwa kipindi cha “Chapa Kazi” ni ithibati tosha kuwa wazungumzaji huweza kuvunja kanuni hii ya namna, bila wao kufahamu au hata wakiwa wanafahamu. Anachosema Jerida katika mfano huu, haueleweki kwa watoto na hata kwa wengine ambao wameshabaleghe. Hii ni kwa sababu si watu wote wanafahamu kinachosimamiwa na kifuniko cha asali. Jerida kwa hivyo, anavunja kanuni ya namna kwa kusema maneno kwa njia isiyowazi.

### 3.2.4 Kanuni ya Uhusiano Katika Kufanikisha Kinachosemwa

Kanuni ya uhusiano ni kanuni ambayo inadai kuwa msemaji anafaa kuyasema mambo ambayo yanahusiana na mada ya mazungumzo husika. Kwamba, msemaji asizungumze kuhusu masuala ambayo hayana mantiki katika mazungumzo yanayoendelea. Maswala ambayo hayana mantiki ni yale ambayo hayana mtiririko wa fikra ambazo zimepangwa ili kujenga hoja inayokubalika.

35. Mwala: Jana mtoto katika kaunti moja humu nchini alifukuzwa shuleni kwa sababu alipigana na mwalimu...

Luchivia: Watoto wetu wamekosa nidhamu shuleni kwa kuwa wengi wao wamejiingiza katika unywaji wa pombe...

Mwala: Pombe haramu inayouzwa mitaani...

Mfano huu unaotoa sababu ya kuongezeka kwa utovu wa nidhamu katika baadhi ya shule zinazopatikana nchini Kenya unatolewa na Luchivia kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya”. Luchivia anatoa mfano wa jinsi wanafunzi wengi siku hizi hujihusisha na unywaji wa pombe haramu, jambo linalowafanya wanafunzi kukosa kutia maanani wanayoambiwa na walimu wao wakiwa shuleni.

Pombe huwa na athari kubwa sana katika maisha ya binadamu, na huweza kumfanya yeyote kuropokwa na maneno au hata kutumia maneno yaliyojaa matusi katika maongezi yake. Haya yanajitokeza katika kipindi cha “Jambo Kenya” cha Redio Citizen.

Mambo anayosema Luchivia yanahusiana na mada husika kwani mambo haya yana mantiki na mazungumzo yanayoendelea, mada husika ikiwa ni utovu wa nidhamu katika baadhi ya shule nchini Kenya. Kulingana na matamshi ya Luchivia, unywaji wa pombe miongoni mwa wanafunzi ni kisababishi cha utovu wa nidhamu katika baadhi ya shule.

Grice (1975) hata hivyo aliendelea kusema kuwa, wakati mwingine kanuni hizi huweza kuvunjwa kwa kusudi fulani. Kwa mfano, wakati mwingine, mtu huweza kusema mambo kwa njia isiyo wazi ama hata kusema uongo. Kutosema mambo kwa njia iliyo wazi pamoja na kusema uongo hufanyika ili kuleta ushirikiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji wake. Vile vile, haya huweza kufanywa ili kuonyesha upole katika mazungumzo.



Kuvunjwa kwa kanuni hizi huweza kuwa na sababu za kimakusudi au sababu zisizo za kimakusudi. Msemaji huweza kuvunja kanuni hizi ili kuibua athari hasi ya kipragmatiki au hata kufanya wasikilizaji wake kuelewa zaidi anachomaanisha katika mazungumzo yake.

Lakoff (1973) akitolea ufafanuzi dhana ya upole, aliweza kutumia kanuni ya ushirikiano (Grice, 1985). Lakoff (1973) anadai kuwa, upole ni njia ya kuepuka mkwaruzano katika mawasiliano. Lakoff (1973) aliendelea na kazi ya Grice (1975) kwa kufafanua zaidi dhana ya upole, na kuibuka na vigezo vitatu vya upole. Vigezo alivyoibuka navyo Lakoff (1973) ni:

1. Kumpa mtu uhuru wa kuamua anachotaka.
2. Kuhakikisha kwamba msikilizaji anahisi vyema.
3. Kutolazimisha ukweli kwa mtu fulani.

Vigezo hivi vitatu vya upole ni muhimu kwa sababu vinasaidia katika kuhakikisha kuwa mazungumzo yanaendelea kwa njia inayofaa. Ushirikiano kwenye mawasiliano unaweza kudumishwa wanaohusika katika mazungumzo wanapopewa uhuru wa kufanya muamuzi kuhusu wanachokitaka. Kuhakikisha kuwa msikilizaji anahisi vyema pamoja na kutolazimisha ukweli kwa msikilizaji au hata mzungumzaji, ni mikakati ya upole ambayo inaweza kutumika katika kuhakikisha kuwa mazungumzo yanahitimu mahitaji yake. Vile vile, vigezo hivi vitatu husaidia katika kuokoa nyuso za wote wanaohusika katika mazungumzo.

### **3.3 Taratibu za Upole za Kuendesha Lugha Katika Mawasiliano**

Taratibu maalum za upole huweza kutumika katika kuhakikisha kuwa mawasiliano yanaendelea kwa njia toshelezi. Taratibu za upole zinazotumika katika mazungumzo husaidia katika kuhakikisha kuwa mawasiliano yanafikia lengo linalokusudiwa. Lengo linalokusudiwa katika mazungumzo ni kupitisha ujumbe kwa wale wanaolengwa. Leech (1983) anadai kuwa, mazungumzo lazima yaendeshwe kwa utaratibu ili maana inayoibuka kutoka kwa ujumbe uweze kueleweka kwa wote wanaohusika katika mazungumzo.

Mzungumzaji huweza kulazimishwa kutumia maneno kwa njia ambayo si ya kawaida kwa sababu anadhamiria kupitisha ujumbe wake kwa njia toshelezi. Mzungumzaji vile vile anaweza kutumia lugha kwa njia mbadala kulingana na mahitaji, tajriba au umri wa wasikilizaji wake.

Kwa mfano, mara nyingine mzungumzaji huweza kusema mambo kinyume na anachomaanisha ili asimkwaze msikilizaji wake.

### 3.3.1 Matumizi ya Taadhima Katika Kuibua Upole Kwenye Mawasiliano

Taadhima hufafanuliwa kama neno ambalo husimamia heshima, utukufu au unyenyekevu. Taadhima husaidia katika kuibua upole kwenye mawasiliano. Mhusika yeyote anayeingilia mazungumzo anaponyenyekea katika mazungumzo yale, husaidia katika kuhakikisha kuwa mazungumzo yanaendelea kama alivyokusudiwa.

Unyenyekevu kwenye mazungumzo ni muhimu kwa sababu, aidha mzungumzaji au msikilizaji anapojiinua katika mazungumzo au hata mmoja kati ya wanaohusika katika mazungumzo akimdunisha mwenzake, yeye humfanya mwenzake kutojiamini. Kutojiamini kwa msikilizaji huweza kumfanya kutokuwa na ari au hata amu ya kuendelea kushiriki katika mazungumzo. Unyenyekevu huweza kumfanya mzungumzaji kujitweza katika mazungumzo ili aweze kuleta maridhiano. Maafikiano huweza kuleta ushirikiano katika mawasiliano, hivyo kufanya mawasiliano kuendelea kwa njia isiyoleta utata.

36. Wilbroda: Luchivia, wewe ni kigogo, mimi nitasema nini?

Luchivia: Sote ni vigogo...

Wilbroda: Asante kigogo, sikuwa nayafahamu hayo...

Kupitia kwa mfano huu unaotoka kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, Luchivia anasema kuwa yeye pamoja na Wilbroda ni vigogo. Luchivia anatoa kauli hii baada ya kuambiwa na Wilbroda kuwa yeye ni kigogo. Kitendo hiki cha kunyenyekea kwa Luchivia kinazua upole kwa sababu kinamfanya Wilbroda kumshukuru Luchivia na kumwambia kuwa hakuwa anafahamu kuwa yeye ni kigogo.

Taadhima huhusisha sifa ambazo huweza kuelekezwa kwa wanaohusika katika mazungumzo. Sifa hutoa taarifa kuhusu mtu au kitu fulani. Kupitia kwa utaratibu wa kusifu, watu huweza kufahamu tabia ya mzungumzaji au hata msikilizaji. Sifa zinazoelekezwa kwa msikilizaji humfanya kuhisi vizuri, hivyo huweza kutoa mchango wake kwenye mijadala inayoendelea.

37. Mwala: Kigogo, uliyasikia yaliyotendeka...

Luchivia: Ndiyo, tunafaa tuwaelekeze...

Kutokana na mfano wa thelathini na sita na wa thelathini na saba, Mwala na Wilbroda wanasikika wakimwita Luchivia kigogo kila mara. Kigogo ni mtu ambaye ana madaraka makubwa ya kiutawala. Katika kumwita kigogo, Mwala na Wilbroda wanaelekeza sifa zao kwa yule mtangazaji mwenzao ambaye hubadilika na kuwa msikilizaji wao wakati wanamzungumzia. Neno kigogo linavyotumika katika muktadha huu linawafanya wazungumzaji na msikilizaji wao kuungana katika majadiliano kisha kuweza kupitisha ujumbe wao kwa njia inayostahili, na ambayo inakubalika.

Taadhima hujumuisha swala la hesima. Mzungumzaji anapomthamini msikilizaji wake, yeye humtia katika kiwango cha juu na kuonyesha ubora na umuhimu wake katika mawasiliano. Thamana inayoelekezwa kwa msikilizaji huashiria upole kwa sababu ubora wa mtu hauwezi kuonyeshwa kwa kutumia maneno hasi. Thamana ya mtu huonyeshwa kupitia kwa matumizi ya maneno chanya.

38. Jerida: Inastaajabisha kuwa wasichana siku hizi hawavai shimizi. Baada ya kuvaa kifuniko cha asali, basi tosha!

Syombua: Wanasema hiyo ndiyo fashoni.

39. Wilbroda: ... amefukuzwa mwanamke mmoja katika kaunti moja humu nchini kwa sababu alizoea kubadilisha harufu ya hewa.

Mwala: Lakini lazima waelewe kuwa kutoa ushuzi ni jambo ambalo haliwezi kuzuiliwa

Kupitia kwa mifano hii miwili, wasikilizaji wa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” wanaonyeshwa hesima kupitia kwa maneno yaliyoteuliwa na kutumika katika mazungumzo. Ni jambo linalobainika kuwa, wasikilizaji wa vipindi hivi viwili hujumuisha watoto kwa vijana pamoja na wazee. Kupitia kwa mifano hii, wasikilizaji wote wanajifundisha jinsi ya kutumia maneno teule ambayo yanazua upole katika matamshi yao. Maneno haya teule yanayozua upole yanafanya mazungumzo kuhitimu malengo yake pasi na kukatizwa kabla ya kumalizika.

### 3.3.2 Utaratibu wa Kibanta Katika Kuzua Upole Kwenye Mazungumzo

Lugha huweza kutumika kwa ukali, lakini lugha hiyo yenye makali huweza kuzua upole. Mzungumzaji anavyotamka maneno yenye makali, huweza kutoa dhihirisho ya upole kwa kiwango fulani. Ukali katika maneno huweza kudhihirika kupitia kwa kupandishwa au



kushushwa kwa sauti mzungumzaji anapotamka maneno. Vile vile, toni ya mzungumzaji anapotamka maneno huweza kudhihirisha upole wa maneno makali. Utaratibu wa kibanta huweza kusaidia katika kubainisha vipengele vya kiisimu ambavyo husaidia kukuza upole kwenye mawasiliano.

40. Wilbroda: Miguu yako imening'inia kitini.

Mwala: Nayafahamu hayo.

Kupitia kwa mfano huu unaotoka kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, Wilbroda anatamka maneno ambayo yanaweza kumkwaza msikilizaji wake ambaye ni Mwala. Hata hivyo, jinsi anavyoyatamka maneno yale yanadhihirisha upole. Hii ni kwa sababu Wilbroda anayasema kwa toni ya chini pamoja na kuhakikisha kuwa ameshusha sauti yake anapoyatamka maneno haya.

Maneno ya Wilbroda yana ukali na yanaweza kumtia machungu au hata kumwaibisha msikilizaji lakini jinsi anavyotoa kauli yake inamfanya mzungumziwa kutokwazika bali anamjibu Wilbroda kwa upole. Mzungumziwa ambaye ni Mwala anamjibu Wilbroda kwa kusema kuwa anayafahamu yale ambayo mzungumzaji huyo anayasema.

### **3.3.3 Matumizi ya Takrima Kama Mkakati wa Upole**

Mzungumzaji anapotoa ahadi kwa msikilizaji humfanya kuwa na furaha. Ahadi hufafanuliwa kama agano au mapatano. Msikilizaji anapoahidiwa kufanyiwa jambo fulani na mzungumzaji, yeye huwa na hisia chanya kumhusu mzungumzaji yule, pamoja na mazungumzo yanayoendelea. Agano huwa tokeo la mapatano, na mapatano hufafanuliwa kama ulinganifu wa mawazo. Haya ni kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Kiswahili.

41. Syombua: Huo wimbo si mtamu, chagua wimbo mwingine.

Msikilizaji: Wacha tu, sina wimbo mwingine.

Jerida: Usijali mama, Syombua atakuchezea wimbo huo baada ya muda mfupi.

Msikilizaji: Nashukuru sana, ubarikiwe.

Kupitia kwa mfano huu kutoka kwa kipindi cha “Chapa Kazi”, Syombua, mtangazaji wa kipindi cha “Chapa Kazi” anamwambia msikilizaji wa kipindi hicho kuwa wimbo aliochagua si mtamu hivyo anamwomba achague wimbo mwingine.

Msikilizaji anapokwazika kutokana na matamshi ya Syombua, Jerida anamtotea ahadi kuwa wimbo wake utachezwa baada ya muda usiokuwa mrefu. Kupitia kwa jibu la msikilizaji yule baada ya kutolewa ahadi na Jerida, linabainika kuwa ameweza kuwa na furaha kwa sababu hatimaye, matakwa yake yatatimizwa. Kwa hivyo, ni bayana kuwa maneno yenye upole na ambayo yanatoa ahadi kwa msikilizaji yanasaidia katika kukuza uhusiano uliopo baina ya wazungumzaji hawa na msikilizaji wao.

### **3.3.4 Matumizi ya Tasfida Katika Kuleta Mapatano Kwenye Mazungumzo**

Tasfida hufafanuliwa kama matumizi ya maneno ambayo hayaibui hisia hasi katika harakati ya kutoa maelezo kuhusu dhana, ambazo huweza kukera yanaposemwa. Tasfida vile vile huweza kufafanuliwa kama matumizi ya maneno ambayo yamejaa adabu. Matumizi ya maneno yaliyojaa adabu kwenye mawasiliano husaidia katika kuonyesha kuwa wote wanaoingilia mazungumzo wana umuhimu. Matumizi ya tasfida vile vile huhakikisha kuwa mazungumzo yanaendelezwa kwa njia inayotosheleza.

42. Luchivia: Ni dhahiri kuwa idadi ya waja wazito wanaoaga dunia ncini Kenya imeenda chini...

Wilbroda: Shukrani nyingi zielekezwe kwa Bi. Kenyatta kwa anayowatendea wanawake...

Maneno anayoyatumia Luchivia katika matamshi yake yanadhihirisha matumizi ya tasfida. Luchivia kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya” anatumia maneno yaliyojaa heshima katika matamshi yake. Kupitia kwa mfano wa 42, Luchivia anatumia maneno ‘waja wazito’ badala ya ‘walio na mimba’. Vile vile, Luchivia anatumia maneno ‘aga dunia’ badala ya ‘kufa’. Maneno ‘wenye mimba’ pamoja na ‘kufa’ yanachukiza yanapotamkwa. Kwa hivyo, Luchivia anateua maneno yake, maneno ambayo yanadhihirisha heshima.

Taratibu za kuendesha lugha zinasaidia katika kuibua upole kwenye mawasiliano. Hii ni kwa sababu taratibu hizo zinasaidia wazungumzaji kufahamu hatua ambazo wanaweza kuchukua katika kuteua maneno wanayoyatumia katika mazungumzo yao.

### **3.3.5 Kujitweza Katika Kuleta Maridhiano Kwenye Mazungumzo**

Kaida hii hutoa ufafanuzi wa msemaji kujidunisha na kuzidisha kauli ya kujitweza katika mazungumzo baina yake na msikilizaji wake. Msaada huweza kuombwa katika kaida ya kujitweza, huku msikilizaji akipata sifa katika jambo linalozungumziwa.

43. Syombua: Huo wimbo si mtamu, chagua wimbo mwingine.

Msikilizaji: Wacha tu, sina wimbo mwingine.

Jerida: Usijali mama, Syombua atakuchezea wimbo huo baada ya muda mfupi.

Kupitia kwa mfano huu unaotoka katika kipindi cha “Chapa Kazi”, inambidi Jerida kujidunisha mbele ya msikilizaji wake pamoja na mtangazaji mwenzake. Hii ni baada ya Jerida kutambua kuwa matamshi yake Syombua yamemkwaza msikilizaji yule, na kuwa msikilizaji yule hataki tena kushiriki kwenye mazungumzo yale.

Kaida ya kujitweza kwa hivyo, huwa na lengo la kuhakikisha kuwa yeyote anayeingilia mazungumzo hakwaziki, bali anafurahia na kuridhishwa na mazungumzo yanayoendelea kati yao. Katika kufanya hivi, uhusiano baina ya mzungumzaji na msikilizaji wake hudumishwa, huku mitagusano kati yao ikionekana kuwa jambo rahisi linaloweza kutimizwa na hao wote ambao wanajihusisha na dayalojia inayoendelea.

### **3.3.6 Ufundi wa Kusema katika Kuleta Ushirikiano**

Mkakati huu wa kutumia maneno kiufundi huweza kujihusisha na kuonyeshwa heshima kwa msikilizaji. Anayemwonyesha msikilizaji heshima ni mzungumzaji hasa wakiwa katika harakati ya kujadiliana kuhusu jambo fulani. Msikilizaji anapoonyeshwa heshima katika mazungumzo, yeye hujiunga na yule mzungumzaji katika kufanya juhudi ya kuhakikisha kuwa mazungumzo yanafikia malengo yake.

Kuonyesha heshima katika mazungumzo huweza kuwa njia mojawapo ya kudhihirisha hisia za mzungumzaji kwa msikilizaji wake. Anayeonyesha wenzake heshima huwadhihirishia kuwa anawathamini sana, pamoja na kuwa, anatambua kuwa wasikilizaji wale wametenga muda ili kujiunga naye katika mazungumzo yanayoendelea. Kwa hivyo matumizi ya maneno kiufundi



husaidia katika kuhakikisha kuwa, wote wanaohusika katika mazungumzo huonyeshwa heshima, kupitia kwa matumizi ya maneno yaliyojaa upole.

44. Mwala: Nakuambia mama, mfalme yule alikuwa amefikia umri wa kufa kama wa nyanya yangu.

Wilbroda: Ukweli kabisa, nyanya yako ameshakula chumvi nyingi...

Kupitia kwa mfano huu wa kipindi cha “Jambo Kenya”, Mwala anaamua kumtambia Wilbroda hadithi ya mfalme mmoja na kusema kuwa, mfalme anayemtaja katika hadithi hiyo yake alikuwa amezeeka. Mwala analinganisha umri wa mfalme anayemzungumzia na ule wa nyanya yake. Hata hivyo, Mwala anaonyesha umri wa mfalme kwa kutumia maneno kiufundi, maneno yanayoibua upole kwenye mazungumzo haya.

Katika kauli yake mzungumzaji huyu, matumizi ya mikakati chanya ya upole imetumika katika kuonyesha umri wa nyanya yake mzungumzaji. Mzungumzaji anaonyesha kuwa nyanya yake ana miaka nyingi lakini ufundi wake wa maneno unasaidia katika kudumisha upole kwenye matamshi yake.

### **3.4 Hitimisho**

Kaida za upole ambazo zinachangia katika kufanikisha matumizi ya upole kwenye mawasiliano zimeshughulikiwa katika sura hii ya tatu. Kama ilivyojadiliwa kwenye sura hii, ni jambo linalobainika wazi kuwa, kanuni za ushirikiano (Grice, 1975), zimebainisha kuwa maneno yenye upole hutumika katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”, vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen. Taratibu mbali mbali za kuendesha lugha pia zimeshughulikiwa katika sura hii. Taratibu hizo za kuendesha lugha zimetumika katika kutoa ithibati kuwa, hatua tofauti tofauti na mikakati mbali mbali inaweza kutumika katika kuibua upole kwenye mazungumzo yanayoendelea kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

## **SURA YA NNE**

### **UTEUZI WA ELEMENTI ZA LUGHA KATIKA KUFANIKISHA UPOLE KWENYE MAWASILIANO**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inachunguza na kubainisha elementi za lugha ambazo zinafanikisha upole kwenye mawasiliano. Vipengele vya kiisimu kama vile neno, virai, vishazi na sentensi vinajadiliwa katika sehemu ya 4.2 huku sehemu ya 4.3 ikichunguza mbinu za lugha ambazo zinaweza kuibua upole katika mazungumzo, hasa katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio Citizen. Mbinu za lugha zinazochunguzwa katika sura hii ni kinaya, chuku pamoja na sitiari.

#### **4.2 Uteuzi wa Vipengele vya Kiisimu Katika Kufanikisha Upole**

Kuna vipengele vya kiisimu vinavyosaidia katika kufanikisha matumizi ya upole katika mawasiliano yoyote. Vipengele vya kiisimu hujitokeza katika kitengo cha sarufi kwenye lugha. Dhana hii ya sarufi huweza kufafanuliwa katika miktadha miwili, miktadha ambayo ina mahusiano kwa kiwango fulani. Kwanza, sarufi huweza kufafanuliwa kama taaluma ambayo hujikita katika kuchambua lugha. Lugha inayochambuliwa huwa na viwango tofauti tofauti, viwango hivyo vikiwa: Kiwango cha mofolojia, kiwango cha fonolojia na kiwango cha sintaksia.

Pili, sarufi huweza kufafanuliwa kama kanuni au sheria ambazo huwa na uwezo wa kuvitawala kila kimoja cha viwango vya lugha. Dhana hizi mbili za ufafanuzi wa sarufi zina uhusiano kwani, uchambuzi wa fonolojia, mofolojia na sintaksia ya lugha unahusisha ubainishaji wa kanuni au utaratibu ambao unajenga kila kimoja wapo cha viwango vya lugha, viwango hivyo vya lugha vikiwa fonolojia, mofolojia na sintaksia.

Vipengele vya kiisimu vinavyofanikisha kanuni ya upole huweza kuwa aidha vipashio vya kiisimu au mbinu za lugha. Vipashio vya kiisimu hujumuisha neno, vishazi, virai pamoja na sentensi huku mbinu za lugha zikiwa matumizi ya kinaya, matumizi ya chuku, taswira pamoja na sitiari. Vipengele hivyo vya kiisimu vinajadiliwa katika sura hii.

Vipashio vya kiisimu husaidia katika kujenga sentensi. Vipashio vinavyosaidia katika ujenzi wa sentensi ni pamoja na neno, kirai na kishazi. Sentensi iliyoundwa na vipashio hivi vya kiisimu vile vile huwa kipengele kimoja wapo cha kiisimu. Sura hii inachanganua vipashio vya kiisimu, ambavyo vinasaidia katika kufanikisha kanuni ya upole kwenye mawasiliano, hasa kupitia kwa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha utangazaji cha Redio Citizen.

#### **4.2.1 Neno**

Tungo huweza kufafanuliwa kama neno au maneno ambayo hutoa taarifa fulani, taarifa ambayo huweza kuwa kamili au isiwe kamili. Neno huwa kipashio kidogo sana cha lugha. Vile vile, neno huweza kuwakilisha maana katika sarufi ya lugha, maana ambayo hukubalika na watumizi wa lugha. Neno vile vile, huwa kipengele cha kiisimu ambacho huundwa na mofimu moja au zaidi.

Maneno huweza kuainishwa na uainishaji wa maneno, hutegemea sifa za maneno yale, pamoja na matumizi ya maneno hayo kisarufi. Kupitia kwa uainishaji wa maneno kisarufi, wazungumzaji na wasikilizaji wao huweza kuibuka na makundi ya maneno. Makundi ya maneno yanayoibuka huweza kuwa nomino, vitenzi, vivumishi, viashiria, vielezi na vinginevyo. Kwa mfano, neno ‘elnino’ ambalo limetumika na Luchivia linaingia katika kundi la kionyeshi kwa sababu linaashiria wingi wa ufasidi uliokithiri nchini Kenya.

Ni muhimu kutambua kuwa maneno huwa na umuhimu mkubwa katika lugha. Lugha huwa chombo cha mawasiliano na neno huwa kipashio kidogo sana cha lugha. Hivyo, katika mawasiliano ya binadamu ya kila siku, neno lazima litumike kwani ni vigumu kuendesha shughuli za kimaisha bila neno au maneno, ambayo hupangwa kwa utaratibu maalum ili yaweze kuibua maana inayohitajika.

Katika lugha, kuna maneno ambayo huwa na uwezo wa kudhihirisha upole, hasa katika matamshi. Maneno hayo huchukuliwa kama ambayo yanazingatia heshima kwa watumizi lugha pamoja na wasikilizaji, huku yakihakikisha kuwa mawasiliano yanaendelea kwa njia inayofaa.

Kuna utaratibu fulani ambao huweza kutumika katika mazungumzo ili kudhibitisha dhana ya upole katika mazungumzo hayo. Utaratibu huo hujulikana kama utaratibu wa ubadilishanaji, utaratibu ambao hufasiriwa kama matumizi ya neno au kipengele kingine chochote cha lugha, badala ya neno au kiungo kingine. Kwa mfano:



45. Luchivia: Gavana wa Bungoma amewatimua maafisa...

Mwala: Amewafukuza maafisa wake...

Kupitia kwa mfano wa arobaini na tatu unaotoka katika kipindi cha “Jambo Kenya” cha Redio Citizen, Luchivia anatumia neno ‘timua’ katika kauli yake, lakini Mwala katika kipindi hiki hiki anabadilisha neno hilo ‘timua’ kuwa ‘fukuza’. Hivyo, kuna matumizi ya utaratibu wa ubadilishanaji katika kauli hii. Hata hivyo, neno ‘timua’ kama anavyolitumia Luchivia, linadhihirisha upole kwa kiwango fulani, hivyo kuokoa nyuso za wale maafisa walioachishwa kazi, huku mazungumzo haya yakitimiza mahitaji yake.

46. Luchivia: Tuna elnino ya uhalifu nchini Kenya...

Wilbroda: Elnino hiyo Luchivia itatuletea balaa hapo mbeleni.

Luchivia kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya” anatumia maneno *elnino ya uhalifu*. Maneno haya *elnino ya uhalifu* yana maana ya uwingi wa kitu fulani, kitu hicho kikiwa uhalifu au hata ufisadi uliokithiri nchini Kenya. Maneno haya yanazua upole, pamoja na kudumisha uhusiano mwema baina ya mzungumzaji Luchivia pamoja na wasikilizaji wake.

Luchivia anatumia maneno yaliyojaa upole katika matamshi yake. Kupitia kwa mfano wa arobaini na nne, Luchivia anatumia neno uhalifu badala ya neno uwizi. Neno uhalifu linadhihirisha upole wa kiwango cha juu katika mazungumzo hayo. Matumizi ya maneno katika mazungumzo huweza kuzua utata, au hata kutozua utata. Kwa mfano, mzungumzaji akitumia neno uwizi katika matamshi yake, uwezekano wa vita kutokea ni asilimia tisini na tano, ikilinganishwa na matumizi ya neno uhalifu, neno ambalo linaweza kufanya vita kuzuka kwa asilimia ishirini tu.

#### 4.2.2 Virai

Kama ilivyo neno, kirai ni kipashio cha kiisimu cha lugha, kipashio ambacho huwa na uwezo wa kufanikisha dhana ya matumizi ya maneno yenye upole katika mawasiliano yoyote. Massamba et al (2012) wanadai kuwa kirai huweza kufafanuliwa kama kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja, lakini ambacho hakina muundo wa kiima kiarifu. Kiima husimamia mtenda jambo huku kiarifu kikisimamia jambo linalotendwa.

Kirai huonyesha mahusiano yanayoweza kupatikana baina ya maneno. Mahusiano yaliyopo baina ya virai huwa yanadhihirika. Vile vile, mahusiano hayo ni ya asili katika lugha yoyote. Kwa hivyo, kirai huweza kufasiriwa kama fungu la maneno ambalo huwa na uhusiano, au ambalo hufungamana, ili kuleta maana maalum katika mawasiliano yoyote. Uainishaji wa virai huwa na msingi wake kwenye aina za maneno. Katika lugha ya Kiswahili, kunapatikana aina nane za maneno. Aina hizi nane za maneno huwa kiini cha uainishaji wa virai katika lugha ya Kiswahili.

#### **4.2.2.1 Aina za Virai**

Kuna aina tofauti tofauti za virai, aina zinazoibuka kutokana na mahusiano yaliyopo baina ya maneno. Hii inamaanisha kuwa, muundo wa kirai hujikita katika aina za maneno, aina za maneno zikiwa kiini cha uhusiano uliopo ndani ya vipengele vinavyounda virai hivyo. Virai-nomino na virai-vitenzi ndivyo vinadhihirika katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo cha Redio Citizen.

##### **4.2.2.1.1 Kirai –Nomino**

Muundo wa kirai-nomino hukitwa kwenye nomino pamoja na maneno ambayo huwa na uhusiano na nomino. Maneno yaliyo na uhusiano na nomino ni kiwakilishi na kivumishi. Nomino husimamia majina ya vitu, majina ambayo huwa muhimu katika sentensi kwani hutegemewa na muundo wa maneno mengine katika sentensi nzima. Kiwakilishi hutumika badala ya nomino, huku kivumishi kikitoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi chake.

47. Luchivia: Idadi ya waja wazito...

Kupitia kwa mfano wa 45 kutoka kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, matamshi ya Luchivia yanadhihirisha matumizi ya kirai – nomino. Maneno “Idadi ya waja wazito” ni kirai – nomino kilichoundwa na nomino pamoja na kirai kihusishi. Haya ni matamshi yanayoibua upole kwani badala ya kuwarejelea akina mama walio karibu kujifungua kama wenye mimba, Luchivia anawarejelea kama waja wazito.

48. Luchivia: Mswada huu wa ardhi ukipitishwa bungeni utaleta mwanya mkubwa...

Luchivia akiwa anazungumza kwenye kipindi cha “Jambo Kenya” anasema kuwa, kuna mswada wa ardhi ambao unataka kupitishwa bungeni na wale wabunge, na kuwa mswada huo

ukipitishwa, utakuwa kama upenyo wa unyakuzi wa ardhi. Luchivia katika matamshi yake anaonyesha jinsi ambavyo ardhi itanyakuliwa. Mwanja ni nomino na mkubwa ni kivumishi kinachoonyesha kimo cha upenyo huo.

Katika kutumia virai-nomino ‘waja wazito’ pamoja na ‘mwanya mkubwa’, Luchivia anadhihirisha kuwa kuna uwezo wa kutumia maneno yenye tasfida katika mazungumzo. Maneno yenye tasfida huwa na nia ya kudumisha na kukuza mahusiano mazuri pamoja na mitagusano kati ya watu tofauti tofauti.

#### **4.2.2.1.2 Kirai – Kitenzi**

Kirai – kitenzi hukitwa katika kitenzi pamoja na maneno ambayo huwa na uhusiano na kitenzi. Neno ambalo huwa na uhusiano na kitenzi ni kielezi. Kitenzi huwa sehemu kuu ya kiarifu, na huweza kunyambuliwa ili kuwakilisha hali mbali mbali za sarufi kama vile nafsi, wakati pamoja na kauli mbalimbali. Kitenzi huonyesha tendo linalotendeka au ambalo lishatendeka huku kielezi kikitoa dhana zaidi kuhusu kitenzi.

49. Luchivia: Idadi ya...wanaoaga dunia...

Luchivia kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya” anatumia kirai – kitenzi ‘aga dunia’ katika matamshi yake. Lazima ikumbukwe kuwa, Luchivia ana uhuru wa kutumia neno ‘kufa’ katika maongezi yake, lakini anaamua kutumia kirai – kitenzi ‘aga dunia’ kwa sababu kinaibua upole katika mazungumzo, ikilinganishwa na neno kufa, neno ambalo linachukiza kwa kiwango fulani.

Fungu hili la maneno ‘aga dunia’ linachukuliwa kama kirai – kitenzi kwa sababu kirai – kitenzi huweza kuundwa na kitenzi pamoja na nomino moja au zaidi. Neno ‘aga’ ni kitenzi ambacho kinamaanisha fariki au sema kwaheri, na dunia ni nomino ambayo inasimamia ulimwengu. Hivyo, kirai – kitenzi hiki kimetumika na Luchivia katika matamshi yake ili kudhihirisha upole.

50. Wilbroda: ...kwa sababu alizoea kubadilisha harufu ya hewa...

Wilbroda kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya” anaonyesha jinsi ambavyo matumizi ya kirai – kitenzi yanaweza kuibua upole. Badala ya kutumia neno ‘jamba’ ambalo huchukiza, Wilbroda anatumia kirai – kitenzi ‘badilisha harufu’. Badilisha ni kitenzi kinachomaanisha ‘geuza’ ilhali harufu ni nomino inayosimamia hewa ambayo imechanganyika na mnukio wa kitu fulani. Mnukio huweza kuwa nzuri au mbaya.



### 4.2.3 Vishazi

Kishazi ni kipashio kingine cha kiisimu ambacho huweza kuibua upole katika mawasiliano. Kishazi kama kipashio cha kiisimu ambacho kina uwezo wa kufanikisha matumizi ya upole katika mawasiliano, kinaweza kufafanuliwa kama fungu la maneno ambalo huwa na kiima na kiarifu au nomino na kitenzi katika sentensi kuu. Haya ni kwa mujibu wa Lyons (1968: 170). Kishazi ni tofauti na kirai kwani kirai ni fungu la maneno lisilo na kiima na kiarifu, ilhali kishazi kina kiima na kiarifu.

Kishazi kama kipashio cha kiisimu, huweza kupatikana ndani ya vipashio vingine ambavyo si lazima viwe sentensi. Baadhi ya vishazi vinavyopatikana ndani ya lugha huweza kutambuliwa vikiwa kwenye vipashio ambavyo huchukuliwa kuwa vidogo kimiundo. Lakini, lazima watumizi lugha watambue kuwa, kuna sheria za lugha ambazo hutumika katika kushusha hadhi kishazi, ndipo kiweze kupatikana ndani ya kipashio kilicho kidogo zaidi yake. Vipashio vidogo ambavyo huweza kubeba vishazi ni virai – vielezi pamoja na virai – nomino. Ikiwa jambo kama hili litatokea, virai – vielezi na virai – nomino kama vipashio vidogo ndivyo humiliki vishazi vinavyopatikana kwenye sentensi.

Kishazi kama fungu la maneno lenye muundo wa kiima kiarifu, na ambalo limo ndani ya sentensi huweza kufanikisha dhana ya upole katika mawasiliano. Fungu hili la maneno huweza kuibua upole wa kiwango fulani, hasa katika mazungumzo yanayoendelea baina ya mzungumzaji na msikilizaji wake. Kwa mfano, ikiwa mzungumzaji atasema:

51. Mzungumzaji: Mama yule aliyekuwa mja mzito amebarikiwa na watoto pacha...

Kutokana na kauli hii, tunaweza kuibuka na kishazi huru pamoja na kishazi tegemezi. Kishazi huru ni sehemu ya sentensi au fungu la maneno kwenye sentensi ambalo huweza kujisimamia kimaana ilhali kishazi tegemezi ni fungu la maneno ambalo haliwezi kujisimamia kimaana, na kuwa lazima fungu lingine la maneno liambatanishwe kwake ndipo liweze kuleta maana kamilifu. Ni muhimu kukumbuka kuwa sentensi hubakia kuwa na maana kamilifu hata ikiwa kishazi tegemezi kitatolewa. Kutokana na mfano uliopo hapo juu:

Kishazi huru:       Mama yule amebarikiwa na watoto pacha

Kishazi tegemezi: ...aliyekuwa mja mzito...

Vishazi hivi viwili vimeibua upole hasa katika matumizi yao. Katika fungu la maneno linalopatikana katika kishazi huru, neno ‘barikiwa’ limetumika badala ya neno ‘zaa’, kisha katika kishazi tegemezi, neno ‘mja mzito’ limetumika badala ya ‘aliyekuwa na mimba’. Kwa hivyo, maneno ‘zaa’ pamoja na ‘aliyekuwa na mimba’ yanachukiza au hayapendezi hivyo, mzungumzaji huyu ametumia kishazi katika kufanikisha dhana ya upole katika mazungumzo yake.

#### 4.2.4 Sentensi

Sentensi huwa tungo yenye maana kisarufi na ambayo hujitegemea kimaana. Maana kisarufi ni maana inayoibuka kutoka kwa maneno kulingana na jinsi maneno yale yametumika katika sentensi. Mahusiano pamoja na hali huweza kuathiri mikondo ya maana, hasa katika tungo nzima au sentensi.

Sentensi huweza kufafanuliwa kama kipashio kilicho kikubwa kimiundo na ambacho kinaibua maaana mahsusi. Sentensi huundwa na vipashio vingine vilivyo vidogo vidogo, vipashio hivyo vikiwa virai pamoja na vishazi. Hii inamaanisha kuwa tungo linaweza kuundwa au linaweza kuwa na miundo ya aina za virai, aina hizi za virai zikitumika pamoja na vishazi au virai na vishazi vinapounganishwa kisha kuibua tungo ambalo huwa na maana kamilifu na ambayo inaeleweka kwa watu wote.

Sentensi nzuri lazima iwe na uwezo wa kuibua maana bila kutegemea maneno mengine. Katika kuibua maana bila kutegemea maneno mengine, sentensi huleta ujumbe ulio kamili, ujumbe ambao hahuhitaji maneno mengine ili kuweza kujisimamia kimaana. Sentensi hutoa dhana tofauti tofauti. Dhana zinazoibuliwa na sentensi ni pamoja na taarifa, swali, ombi au rai, amri au hata hali ya mshangao.

Kutunga na kutumia sentensi iliyo sahihi hutegemea ujuzi alionao mtumizi lugha kuhusu sarufi. Ujuzi wa kisarufi humwezesha mtumizi lugha kutoa mawazo mapya kutoka bongo na kuyatumia mawazo hayo kila mara katika maongezi yake. Mtumizi lugha kwa hivyo, ana uwezo wa kutambua ikiwa sentensi aliotunga ni sahihi au si sahihi. Kwa mfano:

52. Wilbroda: Miguu yako imening’inia kitini.

Mwala: Nayafahamu hayo.

Sentensi hii inayotumika na Wilbroda kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya” inaibua upole huku ikipitisha ujumbe kamili. Ujumbe unaopitishwa katika sentensi hii ni kuwa, Mwala ni mfupi, hivyo akiketi kwenye kiti, miguu yake haiwezi kufika sakafuni bali inaning’inia. Dhana ya upole inayoibuka kwenye kauli ni kuwa, Wilbroda hamwambii Mwala moja kwa moja kuwa yeye ni mfupi, bali anateua maneno ambayo hayamkwazi Mwala.

Yule asiyefahamu kuwa Mwala ni mfupi atafikiria kuwa, Mwala ameamua kushikilia miguu yake kwa juu ili isiguse sakafu. Sentensi hii imeweza kufanikisha matumizi ya upole katika mazungumzo haya yanayoendelea kati ya Wilbroda na Mwala kwenye kipindi cha “Jambo Kenya”.

### **4.3 Uteuzi wa Mbinu za Lugha katika Kuibua Upole**

Pamoja na vipengele vya kiisimu vilivyojadiliwa hapo juu, kuna mbinu za lugha ambazo zinatumika katika vipindi “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”. Mbinu za lugha zinapotumika katika matamshi, husaidia katika kupamba lugha, pamoja na kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyoleta mkwaruzano.

Mbinu za lugha vile vile, huweza kutumika katika kuibua upole. Hii ni kwa sababu mbinu za lugha hutumia maneno yenye maana fiche, huku zikidhamiria kutotaja mambo moja kwa moja. Kutotajwa kwa mambo kwa njia wazi huweza kuibua upole kwa kiwango fulani. Mbinu za lugha zinazopatikana katika vipindi “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” ni kama zinavyochunguzwa katika sehemu zinazofuata.

#### **4.3.1 Matumizi ya Kinaya kwenye Mawasiliano**

Matumizi ya maneno yenye kinaya katika mazungumzo huweza kudhihirisha upole kwa kiwango fulani. Kinaya huweza kufafanuliwa kama stihizai. Stihizai ni hali ya kufanyia mtu mzaha au kumkejeli mtu. Kinaya vile vile huweza kuwa harakati ya kutenda au hata kusema mambo kinyume cha vile inavyotarajiwa na wengine. Matumizi ya kinaya huhifadhi nyuso za wazungumzaji pamoja na wasikilizaji katika mazungumzo. Kinaya huweza kutumika kwa njia ya kutosema jambo fulani moja kwa moja. Hii hufanywa ili kuhifadhi nyuso za wazungumzaji pamoja na wasikilizaji. Kwa mfano:

53. Mzungumzaji: Hapa kuna mtu anatuchukulia vitu vyetu



Msikilizaji: Nakubaliana na wewe. Jana alichukua kalamu yangu, leo amechukua penseli yangu.

Kwa kusema hivi, mzungumzaji anamaanisha kuwa kuna mwizi katikati yao lakini, hataki kuudhuru uso wake kwa kumwambia moja kwa moja kuwa yeye ni mwizi, hivyo, anatumia maneno yenye kinaya katika kauli yake. Kwa kiwango fulani, kutumia neno ‘kuchukua’ kunaibua upole kukilinganishwa na matumizi ya neno ‘kuiba’, neno ambalo linaweza kuzua mabishano kati ya wale wanaohusika katika mazungumzo.

54. Mwala: Kule Turkana watu wameamua kutumia punda kama ambulensi. Wametafuta njia mwafaka ya kuwafikisha wagonjwa hospitalini.

Luchivia: Bora wawe na uhai...

Kupitia kwa mfano huu unaotoka katika kipindi cha “Jambo Kenya”, Mwala anasema kuwa watu wanaoishi sehemu za Turkana wameamua kufanya kinyume na matarajio kwa kutumia punda kama ambulensi. Mwala anaonyesha jinsi ambavyo serikali haijatia maanani mahitaji ya walioko Turkana kwa kutohakikisha kuwa kuna ambulensi za kutosha, za kuwahudumia wagonjwa katika kaunti hiyo ya Turkana. Punda katika mazungumzo haya linasimamia chombo cha usafiri kinachotumika na watu wa kaunti ya Turkana. Kwa hivyo, Mwala analifanyia mzaha swala hili la kutumika kwa punda badala ya ambulensi.

55. Wilbroda: Nataka kuambia wale ambao wamependa kubadilisha harufu ya hewa wakiwa mjini kuwa watafukuzwa alivyofukuzwa mtu katika kaunti moja humu nchini.

Luchivia: Unamaanisha nini Wilbroda?

Wilbroda kupitia kwa mfano huu kutoka kwa kipindi cha “Jambo Kenya” anasema kuwa katika kaunti moja, kaunti ambayo hajataja jina lake, alifukuzwa mtu mjini kwa sababu alizoea kubadilisha harufu ya hewa. Wilbroda anatumia maneno haya kuonyesha kuwa, yule mtu ana tabia ya kutoa ushuzi kila mara. Hivyo, Wilbroda hasemi jambo hili moja kwa moja. Maneno yake Wilbroda yanadhihirisha upole kwa sababu ya maneno yaliyojaa tasfida ambayo yametumika.

56. Jerida: Inastaajibisha kuwa wasichana siku hizi hawavai shimizi. Baada ya kuvaa kifuniko cha asali, basi tosha!

Syombua: Wanasema hiyo ndiyo fashoni.

Jerida anapozungumzia swala la wasichana kutovaa vizuri nyakati hizi kwenye kipindi cha “Chapa Kazi”, anasema kuwa baada ya kuvaa “Kifuniko cha asali”, wasichana huamua kuwa hiyo inatosha na kuwa, nguo zingine kama vile shimizi na nguo ndefu hazina umuhimu wowote. Jerida anamaanisha kuwa wasichana huvaa kocho pekee na kukosa kutia maanani uzito au uwepesi wa nguo ambazo pengine zinahitaji kuwa, waweze kuvalia shimizi ili kuficha uchi wao.

Hivyo, Jerida kupitia kwa kipindi cha “Chapa Kazi” anatumia maneno yake kwa njia fiche ili kuhakikisha kuwa wasikilizaji wake hawachukizwi na matamshi yasiyozingatia swala la kuwepo kwa heshima katika mazungumzo yoyote. Kifuniko cha asali kama anavyotumia Jerida kinasimamia kocho.

#### **4.3.2. Matumizi ya Sitiari Katika Kuibua Upole**

Sitiari hutumiwa kuashiria kitu ambacho hakihusiani na neno fulani, na ambacho hutumika katika mazungumzo ambayo yanaendelezwa. Sitiari hutoa ulinganisho wa kitu kimoja na kingine chenye sifa sawa nacho, moja kwa moja bila kutumia vihusishi vilinganishi. Sitiari huweza kuzua upole inapotumika katika mazungumzo. Hii ni kwa sababu mambo mengine hayatajwi moja kwa moja, bali yanaachiwa jukumu la kuchora picha akilini mwa wasikilizaji.

57. Wilbroda: Wajua wengine wetu wataamua kuacha kazi pindi tu watakapoombwa vyeti vyao vya shule ya upili na msingi.

Luchivia: Kweli kabisa, lakini kumbuka kuwa binadamu wengi ni sungura...

Kupitia kwa mfano huu unaotoka kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, Wilbroda katika mazungumzo yake, mazungumzo yanayotoka katika kipindi cha “Jambo Kenya” anasema kuwa, wengine kati yao wakiambiwa wapeleke vyeti vyao vya shule ya upili katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen ili viweze kukaguliwa, wengine kati yao wataamua kuacha kazi. Wilbroda katika matamshi yake anaonyesha kuwa baadhi ya watu hawakupita mtihani hata ingawa wameweza kupata ajira katika sekta mbali mbali humu nchini.

Luchivia analinganua watu na sungura katika kauli yake. Anachomaanisha Luchivia ni kuwa watu wamekuwa wajanja kwa hivyo, hawawezi kupatikana wakiwa na vyeti vilivyo na alama ya chini. Anachomaanisha Luchivia ni kuwa, watu wengine hutia juhudi na kununua vyeti vinavyoonyesha kuwa walipita mtihani wao. Luchivia kwa hivyo, anafananisha watu na sungura lakini maneno yake yana upole hivyo hayaleti mgongano.



Mkakati huu wa kutumia maneno yenye maneno fiche huibua upole katika mawasiliano na kujitenga na mkwaruzano. Hata hivyo, mkakati huu huwa na athari zake kwa sababu msikilizaji huachiwa jukumu la kufasiri ujumbe jinsi appendavyo na pengine kwa kutoa fasiri ya ujumbe uliojaa mafumbo, msikilizaji huenda akatoa tafsiri isyokuwa na maana iliyokusudiwa na mzungumzaji, hivyo msemaji huenda akakosa kufikia malengo yake.

#### 4.3.3 Matumizi ya Taswira

Taswira ni picha ambayo humjia mtu akilini wakati anaposoma, anapotazama au hata kusikiliza kazi fulani. Taswira huweza kufumbata maana fiche au hata maana ya kijazanda. Mbinu hii ya lugha inaweza kutumika katika kukuza mahusiano kati ya wazungumzaji na wasikilizaji wao. Hii ni kwa sababu mbinu hii huweza kuibua upole kwa kiwango fulani katika mawasiliano.

58. Wilbroda: Miguu yako imening'inia kitini.

Mwala: Nayafahamu hayo.

Luchivia: Nani hafahamu kuwa miguu ya Mwala huning'inia aketipo kitini?

Kupitia kwa mfano huu, Wilbroda katika kipindi cha “Jambo Kenya” cha kituo cha Redio Citizen anamwambia Mwala kuwa miguu yake huning'inia kila anapoketi kwenye kiti. Hili linamaanisha kuwa Mwala ni mfupi sana. Kwa hivyo, Wilbroda anajaribu kuokoa uso wa Mwala kwa kutumia maneno teule yanayochora picha akilini mwa wasikilizaji. Kule kuning'inia kwa miguu ya Mwala anapoketi kitini kunachora picha akilini mwa msikilizaji, picha ya jinsi alivyo mfupi Mwala.

59. Luchivia: Marufuku imetolewa kwa wakaazi wa Meru kutosafirisha miraa.

Mwala: Luchivia hiyo ni kumkataza mtoto kunyonya matiti ya mama yake.

Mwala katika kipindi cha “Jambo Kenya” anatolea swala hili la matumizi ya taswira ithibati anaposema kuwa, wakaazi wa Meru wamekatazwa kunyonya matiti ya mama zao. Mwala anasema haya Luchivia anapozungumzia swala la kupigwa marufuku kwa miraa kusafirishwa kutoka Meru hadi Somali. Mwala analinganisha kusafirishwa kwa miraa na maziwa yatokayo kwenye matiti ya mama. Picha inayotujia akilini ni umuhimu wa biashara ya kuuza miraa kwa wakaazi wa Meru kama ilivyo maziwa yatokayo kwenye titi la mama kwa mtoto wake.



60. Wilbroda: Wajua wengine wetu wataamua kuacha kazi pindi tu watakapoombwa vyeti vyao vya shule ya upili na msingi.

Luchivia: Kweli kabisa, lakini kumbuka kuwa watu ni sungura...

Kupitia kwa mfano huu, Wilbroda katika mazungumzo yake, mazungumzo yanayotoka katika kipindi cha “Jambo Kenya” anasema kuwa, wengine kati yao wakiambiwa wapeleke vyeti vyao vya shule ya upili katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen ili viweze kukaguliwa, wengine kati yao wataamua kuacha kazi.

Wilbroda katika matamshi yake anaonyesha kuwa baadhi ya watu hawakupita mtihani hata ingawa wameweza kupata ajira katika sekta mbali mbali humu nchini. Hivyo, Wilbroda anachagua maneno yake na kuhakikisha kuwa maneno aliyoyateua yanadhihirisha upole huku yakichora picha akilini mwa wasikilizaji, picha ya wafanyikazi wengine walivyofeli katika mitihani.

#### **4.3.4 Matumizi ya Chuku**

Chuku ni hali ya kutia chumvi kwenye kauli. Chuku ni mbinu ambayo kwayo habari zisizo za ukweli huweza kongezwa kwenye maneno ili kuweza kufanya mazungumzo yavutie. Chuku huweza kutumika katika kuibua upole kwenye mawasiliano.

61. Wilbroda: Miguu yako imening’inia kitini.

Luchivia: Nani hafahamu kuwa miguu ya Mwala huning’inia aketipo kitini?

Kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, picha unachorwa akilini mwa wasikilizaji ya jinsi alivyo mfupi Mwala, tunapata kutambua matumizi ya chuku. Hii ni kwa sababu, hata akiwa mfupi wa kimo, miguu yake haiwezi kuning’inia kitini jinsi anavyosema Wilbroda. Kuning’inia kwa miguu ya Mwala inaweza kufasiriwa kuwa kimo chake kinaweza kufananishwa na kile cha mtoto mdogo ambaye pengine ana umri wa miaka mitatu au hata minne. Licha ya kuwa Mwala ni mfupi, ufupi wake unatiwa chumvi kupitia kwa kauli hii.

#### **4.4 Hitimisho**

Ni dhahiri kuwa, kuna vipengele vya kiisimu ambavyo vinajitokeza katika vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen, hasa kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya”, ambacho kimefanyiwa uchunguzi. Vipengele hivyo vya kiisimu ni pamoja na

neni, virai, vishazi na sentensi. Mbinu za lugha pia zimejadiliwa katika sura hii. Dhana ya vipashio vya kiisimu ambavyo vimejadiliwa katika sura hii, vimedhibitisha kuwa, upole huweza kufanikishwa na matumizi ya vipengele hivi vya kiisimu, ili kufanya mawasiliano kutimiza malengo yake, lengo moja likiwa kupitisha ujumbe kwa njia inayotosheleza.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.1 Utangulizi

Data ya utafiti huu imechanganuliwa katika sura ya tatu na sura ya nne ya tasnifu hii. Data ambayo imechanganuliwa imetolewa kutoka kwa vipindi viwili vilivyoteuliwa kutoka kwa kituo cha utangazaji cha Redio Citizen. Sura ya tano ya tasnifu hii hivyo inatoa maelezo kwa kifupi kuhusu ikiwa malengo ya utafiti huu yameafikiwa au hayakuafikiwa. Vile vile, sura hii inaangazia changamoto pamoja na mapendekezo ambayo yanaweza kuwasaidia watafiti wengine ambao, hapo baadaye, watachunguza swala la upole kwenye vituo vya utangazaji katika tafiti zao.

### 5.2 Muktasari wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

1. Kubainisha mikakati ya upole inayotumika katika mazungumzo na vipindi vya salamu.
2. Kubainisha jinsi kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) zinafanikisha lengo la mikakati ya upole katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”, vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha Redio Citizen.
3. Kuchanganua elementi za lugha zinazofanikisha matumizi ya upole kwenye mawasiliano ya vipindi vya Redio Citizen.

Kubainisha mikakati ya upole inayotumika katika mazungumzo na vipindi vya salamu kama lengo la kwanza la utafiti huu, imejadiliwa katika sura ya pili ya tasnifu hii. Sura ya pili ya tasnifu hii imejenga msingi wa sura zingine za tasnifu hii kwa kuchunguza kijumla nadharia ya upole. Sura hii vile vile imeonyesha wanaisimu mbali mbali waliochunguza jinsi upole unaweza kutumika katika mawasiliano pamoja na mitazamo yao kuhusu dhana ya upole kijumla.

Kupitia kwa sura hii ya pili, imebainika kuwa, kuna mikakati ya upole ambayo hutumika na wazungumzaji pamoja na wasikilizaji wao katika kukabiliana na kauli ambazo huwa tishio kwa



nyuso za wanaohusika katika mazungumzo. Mikakati hiyo ya upole imebainika katika vipindi vilivyoteuliwa, na ambavyo vimeshughulikiwa katika tasnifu hii.

Sura ya tatu ya tasnifu hii imejadili lengo la pili la tasnifu hii, lengo hilo likiwa matumizi ya kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) katika kubainisha lengo la mikakati ya upole katika vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”, vipindi vinavyopeperushwa katika kituo cha Redio Citizen. Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) zimesaidia katika kufanikisha lengo la pili la utafiti huu, na kuthibitisha kuwa, kanuni za ushirikiano husaidia katika kutimiza malengo ya mawasiliano, moja wapo ya malengo hayo likiwa kupitishwa kwa ujumbe kwa njia inayotosheleza.

Kanuni za ushirikiano (Grice, 1975) ambazo zimejadiliwa katika sura ya tatu ni kanuni ya ukweli, kanuni ya idadi, kanuni ya namna au jinsi pamoja na kanuni ya uhusiano. Taratibu ambazo zinasaidia katika kuendesha lugha kwenye mawasiliano pia zimechunguzwa katika sura hii. Matumizi ya taadhima katika kuibua upole kwenye mawasiliano, utaratibu wa kibanta katika kuzua upole kwenye mazungumzo, matumizi ya takrima kama mkakati wa upole, matumizi ya tasfida katika kuleta mapatano kwenye mazungumzo, kujitweza katika kuleta maridhiano pamoja na ufundi wa maneno katika kuhakikisha ushirikiano kwenye mazungumzo ndizo taratibu za kuendesha lugha ambazo zimeshughulikiwa katika sura ya tatu ya tasnifu hii.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha uteuzi wa elementi za lugha katika kufanikisha upole kwenye mawasiliano. Kuna vipengele vya kiisimu vinavyosaidia katika kuhakikisha kuwa mawasiliano au mazungumzo yanaendelea kwa njia inayofaa. Vipengele hivyo vya kiisimu vinapatikana ndani ya lugha navyo ni neno, virai, vishazi pamoja na sentensi nzima. Dhana hii ya vipengele vya kiisimu imejadiliwa katika sura ya nne ya tasnifu hii.

Imebainika wazi kuwa, vipengele vingine kati ya hivi vinne, vina vipashio au vijaiina vyao, ambavyo vinasaidia katika kuhakikisha kuwa mawasiliano yanaendeshwa kwa njia inayotosheleza. Kwa mfano, ndani ya kipengele cha kiisimu kijulikanacho kama kirai, kuna kirai – nomino pamoja na kirai – kitenzi huku kishazi kikiwa na kishazi huru pamoja na kishazi tegemezi. Vijaiina hivi vya vipengele hivi vya kiisimu pia vimejadiliwa katika tasnifu hii. Sura hii ya nne vile vile imechunguza mbinu za lugha ambazo zinaweza kutumika katika kuibua upole

kwenye mawasiliano. Mbinu hizo za lugha zinazoibua upole katika mazungumzo ni kinaya, sitiari, taswira na chuku.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Tasnifu hii imebainisha mikakati ya upole ambayo inatumika katika vituo vya utangazaji, hasa kituo cha utangazaji cha Redio Citizen. Vipindi viwili ambavyo vimefanyiwa uchunguzi ni kipindi cha “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya Redio Citizen. Imedhihirika kuwa kuna mikakati ya upole ambayo hutumika ili kuokoa nyuso chanya au nyuso hasi za wale wanaohusika katika mazungumzo.

Kuna kauli ambazo hutisha nyuso za wazungumzaji na wasikilizaji katika mawasiliano yoyote, kauli ambazo hufanya mawasiliano kukatika na kutotimiza malengo yake. Lakini ni dhahiri kuwa, kauli kama hizi za kutisha nyuso huweza kukwepwa katika mazungumzo yoyote kupitia kwa matumizi ya maneno yenye upole, kama ilivyobainishwa na wazungumzaji wa vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi”.

Utafiti huu vile vile umebainisha kuwa, mzungumzaji huweza kunyamazia anachokifahamu ikiwa anashuku kuwa, kusema jambo hilo linaweza kuleta mkwaruzano kwenye mawasiliano. Katika kutowasilisha taarifa, mzungumzaji au msikilizaji huwa na nia ya kudumisha amani, pamoja na kuhakikisha kuwa uhusiano mwema unadumu miongoni mwa watu wanaoshiriki katika mazungumzo.

Vile vile, utafiti huu umeweza kubainisha kuwa, wazungumzaji katika vipindi vya “Jambo Kenya” na kile cha “Chapa Kazi” huafikiana na wasikilizaji wao katika mazungumzo. Makubaliano kati ya wazungumzaji na wasikilizaji yanadhihirika wakati ambapo mmoja kati ya wanaohusika katika mazungumzo anaamua kumwachia mwenzake nafasi ya kutoa kauli hata ikiwa amemkatiza mwenzake kauli.

Vile vile wazungumzaji hao hutumia mbinu ya ucheshi katika kuwasilisha taarifa ambayo huweza kumkwaza msikilizaji. Hii ni kwa sababu mbinu ya ucheshi hupunguza makali ya maneno ambayo huweza kuchukuliwa kama yale yanayowakwaza wasikilizaji.

Wazungumzaji huepuka dhana ya kutokubaliana katika mazungumzo yao. Wazungumzaji huepuka kutokubaliana katika mazungumzo ili kudhihirisha dhana ya upole unavyoweza



kutumika katika mawasiliano yoyote. Kinaya, sitiari, chuku pamoja na taswira hutumika katika vipindi hivi viwili ili kuonyesha jinsi ambavyo kanuni ya upole inaweza kutumika katika kufanikisha malengo ya mawasiliano.

Mazungumzo kwenye vipindi vya “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” yanadhihirisha sifa za kanuni za ushirikiano zilizopendekezwa na Grice (1975), kanuni ambazo hudhamiria kuibua upole katika mazungumzo, huku zikihakikisha kuwa, mazungumzo yanaendelea kwa njia inayofaa. Watangazaji katika vipindi hivi viwili vya kituo cha utangazaji cha Redio Citizen hutumia kanuni hizo za ushirikiano, zikiwemo kanuni ya ukweli, kanuni ya uhusiano, kanuni ya idadi pamoja na kanuni ya jinsi au namna. Hili limebainika kupitia kwa baadhi ya mifano iliyotolewa katika sura ya tatu ya tasnifu hii.

Kaida za upole za Leech (1983) vile vile, zimesaidia katika kudhibitisha kanuni za upole zinazotumika katika kituo cha utangazaji cha Redio Citizen, hasa kupitia kwa vipindi viwili vilivyoteuliwa. Matumizi ya kaida ya kusifu ambayo huhakikisha kuwa sifa zinawaendea wasikilizaji, kaida ya huruma ambayo hudhamiria kumrehemu msikilizaji, kaida ya kujitweza ambayo hutoa ufafanuzi wa mzungumzaji kujidunisha mbele ya msikilizaji wake imethibitika katika vipindi hivi viwili.

Matumizi ya kaida ya kukubaliana au makubaliano imedhihirika kupitia kwa kipindi cha “Jambo Kenya”. Kaida hii ya makubaliano hutahadharisha wale ambao wanashiriki katika mazungumzo kuepukana na kutokubaliana, ili kutofanya mazungumzo kuendelea kwa njia isiyofaa, au hata kuleta utata katika mazungumzo hayo. Bila shaka, mifano iliyotolewa katika tasnifu hii ni ithibati tosha kuwa, kanuni ya upole hudhihirika kwenye kituo cha utangazaji cha Redio Citizen, hususan kupitia kwa vipindi “Jambo Kenya” na “Chapa Kazi” vya kituo hicho.

#### **5.4 Mapendekezo**

Kupitia kwa matokeo ya utafiti huu, mtafiti anatoa mapendekezo kuwa:

Kwanza, uchunguzi zaidi kuhusu dhana ya upole uweze kufanywa katika kituo hiki cha Redio Citizen hasa kwa kuangazia vipindi vingine ambavyo havikufanyiwa utafiti, ili kuweza kubainisha ikiwa watangazaji wote wa kituo hiki hutumia kanuni ya upole katika matangazo yao.



Pili, tafiti hizo ziweze kuonyesha umuhimu wa kutumia kanuni ya upole katika mawasiliano yoyote pamoja na kiwango cha matumizi ya mikakati ya upole katika vipindi hivyo tofauti tofauti.

## Marejeleo

- Brown, P. & Levinson, S. (1978). Universals in Language Use: Politeness phenomena. In E.N. Goody (ed.). *Questions and Politeness*. Cambridge:Cambridge University Press.
- Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politeness: Some universals in Language usage*. Cambridge: Cambridge University Press
- Coates, J. (2004). *Women, Men and Language* 3rd ed. Great Britain : Pearson Education Limited
- Cutting, J. (2008). *Pragmatics and Discourse: A resource book for students*. London:Routledge
- Fraser, B. (1990). Perspectives on Politeness. In *Journal of Pragmatics*14: 232
- Gee, J. p. (2005). *An introduction to Discourse Analysis.Theory and Method*. 2nd ed. New York : Routledge
- Goffman, E. (1967). *Interaction Ritual; Essays on face-face behavior*. Garden city, NY: Doubleday.
- Grice, H.P. (1975). Logic and Conversation. In Peter Cole & Jerry Morgan (eds.). *Syntax andSemantics*, volume 3: *Speech Acts*. New York, NY: Academic Press.
- Leech, G. (1983). *Principles of Politeness*. London: Longman
- Lyons, J. (1968) *Introduction to Theoretical Linguistics*. London: Cambridge University Press.
- Massamba, D.P.B.et al. (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar-es-Saalam,
- Mills, S. 2003. *Gender and Politeness*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Thimm, C., Koch, S.C. & Schey, S. 2004. Communicating Gendered Professional Identity : Competence, Cooperation & Conflict in the work place, in Holmes, J. & Meyerhoff, M. (ed.).*The handbook of Language and Gender*. UK: Blackwell Publishing.
- Tolson, A. 2006. *Media Talk. Spoken Discourse on TV and Radio*. Edinburgh University Press
- TUKI (2006) *Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili*. Toleo la Tatu. Dar-es-saalam: TUKI

## **Kiambatisho A**

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Jambo Kenya” – Tarehe 14, Agosti 2016**

A<sup>1</sup> Luchivia: Nakumbuka mama yangu akiniambia hadithi kuhusu walivyokuwa wakiaga dunia wanawake waliokuwa katika harakati ya kujifungua lakini naona mambo yamebadilika. Wakati huu idadi ya wajawazito wanaoaga dunia nchini Kenya imeenda chini kwa sababu ya huduma wanayopata kutoka hospitali zetu.

A<sup>2</sup> Wilbroda: Mwala yeyote anayeendeleza ufisadi nchini Kenya anaachishwa kazi. Ringera ameamua kuwatimua majaji waliojawa na virusi vya ufisadi. Sasa hawana kazi tena. Ole wao!

A<sup>3</sup> Luchivia: Awilo

Wilbroda: Sema kigogo

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Jambo Kenya” – Tarehe 18, Agosti 2016**

A<sup>4</sup> Mwala: Wanafunzi siku hizi wamekosa nidhamu. Nakumbuka wakati nilikuwa nikisoma hata mwalimu sikutaka kukutana naye kwa sababu walimu walikuwa wakali kweli kweli lakini jana mtoto katika kaunti moja humu nchininalifukuzwa shuleni kwa sababu alipigana na mwalimu. Mambo ya kiajabu yanatendeka humu nchini.

Luchivia: Wajua watoto wetu wamekosa nidhamu shuleni kwa kuwa wengi wao wamejiingiza katika unywaji wa pombe haramu. Wazazi pia wanaweza kulaumiwa kwa hayo yanayotendeka kwa sababu wao ndio wanawapa watoto wao pesa nyingi.

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Jambo Kenya” – Tarehe 21, Agosti 2016**

A<sup>5</sup> Wilbroda: Kigogo, hivi karibuni utanisaidia kumwambia mwala wimbo wa siku ya kuzaliwa kwake lakini Mwala kinachonishangaza ni kuwa unaongeza umri lakini urefu umeukataa. Miguu yako imening'inia kitini.

A<sup>6</sup> Luchivia: Lazima tuwapongeze viongozi wetu ambao hawataki kujihusisha na maswala ya ufisadi. Mwala wajua kuwa tuna elnino ya uhalifu nchini Kenya lakini pongezi kwake gavana wa Bungoma aliyewatimua maafisa wanaoshukiwa kutumia mali ya umma vibaya.

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Jambo Kenya” – Tarehe 2, Septemba 2016**

A<sup>7</sup> Mwala: Wajua uhai ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Kule Turkana watu wameamua kutumia punda kama ambulensi. Wametafuta njia mwafaka ya kuwafikisha wagonjwa hospitalini. Luchivia, hili ni jambo la kushangaza sana.



A<sup>8</sup> Wilbroda: Unajua kigogo, kuna watu ambao hupenda kuachilia hewa mahali popote. Nataka kuambia wale ambao wamependa kubadilisha harufu ya hewa wakiwa mjini kuwa watafukuzwa alivyofukuzwa mtu katika kaunti moja humu nchini. Mimi sitataja jina la kaunti hiyo lakini ninawapa onyo, msiseme Awilo hakuwaambia.

## **Kiambatisho B**

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Chapa Kazi” – Tarehe 12, Agosti 2016**

B<sup>1</sup> Syombua: Katika shule ya Longean kule Samburu ya kati, kuna wanafunzi ambao walibugia kemikali aina ya ethanol wakidhania ni pombe. Rajab Shabaan ambaye ni daktari katika hospitali ya rufaa ya Samburu amesema kuwa mwanafunzi wa miaka kumi na saba aliyelazwa anasema kuwa anahisi machungu tumboni. OCPD wa Samburu ya kati amesema kuwa mmoja wa wanafunzi hao alisema kuwa waliiba kemikali hiyo kutoka kwa maabara ya shule huku baadhi wakichanganya na soda ili kunywa na wengine wakabugia bila kuchanganya na kinywaji chochote kile. Wanafunzi wengine sita walitibiwa na kuruhusiwa kurejea nyumbani. Mwili wa mwanafunzi aliyeaga dunia ulipelekwa katika hifadhi ya rufaa ya Samburu.

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Chapa Kazi” – Tarehe 2, Septemba 2016**

B<sup>2</sup> Jerida: Ni vizuri wale wanaosimamia shule wahakikishe kwamba usalama wote shuleni umedhibitiwa. Isiwe kuwa watu wa nje wanatumia ‘advantage wanaenda shuleni ama kuna hitilafu ya nguvu za umeme.

Syombua: Unajua umeongea hivyo nikakumbuka kwamba kuna wakati ambapo wanafunzi walikuwa wakisoma na ‘pressure lamps’. Wanafunzi walikuwa wanawasha taa hizo vizuri bila kusumbua. Wakati huu ambapo tuna stima watu wasitumie wanafunzi vibaya.

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Chapa Kazi” – Tarehe 8, Septemba 2016**

B<sup>3</sup> Jerida: Niliyoyaona leo, sitayasahau. Macho yangu karibu yalinitoke. Inastaajabisha kuwa wasichana siku hizi hawavai shimizi. Baada ya kifuniko cha asali basi tosha!

Syombua: Aah nawe! Hujawahi sikia kuwa wasichana wanasema hiyo ndiyo fashoni ya sasa. Lazima utaelewa Jerida.

B<sup>4</sup> Jerida: Papa mtakatifu alituonyesha jinsi ambavyo tunafaa kuishi kama wanajamii. Ulimwona alivyokuwa akitekeleza majukumu yake, pamoja na wosia wake kwetu sisi kama wakristo

Syombua: Mimi nilipata funzo kutokana na kuzuru kwake Kenya. Maneno yake Papa Francis yalionyesha upendo wa dhati kwa waja wa Mungu. Kila mtu anafahamu

jinsi ambavyo wazazi hupatwa na machungu mabaya yanapowapata watoto wao. Hivyo ndivyo anavyohisi papa Francis wanyonge wanapokandamizwa.

### **Mazungumzo kutoka kipindi cha “Chapa Kazi” – Tarehe 15, Septemba 2016**

B<sup>5</sup>Msikilizaji: Mimi naupenda huo wimbo na kama waonelea kuwa huo wimbo si mtamu wacha tu, sina wimbo mwingine.

Jerida: Aah nawe, usiwe mtu wa kukasirika haraka hivyo. Syombua anakufanyia tu mzaha kwa hivyo usijali mama, Syombua atakuchezea wimbo huo baada ya muda mfupi.